



Uwanja wa Mpira wa KMC Complex wenye uwezo wa kubeba watu 6,000 uliojengwa kwa fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni

**Mji wa Serikali – Mtumba,
Mtaa wa TAMISEMI,
S.L.P 1923,
41185 DODOMA.**

**Simu: +255 26 232 1234
Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz
Tovuti: www.tamisemi.go.tz**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA
ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, MHESHIMIWA
MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB), KUHUSU
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI
KWA MWAKA 2025/26**





Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (katikati) akizindua Shule ya Wasichana ya Sayansi ya Mkoa wa Ruvuma ya Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa ziara yake mkoani humo



Wanafunzi wa Kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Sayansi ya Mkoa wa Geita wakifanya mazoezi kwa vitendo kwenye maabara



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiangalia urefu wa Daraja la Berega lililopo Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro, baada ya kulizindua wakati wa ziara yake mkoani humo



Muonekano wa Daraja la Berega lenye urefu wa Mita 140 lililopo Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA,
MHESHIMIWA MOHAMED OMARY MCHENGERWA
(MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI KWA MWAKA 2025/26**

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

VIONGOZI WAKUU



Mhe. Mohammed O. Mchengerwa (Mb)
Waziri wa Nchi OR – TAMISEMI



Mhe. Zainab A. Katimba (Mb)
Naibu Waziri – Elimu



Mhe. Dkt. Festo J. Dugange (Mb)
Naibu Waziri – Afya



Ndg. Adolf H. Ndunguru
Katibu Mkuu OR – TAMISEMI



Ndg. Atupele Mwambene
Naibu Katibu – Elimu



Ndg. Sospeter M. Mtwale
Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI



Eng. Rogatus H. Mativila
Naibu Katibu Mkuu – Miundombinu

YALIYOMO

SEHEMU YA KWANZA.....	1
1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Shukrani na Pongezi.....	2
1.2 Salamu za Pole.....	7
1.3 Majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI.....	7
SEHEMU YA PILI.....	10
2.0 Utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kuanzia Novemba, 2020 hadi Machi, 2025	10
2.1 Usimamizi na Uendeshaji wa Elimumsingi na Sekondari.....	11
2.2 Uratibu na Usimamizi wa Huduma za Afya ya Msingi.....	17
2.3 Huduma za lishe	22
2.4 Huduma za Ustawi wa Jamii	24
2.5 Ujenzi, Ukarabati na Matengenezo ya Barabara	28
2.6 Huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka.....	30
2.7 Utawala Bora, Kujenga Uwezo, Usimamizi wa Rasilimali, Ujenzi wa Majengo ya Utawala na Makazi ya Viongozi.....	32
2.8 Ulinzi wa Mazingira, uhifadhi wa Maliasili, Mabadiliko ya Tabianchi na Biashara ya Kaboni.....	35
2.9 Mamlaka za Serikali za Mitaa	36
2.10 Uendelezaji Miji.....	42
2.11 Uendelezaji wa Miji Midogo Inayochipukia..	44

SEHEMU YA TATU	46
3.0 Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Mafungu 28) Kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025	46
3.1 Vipaumbele vya Bajeti kwa Mwaka 2024/25	46
3.2 Ukusanyaji wa Kodi ya Majengo, Maduhuli na Mapato ya Ndani ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Mafungu 28) Mwaka 2024/25..	47
3.3 Taarifa ya Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo	48
3.4 Mafanikio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2024/25	49
3.5 Shughuli Zilizotekelezwa Kupitia Fedha za Mapato ya Ndani ya Halmashauri.....	50
3.6 Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024.....	54
3.7 Uratibu na Usimamizi wa Huduma za Afya ya Msingi	54
3.8 Usimamizi na Uendeshaji wa Elimumsingi na Sekondari.....	57
3.9 Utawala Bora, Usimamizi wa Rasilimali, Ujenzi wa Majengo ya Utawala na Makazi ya Viongozi	65
3.10 Usimamizi wa Mifumo ya TEHAMA	70
3.11 Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu	76
3.12 Huduma Ndogo za Fedha	77
3.13 Usimamizi wa Mazingira, Uhifadhi wa Maliasili na Mabadiliko ya Tabianchi.....	77

3.14	Uendelezaji Vijiji na Miji	78
3.15	Ujenzi, Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Wilaya.....	79
3.16	Huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka.....	86
3.17	Shirika la Masoko ya Kariakoo.....	87
3.18	Chuo cha Serikali za Mitaa.....	89
3.20	Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa.....	93
3.21	Tume ya Utumishi wa Walimu	95
	SEHEMU YA NNE.....	98
4.0	Makadirio ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26	98
4.1	Vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26 Fungu Namba 56.....	98
4.2	Vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26 Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Na. 2	100
4.3	Vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26 Mafungu 26 ya Mikoa ikijumuisha Halmashauri 184.....	101
4.4	Makadirio ya Kodi ya Majengo, Maduhuli na Mapato ya Ndani ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri Mwaka 2025/26	104
4.5	Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Mafungu 28) kwa Mwaka wa Fedha 2025/26	104
4.6	Makadirio ya Mpango na Bajeti ya Maendeleo ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI (Mafungu 28) kwa Mwaka 2025/26.....	105

4.7	Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI (Mafungu 28) kwa Mwaka 2025/26.....	105
4.8	Makadirio ya Makusanyo ya Kodi ya Majengo, Maduhuli na Mapato ya Ndani kwa Mwaka 2025/26.....	134
4.9	Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Mafungu 28) kwa Mwaka 2025/26.....	135

VIFUPISHO VYA MANENO

ACSEE	Advanced Certificate of Secondary Education Examination
AFCS	Automated Fare Collection System
AfDB	African Development Bank
AMREF	African Medical and Research Foundation
BRT	Bus Rapid Transit
CAMFED	Campaign for Female Education
CCM	Chama cha Mapinduzi
CDC	Centers for Disease Control and Prevention
CRDB	Cooperative and Rural Development Bank
CSEE	Certificate of Secondary Education Examination
D by D	Decentralization by Devolution
DANIDA	Danish International Development Agency
DART	Dar Rapid Transit Agency
EGPAF	Elizabeth Glaser Pediatric AIDS Foundation
Elmis	Electronic Logistic Management Information System
EMD	Emergence Medical Department
EP4R	Education Performance for Result
EU	European Union
FCDO	Foreign, Commonwealth & Development Office
FFARS	Facility Financial Accounting and Reporting System
FOCAC	Forum on China-Africa Cooperation
FTNA	Form Two National Assessment
GAVI	Global Alliance for Vaccine immunization

GIS	Geographical Information System
GiZ	German Agency for International Cooperation
GoTHOMIS	Government of Tanzania Health Operations Management Information System
GPE	Global Partnership for Education
HIV/AIDS	Human Immunodeficiency Virus/Acquired Immunodeficiency Syndrome
HJFMRI	Henry Jackson Foundation for the Advancement of Military Medicine, Inc
ICAP	International Center for AIDS Programs
ICU	Intensive Care Unit
ITS	Intelligent Transportation Systems
JICA	Japan International Cooperation Agency
KMC	Kangaroo Mother Care
KOFIH	Korea Foundation for International Healthcare
KOICA	Korea International Cooperation Agency
MEMKWA	Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa
MEWAKA	Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini
MSD	Medical Store Department
MSDQI	Medical Supply Distribution Quality Indicator
NIDA	National Identification Authority
NMB	National Microfinance Bank
O&OD	Opportunities and Obstacles to Development
PoS	Point of Sale
PSLEE	Primary School Leaving Examination

RISE	Roads to Inclusion and Socioeconomic Opportunities
RTI	Research Triangle Institute
SDC	Swiss Agency for Development and Cooperation
SEQUIP	Secondary Education Quality Improvement Project
SFNA	Standard Four National Assessment
SIDA	Swedish International Development Cooperation Agency
SRWSS	Sustainable Rural Water Supply and Sanitation
TACTIC	Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness
TAMISEMI	Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
TARURA	Tanzania Rural and Urban Roads Agency
TASUFIP	Tanzania Sustainable Finance Initiative Project
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
THPS	Tanzania Health Promotion Support
TMCHIP	Tanzania Maternal and Child Health Investment Program
TRC	Teacher Resource Center
TSC	Teachers' Service Commission
TSCMIS	Teachers Service Commission Management Information System
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
UMISSETA	Umoja wa Michezo ya Shule za Sekondari Tanzania
UNITASHUMTA	Umoja wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania
UN	United Nations

UNCDF	United Nations Capital Development Fund
UNDP	United Nations Development Programme
UNEP	United Nations Environment Programme
UNFPA	United Nations Population Fund
UNICEF	United Nations International Children's Emergency Fund
UPS	Uninterruptible Power Supply
USAID	United States Agency for International Development
UVIKO	Ugonjwa wa Virusi vya Korona
WFP	World Food Programme.
WHO	World Health Organization
WWF	World Wildlife Fund

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA,
MHESHIMIWA MOHAMED OMARY MCHENGERWA
(MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI KWA MWAKA 2025/26**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 Utangulizi

1. *Mheshimiwa Spika*, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ninaomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Fungu Na. 56); Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 02) na mafungu 26 ya mikoa, ikijumuisha halmashauri 184 kwa mwaka 2024/25. Aidha, ninaomba Bunge lako lijadili na kuidhinisha mpango wa utekelezaji, makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa ajili ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu na mafungu 26 ya mikoa ikijumuisha halmashauri 184 kwa mwaka 2025/26.

2. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa taarifa kuwa, hotuba hii itaonesha utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kwa kipindi cha kuanzia Novemba, 2020 hadi Machi, 2025. Aidha, hotuba hii ni ya mwisho katika utekelezaji wa: Mpango Mkakati wa

Ofisi ya Rais - TAMISEMI wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 pamoja na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; na Kipindi cha Kwanza cha Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

1.1 Shukrani na Pongezi

3. **Mheshimiwa Spika**, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunijalia kusimama mbele ya Bunge hili. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake wenye dira, maono na dhamira ya kuwaletea wananchi maendeleo kwa vitendo. Miongozo, maelekezo na usimamizi wake umeendelea kututia moyo sisi wasaidizi wake na tunamuahidi kufanya kazi bila kuchoka ili kuboresha maisha ya watanzania. Imekuwa heshima kwangu kuhudumu chini ya uongozi wake mahiri, na hakika amethibitisha kuwa, uongozi si nafasi bali ni jukumu la kusukuma mbele gurudumu la maendeleo.

4. **Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa nafasi ya urais kwa kipindi cha pili Awamu ya Sita kupitia Chama cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba, 2025, tunamuamini na tunaendelea kuamini ataendelea kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu. Aidha, nampongeza

Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa mgombea mwenza. Mwenyezi Mungu awape afya njema, hekima na maarifa katika kutekeleza majukumu yao.

5. **Mheshimiwa Spika**, ninaomba kuwashukuru waheshimiwa: Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati kwa uongozi wao thabiti na kujitolea kwa dhati katika kutimiza majukumu yao, pamoja na miongozo na maelekezo yao ya mara kwa mara yenye hekima na busara ambayo yemenisaidia sana katika majukumu yangu ya usimamizi wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali kwa ufanisi mkubwa.

6. **Mheshimiwa Spika**, kipekee ninaomba nikushukuru wewe binafsi, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, kwa kuliongoza Bunge kwa weledi na umahiri wa hali ya juu. Umeonesha uongozi bora kwa kuhakikisha majadiliano yenye tija yanakuwa msingi kwenye Bunge letu. Pia, ninampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kukusaidia kuendesha shughuli za Bunge. Vilevile, ninawapongeza Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama

(Mb.), Jimbo la Madaba, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb.), Jimbo la Njombe Mjini na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.), wa Viti Maalum kwa umakini wao wa kuliongoza Bunge lako.

7. **Mheshimiwa Spika**, Ninamshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Jimbo la Kilolo; Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Jafari Chege Wambura, Mbunge wa Jimbo la Rorya; Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge za: Hesabu za Serikali za Mitaa; Sheria Ndogo; Hesabu za Serikali; Uwekezaji Mitaji ya Serikali; Bajeti; na Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge. Ninawiwa kusema kazi zenu ni za thamani na zina mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa na ustawi wa wananchi.

8. **Mheshimiwa Spika**, ninawashukuru waheshimiwa mawaziri, naibu mawaziri, makatibu wakuu, naibu makatibu wakuu na watendaji wote wa wizara mbalimbali ambao wameendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kufanya kazi kwa pamoja ya kuwaletea maendeleo watanania. Ninathamini sana mchango wao, kwa pamoja tutaendelea kujenga taifa lenye nguvu na ustawi zaidi.

9. **Mheshimiwa Spika**, ninaomba kuwashukuru viongozi wenzangu na wataalamu wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Ninatambua mchango wao

katika kuhakikisha wananchi wanahudumiwa katika nyanja zote. Kipekee ninawashukuru: Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, Naibu Waziri anayeshughulikia afya na Mbunge wa Jimbo la Wanging'ombe, Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Naibu Waziri anayeshughulikia elimu na Mbunge wa Viti Maalum, Ndg. Adolf Ndunguru, Katibu Mkuu; Naibu Makatibu Wakuu: Ndg. Sospeter Mtwale (TAMISEMI), Mhandisi Rogatus Mativila (Miundombinu) na Ndg. Atupele Mwambene (Elimu); Mwl. Paulina Nkwama Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu; watendaji wakuu wa taasisi, wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa, wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri na watumishi wote.

10. ***Mheshimiwa Spika***, kipekee kabisa ninaendelea kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Rufiji kwa imani yao kwangu. Ninaendelea kuwaahidi kuwa nitafanya kazi bila kuchoka ili kutimiza ahadi ambazo tumeziweka kwa pamoja. Nitumie nafasi hii kuwaambia kuwa, mara zote ninapoiwaza Rufiji napata matumaini, imani, nguvu na ari ya kujitoa zaidi kwa mustakabali bora wa jimbo letu. Niwahakikishie, sichukulii dhamana waliyonipa kwa urahisi hata kidogo. Imani yao ni deni kwangu; sauti zao daima zitaongoza matendo yangu. Nitaendelea kuwahudumia kwa uadilifu, uwazi na uwajibikaji. Nawashukuru sana. Wahenga walisema, ***“Asiyekumbuka kwao ni mtumwa”***.

11. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki cha utumishi wangu kwa wananchi wa Rufiji na Taifa kwa ujumla, nimepata faraja na msukumo mkubwa kutoka kwenye kumbukumbu ya baba yangu mpendwa, ambaye alifariki dunia akiwa kwenye ibada tukufu huko Makka. Hii ni bajeti yangu ya kwanza kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu tangu kumpoteza baba yangu. Ni tukio lenye uzito wa kipekee katika maisha yangu ya uongozi, kwani kila hatua ya safari yangu katika utumishi wa umma imekuwa ikiambatana na maombi, ushauri, na baraka zake. Ingawa ni huzuni kubwa kumpoteza, maisha yake yamebaki kuwa dira yenye nguvu kwangu na kwa wengi waliomfahamu. Baba yangu alikuwa mtu wa maono, msimamo, heshima na hekima. Alinilea katika misingi ya maadili, kujituma, na kuheshimu kila mwanadamu – misingi ambayo imekuwa msingi wa uongozi wangu leo.

Alinihimiza kuwa kiongozi mwenye kusikiliza, mwenye kujifunza kila siku, na mwenye kumtanguliza Mungu katika kila hatua ya maisha. Maisha yake yalijaa ibada, kujitoa kwa jamii, na kusimamia haki hata katika mambo madogo. Haya yote yamekuwa nguzo imara ya mtazamo wangu wa kulihudumia Taifa kwa moyo wote.

12. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na huzuni ya kumpoteza, moyo wangu unafarijika na kujazwa nguvu kila ninapoyaona matunda ya kazi inayofanywa na ofisi ninayoiongoza chini ya

mwongozo wa Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mambo makubwa na ya kihistoria yanaendelea kufanyika – kutoka kwenye maboresho ya miundombinu, utoaji wa huduma kwa jamii, hadi mageuzi ya kimfumo yanayolenga kuleta maendeleo kwa wananchi wetu.

Kwa hiyo, japo Kifo chake kimeniacha na pengo kubwa moyoni, pia kimeniacha na kumbukumbu hai ya kiongozi wa kweli niliyemjua tangu utoto. Ni kumbukumbu inayonipa msukumo wa kuendelea kufanya kazi kwa bidii, kwa kujitoa, kwa uadilifu na kwa upendo kwa watu wangu – kwa sababu najua, kule aliko, angependa kuona mwanaye akiendeleza dhamira yake ya kuwatumikia watu kwa moyo mmoja.

1.2 Salamu za Pole

13. ***Mheshimiwa Spika***, natoa pole kwa Bunge lako kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, Mkoani Dar es Salaam na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika. Mwenyezi Mungu ampe pumziko la milele.

1.3 Majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI

14. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ina jukumu la kuratibu na kusimamia mafungu 28 yanayojumuisha: Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Fungu Na. 56) pamoja na Taasisi zilizo chini yake ambazo

ni Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini, Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka, Chuo cha Serikali za Mitaa, Shirika la Elimu Kibaha, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa na Shirika la Masoko ya Kariakoo; Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 02) na Mafungu 26 ya mikoa ikijumuisha halmashauri 184.

15. ***Mheshimiwa Spika***, maelekezo ya mgawanyo wa majukumu yaliyotolewa na Hati Idhini ya Rais (*Presidential Instrument*) ya tarehe 30 Agosti, 2023 yanaainisha majukumu ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kama ifuatavyo: -

- (i) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ugatuuji wa Madaraka (D by D), tawala za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa, maendeleo vijijini na mijini;
- (ii) Kuziwezesha tawala za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kutekeleza majukumu yake ya kisheria;
- (iii) Kuratibu shughuli za utoaji wa huduma mijini kama vile usafiri, usafirishaji na usafi wa mazingira;
- (iv) Kusimamia shughuli za Tume ya Utumishi wa Walimu;
- (v) Kusimamia shughuli za elimumsingi na sekondari;
- (vi) Kusimamia na kuratibu shughuli za utoaji wa huduma za afya ya msingi, ustawi wa jamii na lishe;

- (vii) Kuratibu na kusimamia mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika ofisi za wakuu wa mikoa, mamlaka za serikali za mitaa na taasisi;
- (viii) Kuwatambua na kuwaendeleza wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo;
- (ix) Kutambua vipaji na kuviendeleza;
- (x) Kujenga uwezo wa watumishi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, ofisi za wakuu wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa; na
- (xi) Kusimamia utendaji wa mashirika, taasisi, programu na miradi iliyo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

SEHEMU YA PILI

2.0 Utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kuanzia Novemba, 2020 hadi Machi, 2025

16. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka mitano (5) bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI pamoja na mafungu yake imekuwa ikiongezeka kutoka shilingi trilioni 7.01 Mwaka 2020/21 hadi shilingi trilioni 10.53 Mwaka 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 50.21. Ofisi ya Rais - TAMISEMI inamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa Serikali za Mitaa na kuziongezea bajeti. Hii inaonesha namna anavyowajali wananchi kwa kupeleka maendeleo kwa vitendo katika maeneo yao.

17. **Mheshimiwa Spika**, ongezeko hili si tu la fedha; ni ushahidi wa mabadiliko. Ni matumaini mapya kwa mwananchi wa taifa hili kupata huduma bora. Ni daraja jipya linalounganisha maendeleo na maisha ya kila siku. Ni shule mpya, zahanati, barabara, maji safi – na juu ya yote, ni heshima kwa utu wa mtanzania wa kawaida.

Leo hii, tunapopitia mafanikio haya, tunasema kwa sauti kubwa: Serikali ya Awamu ya Sita inatekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa

vitendo. Na sisi sote, kama wawakilishi wa wananchi, tunayo dhamana ya kuendeleza kasi hii – kwa mshikamano, uadilifu na moyo wa kizalendo. Tanzania mpya inawezekana – na inaendelea kujengwa mbele ya macho yetu!

18. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imetekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 katika maeneo yafuatayo;

2.1 Usimamizi na Uendeshaji wa Elimumsingi na Sekondari

19. ***Mheshimiwa Spika***, ibara ya 80 (a - j) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 inaelekeza: Kujenga na kukarabati miundombinu ya elimu pamoja na kuhifadhi na kuendeleza mazingira ya shule hizo; Kuendeleza Mpango wa Kutoa Elimu bila Ada kwa Shule za Msingi na Sekondari ili kuwawezesha vijana wenye sifa kuanza na kuendelea na masomo bila kikwazo; Kuhakikisha kuwa kila shule ya msingi inatoa elimu ya awali kwa ufanisi katika mazingira na miundombinu iliyoboreshwa; Kuimarisha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum; Kuimarisha ufundishaji wa Masomo ya Sayansi ya Hisabati, Fizikia, Kemia na Baiolojia na kuongeza upatikanaji wa walimu wa kufundisha masomo hayo; Kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji wa masomo ya stadi za kazi na lugha ikiwemo lugha za alama katika elimu

ya msingi; na Kuimarisha shule zote za michepuo ikijumuisha Elimu ya Ufundi, Kilimo na Biashara kwa kuzipatia vifaa vya kisasa.

20. **Mheshimiwa Spika**, elimu ni urithi wa kizazi – urithi usioharibika, usioibwa, na usiozeeka. Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano, aliweka msingi imara aliposema, **“Ni jukumu letu kuimarisha elimu ya ufundi na mafunzo ili vijana wetu wawe na ujuzi wa kukabiliana na ajira”**.

Kauli hii si tu kauli ya kisera, bali ni mwamko wa kiroho na kijamii – mwamko wa taifa linalojua kuwa maendeleo ya kweli hayaanzi na barabara wala majengo, bali na maarifa yaliyowekezwa kwa watu wake.

Mheshimiwa Spika, leo ninapowasilisha mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa upande wa Elimumsingi na Sekondari, ninatoa ushahidi wa mabadiliko ya kweli – mabadiliko ya shule zilizofufuliwa, walimu walioajiriwa, watoto waliowezeshwa, na matumaini mapya yaliyochipuka kila pembe ya nchi yetu. Kwa sababu katika taifa lenye maono, kila darasa linalojengwa si tu ukuta – bali ni mlango wa maisha mapya kwa mtoto wa kitanzania.

21. **Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza jukumu hilo, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani katika huduma ya elimu kama ifuatavyo:

- (i) Kujenga na kukarabati miundombinu ya elimu, ambapo kumekuwa na ongezeko la vyumba vya madarasa kutoka 191,708 hadi 254,393, sawa na asilimia 32.69; shule za msingi kutoka shule 16,406 hadi 17,986 sawa na ongezeko la asilimia 9.63; shule za sekondari kutoka shule 3,863 hadi 4,894 sawa na asilimia 26.68; ongezeko la matundu ya vyoo kutoka 206,670 hadi 278,911 (shule za msingi) sawa na asilimia 34.95; na kutoka matundu 92,724 hadi 120,970 (shule za sekondari) sawa na asilimia 30.43. Aidha, nyumba za walimu zimeongezeka kutoka 58,637 hadi 60,429 sawa na ongezeko la asilimia 3.05; maktaba kutoka 1,537 hadi 2,665 sawa na ongezeko la asilimia 73.38; maabara kutoka 8,072 hadi 8,710 sawa na asilimia 7.90; mabweni kutoka 2,245 hadi 3,245 sawa na asilimia 44.54; na mabwalo kutoka 871 hadi 1,004 sawa na asilimia 15.26. Vilevile, shule 868 zimekarabatiwa zikiwemo za msingi 794 na za sekondari 74;
- (ii) Kuendeleza Mpango wa Kutoa Elimu bila Ada kwa shule za msingi na sekondari ili kuwawezesha vijana wenye sifa kuanza na kuendelea na masomo bila kikwazo, ruzuku ya Elimu Bila Ada imeongezeka kutoka shilingi bilioni 249.66 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 484.27 mwaka 2024/25 kwa mwaka sawa na asilimia 93.97;

- (iii) Kutoa elimu ya awali katika shule za msingi kwa ufanisi katika mazingira na miundombinu iliyoboreshwa, idadi ya wanafunzi katika shule za awali imeongezeka kutoka 1,278,886 (wavulana 647,609 na wasichana 631,277) hadi 1,558,549 (wavulana 791,520 na wasichana 767,029) sawa na asilimia 21.87, na shule zenye madarasa ya awali zimeongezeka kutoka 16,355 hadi 18,011 sawa na asilimia 10.12;
- (iv) Kutoa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo uandikishaji umeongezeka kutoka 28,482 hadi 78,429 sawa na asilimia 175. Aidha, madarasa 44, matundu ya vyoo 132 na mabweni 172 yamejengwa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
- (v) Kufundisha Masomo ya Sayansi ya Fizikia, Kemia, Baiolojia na Hisabati na kuongeza upatikanaji wa walimu wa kufundisha masomo hayo. Idadi ya Wanafunzi wanaosoma Masomo ya Sayansi na Hisabati katika shule za sekondari kuanzia kidato cha tatu imeongezeka kutoka 2,497,450 hadi 2,792,584 sawa na ongezeko la wanafunzi 295,134;
- (vi) Ujifunzaji na ufundishaji wa masomo ya stadi za kazi na lugha ikiwemo lugha za alama katika elimu ya msingi ambapo walimu 127 wa lugha za alama wameajiriwa na kusambazwa katika shule 127;

- (vii) Imeboresha shule 28 za mchepuo wa elimu ya ufundi/amali kwa kuzikarabati na kutoa vifaa vya kisasa. Aidha, shule 274 za michepuo ya kilimo na 28 za michepuo ya biashara zimeboreshwa **(Kiambatisho Na.1)**;
- (viii) Kuajiri walimu 45,804 wakiwemo walimu 447 wa elimu maalumu;
- (ix) Kutoa mafunzo kazini kwa walimu 106,806 ikiwa ni pamoja na walimu 29,399 wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Teknolojia kwa lengo la kuimarisha ufundishaji wa masomo hayo;
- (x) Kununua na kusambaza vitabu vya kiada na ziada 66,553,455 kwa shule za msingi na sekondari;
- (xi) Kuandikisha wanafunzi wa Darasa la Kwanza ambapo uandikishaji umeongezeka kwa asilimia 14.87 kutoka wanafunzi 1,621,724 (wavulana 811,401 na wasichana 810,323) hadi 1,862,539 (wavulana 937,260 na wasichana 925,279), idadi ya wanafunzi katika shule za msingi za umma imeongezeka kutoka 10,460,785 hadi 10,739,975 sawa na asilimia 2.69 na elimu ya sekondari kutoka 2,172,257 hadi 2,999,530 sawa na asilimia 38.01; na
- (xii) Kuimarika kwa matokeo ya mitihani ya kitaifa ambapo Darasa la Saba ufaulu

umefikia asilimia 80.87, Kidato cha Nne asilimia 92.37 kutoka 85.8 na Kidato cha sita ufaulu umefikia asilimia 99.99 kutoka 99.90.

22. ***Mheshimiwa Spika***, matokeo haya si tu mafanikio ya kiutawala ni ushindi wa kitaifa. Kuongeza miundombinu ya elimu; kuwekeza karibu shilingi bilioni 500 katika Elimu Bila Ada; na kuongeza idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa asilimia 175 haya ni matendo yanayosema kwa sauti kubwa kuliko maneno: kwamba serikali hii haikuja kuahidi tu, bali kutekeleza.

23. ***Mheshimiwa Spika***, wapo waliokuwa na mashaka, wapo waliokuwa wamesahau matumaini lakini leo, tuna ushahidi kuwa pale ambapo kuna nia njema, kuna njia na katika kila kona ya Tanzania, kuna darasa, mwalimu na mwanafunzi anayesimama kama ushahidi wa mabadiliko haya. Hivyo, ninaomba nitamke kauli ambayo itakumbukwa kwa miaka mingi ijayo: **Mtoto wa Kitanzania, popote alipo hawezi tena kuzuiwa na umbali na hawezi tena kusahaulika kwa sababu ya ulemavu**; elimu sasa ni haki ya kila mmoja na Tanzania mpya inaanzia darasani.

Na kwa misingi hiyo, tunaamini kabisa: Elimu Yetu, Uhai wa Taifa Letu.

2.2 Uratibu na Usimamizi wa Huduma za Afya ya Msingi

24. **Mheshimiwa Spika**, ibara ya 83 (d, f, l, q, u na z) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 imeelekeza kutekeleza mambo yafuatayo: Kujenga na kuimarisha vituo vya kutolea huduma za afya ili viweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi. Hadi kufikia 2025 Serikali itaongeza vituo vya kutolea huduma za afya kwa asilimia 20 ya vituo 8,446 vilivyopo sasa; vipaumbele vitawekwa katika ujenzi wa vituo vya afya na ukamilishaji wa maboma kwa kuzingatia uwiano wa kijografia, idadi ya watu na wingi wa magonjwa; Kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa hospitali 98 za halmashauri; Kuajiri wataalamu wa kutosha wenye ujuzi na kuboresha mazingira ya kazi; Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za afya ikiwemo tiba mtandao, mafunzo, utawala, usimamizi wa fedha, dawa na bidhaa zote za dawa pamoja na uboreshaji wa ukusanyaji na matumizi ya takwimu za afya katika hospitali za halmashauri, hospitali ngazi ya wilaya, vituo vya afya na zahanati; Kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya na kuzifanya rafiki kwa wanawake, wanaume na vijana ikiwemo kutoa huduma ya msingi ya dharura ya afya ya uzazi na mtoto, huduma tembezi na mkoba; Kuimarisha mfumo wa upelekaji wa fedha moja kwa moja kwenye akaunti za vituo vya kutolea huduma za

afya ngazi ya msingi kwa kushirikisha wadau wote wanaotekeleza afua za afya.

25. Mheshimiwa Spika, Hayati Mheshimiwa Benjamin Wiliam Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu alisema: "Tusiposhughulikia masuala ya afya ya msingi, hatutaweza kupiga hatua kubwa katika maendeleo." Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani katika huduma za afya ya msingi kama ifuatavyo:

- (i) Kujenga na kuimarisha vituo vya kutolea huduma za afya ili viweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi ambapo Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeongeza vituo vya kutolea huduma ya afya ya msingi kutoka 6,081 hadi 7,713 sawa na ongezeko la vituo 1,632 au asilimia 26.80. Kati ya vituo hivyo, zahanati ni 1,158, vituo vya afya 345 na hospitali za halmashauri 129;
- (ii) Ujenzi wa hospitali mpya za halmashauri 129 ikiwa ni ongezeko la asilimia 31.63 ya lengo la kujenga hospitali 98. Kati ya hospitali hizo, 67 zimejengwa majengo 14 ambayo ni; jengo la utawala, jengo la huduma kwa wagonjwa wa nje, jengo la maabara, jengo la mionzi, wodi ya wazazi, jengo la kutunzia dawa, jengo la kufulia, wodi ya magonjwa mchanganyiko (*medical ward*) wanawake na wanaume, wodi ya watoto, jengo la upasuaji, wodi ya upasuaji wanaume na wanawake na jengo la kuhifadha maiti; hospitali 86 kati ya hizo zimejengwa majengo

ya kuhudumia wagonjwa wa dharura (*Emergence Medical Department- EMD*) na hospitali 30 zimejengwa majengo ya kuhudumia wagonjwa mahututi (*Intensive Care Unit - ICU*) na kufanya idadi ya majengo yaliyokwisha jengwa kwa baadhi ya hospitali kufikia kati ya 14 hadi 16; na hospitali 62 zinaendelea na ujenzi wa majengo hayo katika hatua mbalimbali. Aidha, hospitali 128 kati ya 129 zimesajiliwa na tayari zinatoa huduma muhimu za awali, ikiwemo huduma kwa wagonjwa wa nje na huduma za uzazi;

- (iii) Wataalamu wa afya 34,720 wameajiriwa ambapo madaktari ni 1,851, matabibu 6,546, wauguzi 10,213, watekinolijia mionzi, macho, maabara, meno na dawa 1,488, wafamasia 993, maafisa lishe 328, maafisa ustawi 224, fundi sanifu vifaa tiba 239 na kada nyingine watumishi 12,838, wameajiriwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi. Aidha, watumishi 700 wameajiriwa kwa mkataba wa miaka mitatu (3) na watumishi 150 wa mkataba wa UVIKO;
- (iv) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwa kuboresha mfumo wa uendeshaji na usimamizi wa utoaji wa huduma za afya (GoTHOMIS) katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo vituo 4,915 au asilimia 67.88 ya vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi vinatumia mfumo. Kati ya vituo hivyo, hospitali za

halmashauri ni 186, vituo vya afya 848, zahanati 3,860, kliniki 3 na hospitali teule za wilaya 7 na vituo vingine 11 vinavyomilikiwa na taasisi za umma;

- (v) Kusimamia na kuratibu Mfumo wa Huduma ya Usafiri wa Dharura kwa akina Mama Wajawazito na Watoto Wachanga (M-MAMA) ambapo wateja 135,526 wamehudumiwa katika mfumo huo (kinamama wajawazito 110,722; watoto wachanga 24,537 na mama na mtoto 267). Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya na kuzifanya rafiki kwa wanawake, wanaume na vijana ikiwemo kutoa huduma ya msingi ya dharura ya afya ya uzazi na mtoto, huduma tembezi na mkoba ambapo yafuatayo yamefanyika:

- (a) Uimarishaji wa huduma za afya na utoaji wa huduma za mkoba zimeongeza idadi ya kinamama kuhudhuria kliniki. Aidha, akina mama wajawazito wanaohudhuria kliniki mahudhurio manne wameongezeka kutoka 2,374,666 mwaka 2020 kufikia 3,143,332 mwaka 2024, pia idadi ya wajawazito waliohudhuria hudhurio la kwanza kliniki kabla ya wiki 12 imeongezeka kutoka 848,149 mwaka 2020 hadi 1,186,812 mwaka 2024;

- (b) Uimarishaji wa huduma za akinamama katika vituo vya kutolea huduma na kuzifanya kuwa rafiki umechangia ongezeko la akina mama wanaojifungua katika vituo vya kutolea huduma za afya. Katika mwaka 2020 akina mama 52,585 walijifungua katika vituo vya kutolea huduma za afya msingi hadi kufikia akina mama 141,386 mwaka 2024;
- (c) Kuimarisha huduma za wajawazito ambapo uimarishaji wa huduma kwa mama wajawazito kumesaidia kuongeza idadi ya watoto wachanga waliozaliwa hai ambapo imeongezeka kutoka 1,392,634 mwaka 2020 hadi 1,828,285 mwaka 2024. Pia, Serikali imejenga vyumba maalumu 114 kwa ajili kutoa huduma za dharura kwa watoto wachanga (*Neonatal Care Unit - NCU* na *Kangaroo Mother Care - KMC*);
- (d) Utoaji wa huduma kwa vijana unaendelea kufanyika na halmashauri 22 kati ya 184 zimeshaanzisha vituo maalumu kwa ajili ya huduma rafiki kwa vijana; tumeyaishi kwa vitendo maneno ya ***Hayati Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi Rais wa Awamu ya Pili aliyosema, "Tuwekeze katika afya ya mama na mtoto kwa kuwa wao ni***

msingi wa kizazi kijacho chenye nguvu"; na

- (vi) Kuratibu upelekaji wa fedha moja kwa moja katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo vituo vinavyopokea fedha moja kwa moja vimeongezeka kutoka vituo 5,913 hadi 7,295. Aidha utaratibu huu umeboresha upatikanaji wa fedha katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi hivyo kuboresha huduma zinazotolewa.

2.3 Huduma za lishe

26. ***Mheshimiwa Spika***, ibara ya 86 (a, b, c na d) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 inaelekeza: Kutekeleza mikakati ya kupunguza idadi ya watoto chini ya miaka mitano wenye udumavu na ukondefu kwa kasi kubwa zaidi; Kupunguza idadi ya watoto wanaozaliwa na uzito pungufu yaani chini ya uzito wa kilogramu 2.5 ili iwe chini ya asilimia 50; na kupunguza kwa asilimia 50 viwango vya upungufu wa damu kwa wanawake walio katika umri wa kuzaa yaani miaka 15 – 49.

Mheshimiwa Spika, Hayati Ali Hassan Mwinyi Rais wa Awamu ya Pili aliwahi kusema, "Lishe bora na usafi wa mazingira ni silaha madhubuti za kupambana na magonjwa yanayozuilika."

27. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani katika huduma za lishe kama ifuatavyo:

- (i) Kusimamia utoaji wa huduma mbalimbali za lishe zinazolenga kupunguza udumavu, uzito pungufu wa kuzaliwa na uzito uliozidi kwa watoto. Miongoni mwa huduma zilizotolewa ni kutathimini hali ya lishe ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Takribani watoto 7,454,996 walipimwa hali ya lishe kwenye vijiji na mitaa nchini. Upimaji huo uliwezesha kuwabaini na kuwapa matibabu ya utapiamlo mkali watoto 149,308 kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi. Huduma nyingine zilizotolewa ili kudhibiti udumavu ni pamoja na ukaguzi wa ubora na usalama wa vyakula na utoaji wa elimu ya lishe kwa jamii. Wazazi na walezi 11,449,738 walipatiwa elimu na unasihi wa lishe na kuhimizwa kuboresha taratibu za ulishaji wa watoto ili kupunguza udumavu;
- (ii) Kutoa vidonge vya madini chuma na vitamini ya foliki kwa wanawake wajawazito ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa damu unaochangia vifo vya wanawake vitokanavyo na uzazi. Wajawazito 7,440,632 walipatiwa vidonge vya kuongeza wingi wa damu katika vituo vya kutolea huduma ya afya ngazi ya msingi. Aidha, vidonge vya Vitamini A ya nyongeza vimetolewa kwa watoto wenye umri

chini ya miaka mitano (5) ili kuimarisha kinga ya mwili na kupunguza kasi ya maambukizo ya magonjwa yanayochangia tatizo la udumavu. Watoto 8,944,200 wenye umri chini ya miaka mitano walipatiwa nyongeza ya matone ya Vitamini A kupitia kampeni za kitaifa zinazofanyika mara mbili kila mwaka; na

- (iii) Kutenga shilingi 1,000 au zaidi kwa kila mtoto chini ya umri wa miaka mitano (5) kutoka mapato ya ndani ya halmashauri ambapo shilingi bilioni 48.56 zilitolewa na kutumika kutoa huduma katika afua za lishe. Aidha kiwango cha utoaji wa shilingi 1,000 au zaidi kwa kila mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano katika mikoa na halmashauri nchini kimefikia wastani wa kitaifa wa shilingi 1,546.

2.4 Huduma za Ustawi wa Jamii

28. ***Mheshimiwa Spika***, ibara za 91(a, e na f), 93(b, c, f, i na l) na 95(i na h) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 zinaelekeza: Kuimarisha huduma za matibabu bila malipo kwa wazee; Kutoa huduma za matunzo na kisaikolojia kwa wazee na watu wenye ulemavu; Kuimarisha mabaraza ya wazee maeneo yote nchini; Kuunda kamati za ulinzi wa wanawake na watoto na kuzijengea uwezo ili kuhakikisha kuwa zinatekeleza afua za ulinzi na usalama wa wanawake na watoto na kulinda maadili chanya ya taifa; Kusimamia, kufuatilia na kuimarisha uanzishaji na

uendelezaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo na vituo vya maendeleo ya awali ya mtoto katika ngazi ya jamii ili kuboresha malezi na makuzi ya kila mtoto; Kuimarisha huduma kwa watoto walio katika mkinzano na sheria kwa kuboresha mahabusu za watoto; Kuimarisha huduma za usuluhisho wa migogoro ya ndoa na matunzo kwa watoto; Kuboresha rejista ya watu wenye ulemavu itakayotoa taarifa sahihi za watu wenye ulemavu ili kuimarisha utoaji wa huduma na misaada; pamoja na kuboresha na kusimamia utoaji wa msaada wa kisaikolojia kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, “Maendeleo ya kweli hayawezi kupatikana kama hatuwekezi katika afya, elimu, na ustawi wa jamii. Taifa imara linajengwa kwa kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma bora na fursa sawa za maendeleo.” - Hayati Benjamini William Mkapa Rais wa Awamu ya Tatu

29. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani katika huduma za ustawi wa jamii kama ifuatavyo:

- (i) Kutambua wazee 4,975,473 (wanawake 2,682,210 na wanaume 2,293,263) na kutoa huduma za matibabu bila malipo. Kati ya wazee waliotambuliwa wazee 2,199,588 (wanawake 1,189,512 na wanaume 1,010,076) wamepatiwa vitambulisho/bima ya afya kwa ajili ya msamaha wa matibabu. Aidha, vituo 7,300 vya kutolea huduma ya afya, vimeanzisha

madirisha 4,574 ya kutolea huduma za afya kwa wazee. Vilevile, kutokana na uhaba wa vyumba maalumu kwa huduma za wazee vituo 2,726 vinazingatia ujumbe wa “Mpishe mzee kwanza” ili apatiwe huduma katika vituo vilivyopo kwenye halmashauri zote 184;

- (ii) Kuunda na kuimarisha mabaraza 20,768 ya ushauri ya wazee katika ngazi za mikoa 26, halmashauri 184, kata 3,956, vijiji 12,333 na mitaa 4,269. Aidha, kamati za watu wenye ulemavu 2,449 ziliundwa. Kupitia kamati hizo, wazee na watu wenye ulemavu wanapatiwa huduma za matunzo na kisaikolojia;
- (iii) Kuunda kamati 20,768 za ulinzi na usalama wa mwanamke na mtoto, uanzishwaji wa vituo vya huduma kwa pamoja (*one stop centre*) katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo vituo vya huduma kwa pamoja vimeongezeka kutoka 21 hadi 25. Aidha, vituo vya kulelea watoto wadogo mchana vimeongezeka kutoka 2,378 hadi 3,362;
- (iv) Kuanzisha vituo 206 vya kulelea watoto wadogo vinavyotoa huduma kwa watoto 11,675 (wanaume 4,833 na wanawake 6,842). Aidha, vituo binafsi vilivyosajiliwa ni 3,862 vinavyohudumia watoto 397,935 (wanaume 175,517 na wanawake 222,418);
- (v) Kushughulikia ukatili wa kijinsia ambapo mashauri 517,286 ya ukatili wa kijinsia na

ukatili dhidi ya watoto yameshughulikiwa. Kati ya mashauri hayo, ya ngono na ulawiti yalikuwa 53,925, ya kupigwa au kuumizwa 180,047, ya kuumizwa kihisia 272,571 na kutelekezwa 10,743. Aidha, migogoro ya ndoa na familia 97,234 imeshughulikiwa na kati ya migogoro hiyo, migogoro 15,414 ilipelekwa mahakamani kwa usuluhishi zaidi;

- (vi) Watu wenye Ulemavu 821,763 (wanaume 411,321 na wanawake 410,442) walipatiwa huduma za msaada wa kisaikolojia. Kati ya hao, watu wenye Ualbino 67,502 walipatiwa msaada wa kisaikolojia wakati wa uendes haji wa kliniki za uchunguzi wa saratani ya ngozi katika mikoa 24 na halmashauri 172; na
- (vii) Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi 2,592,963 (wanaume 1,142,014 na wanawake 1,450,949) walitambuliwa na kupatiwa huduma mbalimbali zikiwemo mafunzo ya ufundi stadi, kadi za bima ya afya ya Jamii na vifaa vya shule. Kati ya watoto hao, waliotambuliwa wanaoishi na kufanya kazi mitaani ni 18,291 (wanaume 9,448 na wanawake 8,843), ambapo watoto 21 waliweza kuunganishwa na vyuo vya ufundi na wengine 18,270 waliunganishwa na familia zao. Aidha, jumla ya watoto 4,207,796 walio na umri chini ya miaka mitano (5) wamesajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa sawa na asilimia 45.7 ya jumla ya watoto wa kundi hilo.

2.5 Ujenzi, Ukarabati na Matengenezo ya Barabara

30. **Mheshimiwa Spika**, Ibara 57 (c-d) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 inaelekeza kuongeza kiwango cha barabara za changarawe kutoka kilomita 24,493 hadi kilomita 35,000; kuongeza urefu wa barabara za vijijini na mijini zilizojengwa kwa kiwango cha lami kutoka kilomita 2,025 hadi kilomita 3,100; na kuongeza mtandao wa barabara toka kilomita 108,946.19, mwaka, 2020 hadi kufikia kilomita 143,881 mwaka 2025.

31. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani katika ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara kupitia TARURA kama ifuatavyo:

- (i) Ujenzi wa barabara za changarawe ambao umeongezeka kutoka kilomita 24,493 hadi kilomita 44,372.21 sawa na ongezeko la asilimia 81.16. Urefu wa barabara za vijijini na mijini zilizojengwa kwa kiwango cha lami umeongezeka kutoka kilomita 2,025 hadi kilomita 3,467.30 sawa na ongezeko la asilimia 71.22. Aidha, kuongeza mtandao wa barabara kutoka kilomita 108,946.19 hadi kilomita 144,429.77, sawa na ongezeko la asilimia 32.57;
- (ii) Kufanya tafiti kwa kutekeleza kazi za ujenzi wa miundombinu ya barabara kwa kutumia

teknolojia mbadala (*ecoroads*, *ecozyme* na *polymer*) ambapo barabara zenye urefu wa kilomita 61.7 zinaendelea kufanyiwa tafiti ili kupunguza gharama za ujenzi, matengenezo na ukarabati. Teknolojia hiyo huimarisha tabaka la chini la barabara na hivyo kuzifanya kuwa stahimilivu dhidi ya uharibifu wa mapema unaotokana na maji na uzito. Aidha, kwa kutumia malighafi zinazopatikana mahali pa kazi ujenzi wa miundombinu ya barabara kilomita 28.92 na madaraja 395 kwa kutumia mawe katika barabara za wilaya umekamilika; na

- (iii) Tulipotoka kulikuwa na vumbi, lakini leo tunatembea kwenye lami. Tulipotoka kulikuwa na miteremko isiyopitika, leo tuna barabara zinazounganisha ndoto na fursa. Kuongezeka kwa barabara za changarawe kwa asilimia 81.16 na lami kwa asilimia 71.22 ni ushahidi wa nchi inayojenga msingi wa maendeleo kwa kila mtanzania – kuanzia kijijini hadi mjini. Huu siyo mradi wa barabara tu, huu ni mradi wa matumaini!

Kila kilomita mpya ya barabara iliyojengwa ni daraja kati ya umaskini na maendeleo; ni njia ya mtoto kufika shuleni, mama kufika hospitali, mkulima kupeleka mazao sokoni na taifa kusonga mbele. Kuongeza mtandao wa barabara kutoka kilomita 108,946 hadi zaidi ya 144,000 si takwimu tu – ni

mabadiliko ya kweli yanayoonekana, yanayogusika na yanayogusa maisha.

Barabara hizi ni sauti ya serikali inayosema: **'Hatukuwaacha Nyuma.'** Hizi ni njia zinazotufikisha kwenye Tanzania ya viwanda, fursa na mshikamano wa kitaifa.

2.6 Huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka

32. **Mheshimiwa Spika**, ibara ya 57(e) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 inaelekeza kuimarisha utoaji wa huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam.

33. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani kwa kutoa Huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka kupitia DART kama ifuatavyo:

- (i) Kusambaza kadi janja 62,000 kati ya 200,000 katika awamu ya kwanza na kusimika mageti janja kwenye vituo vyote 27;
- (ii) Kusimika Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji Nauli (*Automated Fare Collection System-AFCS*) ambao utafungamanishwa na mfumo wa kuongozea magari (*Intelligent Transport System - ITS*) ambao upo kwenye hatua ya ununuzi; na
- (iii) Wakala imenunua watoa huduma watatu (3) wa uendeshaaji kwa njia ya ubia (PPP) wa

mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili na mikataba imeshasainiwa.

34. **Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu watu wa Jiji la Dar es Salaam wamekuwa wakisubiri – wengine kwa matumaini, wengine kwa mashaka lakini wote kwa kiu ya mabadiliko. Leo, kwa mara ya kwanza tunasema: subira yao haikuwa ya bure. Kupitia ubia kati ya Serikali na sekta binafsi (PPP), tumefanikisha hatua ya kihistoria – kusaini mikataba na watoa huduma watatu (3) wa uendeshaji wa Awamu ya Pili ya Mabasi Yaendayo Haraka. Hili ni tukio la mwanzo wa zama mpya – siyo tena hadithi ya ahadi zisizotekelezwa, bali ya huduma bora zinazoonekana na kuguswa."

"Great things take time."

35. **Mheshimiwa Spika**, wanafalsafa wanasema, **"Mambo Makubwa Yanahitaji Muda."** Hatua hii si tu ununuzi wa huduma, bali ni ununuzi wa matumaini mapya kwa wakazi wa jiji letu. Hatutaki kurudia makosa ya jana, bali tunajenga mfumo imara, unaozingatia ubora, ufanisi na heshima kwa muda na maisha ya abiria.

***"Hope is being able to see that there is light despite all the darkness."* – Desmond Tutu.**

36. **Mheshimiwa Spika**, kwa miaka mingi wananchi wamepitia usumbufu, foleni zisizokwisha na huduma zisizoeleweka. Lakini leo, tunasema kwa sauti ya matumaini: nuru inaanza kuonekana.

Mabasi haya hayatakuwa tu magari ya kusafirisha watu – yatakuwa magari ya kusukuma uchumi, kuunganisha fursa na kupunguza mzigo wa maisha ya kila siku.

"Progress is not in enhancing what is, but in advancing toward what will be." – Khalil Gibran.

37. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unaonesha jinsi tunavyotoka kwenye kilichozoeleka – foleni, ajali, uchakavu na kuelekea kwenye kile kinachowezekana: usafiri wa kisasa, wa heshima, wa watu wote. Tunajenga mfumo wa usafiri wa umma ambao utaweka heshima kwa abiria, uwajibikaji kwa watoa huduma na thamani kwa kila senti inayowekezwa.

38. ***Mheshimiwa Spika***, awamu hii mpya ni jibu la kilio cha miaka mingi, ni ushahidi kuwa Serikali ya Awamu ya Sita haikosei mwelekeo – tunasonga mbele kwa busara, kwa maono, na kwa nia njema ya kuwahudumia Watanzania."

2.7 Utawala Bora, Kujenga Uwezo, Usimamizi wa Rasilimali, Ujenzi wa Majengo ya Utawala na Makazi ya Viongozi

39. ***Mheshimiwa Spika***, ibara za 18 (b) (vii), 122 (a, e, l) na 235 (a, e) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 zimeelekeza kutekeleza mambo yafuatayo: Kuimarisha mifumo ya kitaasisi na uwezo wa

viongozi na watendaji wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwenda vijijini kusikiliza na kushughulikia kero na malalamiko ya wananchi kwa wakati, haki na uadilifu. Aidha, kuwapokea, kuwasikiliza na kuwahudumia wananchi wanaotembelea ofisi hizo kwa weledi, hekima na busara; Kujenga uwezo wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwa kutoa mafunzo, mifumo na vitendea kazi ili kuiwezesha kutoa huduma kwa wananchi; na Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kujenga ofisi za wakuu wa mikoa, wilaya, tarafa, kata na vijiji pamoja na nyumba za watumishi kwa kuweka kipaumbele katika maeneo ambayo hayana ofisi na nyumba za viongozi na watumishi.

40. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani kwenye eneo la utawala bora kama ifuatavyo:

- (i) Kero 282,124 zimepokelewa na kusikilizwa katika ngazi ya mikoa na wilaya ambapo jumla ya kero 263,893 zimetatuliwa na kero 18,231 zipo katika hatua mbalimbali za utatuzi, baadhi ya kero zilizotatuliwa ni pamoja na masuala ya ardhi, barabara, umeme na maji;
- (ii) Mafunzo yanayohusu uongozi katika usimamizi wa rasilimaliwatu na fedha yalitolewa kwa wakuu wa mikoa 26, makatibu tawala wa mikoa 26, wakuu wa wilaya 139, makatibu tawala wa wilaya 139. Aidha, makatibu tawala wasaidizi wa mikoa 208 walipatiwa mafunzo kuhusu uandaaji wa mpango mkakati, uchumi mahalia,

mkataba wa huduma kwa mteja, uendeshaji wa mabaraza ya biashara, ukaguzi na ufuatiliaji wa fedha, usimamizi na uendeshaji wa shughuli za elimu na afya;

- (iii) Kuajiri maafisa tarafa 72, wahandisi 52, wakadiriaji majenzi 25 na wataalamu wa ununuzi 12 na kupangiwa katika ofisi za wakuu wa mikoa;
- (iv) Ujenzi wa majengo 289 na ukarabati wa majengo 220, ambapo ujenzi wa ikulu ndogo 7 na ukarabati wa ikulu ndogo 16, ujenzi wa ofisi sita (6) na ukarabati wa ofisi 20 za wakuu wa mikoa, ujenzi wa ofisi 34 na ukarabati wa ofisi 51 za wakuu wa wilaya, ujenzi wa ofisi 133 na ukarabati wa ofisi nane (8) za maafisa tarafa, ujenzi wa nyumba nane (8) na ukarabati wa nyumba 13 za wakuu wa mikoa, ujenzi wa nyumba tano (5) na ukarabati wa nyumba 17 za makatibu tawala wa mikoa, ujenzi wa nyumba 31 na ukarabati wa nyumba 42 za wakuu wa wilaya, ujenzi wa nyumba 47 na ukarabati wa nyumba tisa (9) za makatibu tawala wasaidizi, ujenzi wa nyumba 18 na ukarabati wa nyumba 44 za makatibu tawala wa wilaya umefanyika; na
- (v) Ununuzi wa magari 346 kati ya hayo 18 ya wakuu wa mikoa, 14 ya makatibu tawala wa mikoa, 120 ya wakuu wa wilaya na 68 ya idara katika ofisi za wakuu wa mikoa na 126

ya wakurugenzi wa halmashauri na ununuzi wa pikipiki 1,206 za watendaji wa kata.

2.8 Ulinzi wa Mazingira, uhifadhi wa Maliasili, Mabadiliko ya Tabianchi na Biashara ya Kaboni

41. **Mheshimiwa Spika**, Ibara za 68(c) na 235(e) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 zimeelekeza kuimarisha ushiriki wa jamii katika usimamizi wa rasilimali za misitu kwa kutekeleza programu zinazolenga kuzalisha ajira na kuongeza kipato; na Kubuni na kuweka mikakati ya kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kwa lengo la kupunguza kasi ya uharibifu wa mazingira kwa kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala ikiwemo gesi na umeme.

42. **Mheshimiwa Spika**, shilingi bilioni 45 zimepokelewa kutoka kampuni ya Carbon Tanzania Ltd na Kaderes Peasant Development PLC kutokana na uuzaji wa kaboni. Fedha hizo zimenufaisha wananchi wa Halmashauri 10 za Mikoa ya Katavi (Tanganyika), Manyara (Kiteto na Mbulu), Arusha (Karatu), Kagera (Kyerwa, Karagwe, Misenyi, Muleba, Ngara na Bukoba Vijijini).

43. **Mheshimiwa Spika**, shuguli zilizotekelezwa kutokana na fedha zilizopatikana kutokana na biashara ya kaboni ni kama ifuatavyo:

- (i) Ujenzi vyumba vya madarasa 64 katika shule za msingi na sekondari;
- (ii) Ujenzi wa matundu ya vyoo 160 katika zahanati na shule;
- (iii) Ujenzi wa nyumba 26 za watumishi;
- (iv) Ukamilishaji wa masoko 6 ya vijiji na vivuko 3;
- (v) Ukamilishaji wa vituo 4 vya polisi na majosho 2 kwa ajili ya mifugo;
- (vi) Ujenzi wa jiko na stoo kwa shule za msingi 6; na
- (vii) Ujenzi na ukamilishaji wa mabweni 8 yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 960 katika shule za Sekondari za Mwese, Ndedo na Domaga.

44. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza mkakati wa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kwa lengo la kupunguza kasi ya uharibifu wa mazingira kwa kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala ikiwemo gesi na umeme Ofisi ya Rais - TAMISEMI imehamasisha matumizi ya nishati safi ambapo taasisi 903 zikiwemo shule za msingi 83, sekondari 650 na taasisi zingine 170 zimeanza kutumia mfumo wa nishati safi.

2.9 Mamlaka za Serikali za Mitaa

45. ***Mheshimiwa Spika***, ibara za 19(a) (ii), 32 (s) na 122 (c, d, e, h, i, j, l, m, n), ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa

Mwaka 2020 zinaelekeza yafuatayo: Kuimarisha huduma za kifedha kwa wananchi kutokana na kutungwa kwa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017 na kanuni zake za mwaka 2019 pamoja na kuboresha usimamizi wa taasisi za kifedha na maadili ya watumishi wa taasisi hizo ili kumlinda mteja; Kuhakikisha kwamba halmashauri zote nchini zinaendelea kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa mujibu wa sheria ili kuwezesha vijana na makundi mengine katika jamii zetu kupata mikopo isiyo na riba; Kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi; Kuimarisha serikali za mitaa ili ziendeleo kuwa chombo cha kuwapa wananchi uwezo na sauti ya kuamua na kushiriki kwa karibu katika shughuli za maendeleo; Kujenga uwezo wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwa kutoa mafunzo, mifumo na vitendea kazi ili kuiwezesha kutoa huduma kwa wananchi; Kubuni na kuibua miradi ya kimkakati ambayo itaboresha utoaji wa huduma katika mamlaka za serikali za mitaa na kuongeza mapato ya ndani na kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu; Kuimarisha utekelezaji wa maboresho ya serikali za mitaa kupitia sera na sheria mbalimbali ili kuendana na dhana ya kupeleka madaraka karibu na wananchi; Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kujenga ofisi za wakuu wa mikoa, wilaya, tarafa, kata na vijiji na nyumba za watumishi kwa kuweka kipaumbele katika maeneo ambayo hayana ofisi na nyumba za

viongozi na watumishi; Kuboresha mazingira ya kufanyia biashara na uwekezaji katika mamlaka za serikali za mitaa kwa kutenga maeneo ya uwekezaji na kuzipatia ufumbuzi kero za wafanyabiashara ndogondogo; na kusimamia kikamilifu suala la utawala bora, uadilifu, uwajibikaji na matumizi sahihi ya rasilimali za umma pamoja na miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika mamlaka hizo ili itekelezwe kwa kiwango kinachokusudiwa na kuhakikisha kuwa ubora wa miradi unalingana na thamani ya fedha iliyotumika.


46. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani katika mamlaka za serikali za mitaa kama ifuatavyo:

- (i) Kusajili vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha ambapo vikundi 57,364 vimesajiliwa katika halmashauri zote nchini;
- (ii) Kutoa mikopo ya shilingi bilioni 158.50 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambapo shilingi bilioni 63.40 ni wanawake (vikundi 8,576), shilingi bilioni 63.40 ni vijana (vikundi 4,981) na shilingi bilioni 31.70 watu wenye ulemavu (vikundi 2,319);
- (iii) Bajeti ya mapato ya ndani ya halmashauri imeongezeka kutoka shilingi bilioni 814.96 hadi shilingi trilioni 1.35 sawa na asilimia 60; Aidha, fedha za mapato ya ndani zilizoidhinishwa katika miradi ya maendeleo zimeongezeka

kutoka shilingi bilioni 333.09 hadi bilioni 454.41 sawa na asilimia 36.42;

- (iv) Makusanyo halisi ya mapato ya ndani ya halmashauri yameongezeka kutoka shilingi bilioni 757.05 mwaka 2020/21 hadi shilingi trilioni 1.15 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 77 mwaka 2024 **Kielelezo Na. 1**. Aidha, fedha za mapato ya ndani zilizopelekwa katika miradi ya maendeleo zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 276.69 hadi shilingi bilioni 313.26 sawa na asilimia 13.21.

Kielelezo Na.1: Mwenendo wa Bajeti na Makusanyo Halisi ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri Mwaka 2020/21 – Machi, 2024/25



- (v) Miradi 30,928 imeibuliwa na wananchi ambapo sekta za elimu 16,080, afya 7,472, barabara 1,232, maji 608 na utawala 5,536 kupitia Mfumo wa Fursa na Vikwazo vya Maendeleo Ulioboreshwa (*Improved Opportunities and Obstacles to Development - O&OD*);
- (vi) Mafunzo elekezi kuhusu Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo Ulioboreshwa (*improved O&OD*) yalitolewa kwa wakurugenzi 184, vikosi kazi vya halmashauri zote 184 vyenye maafisa 1,288 na maafisa TEHAMA 184. Aidha, mafunzo hayo yametolewa kwa wawezeshaji kata 207 kutoka halmashauri 20 na kwa maafisa ugani 249 wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma (123), Manispaa ya Morogoro (6) na Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa (120);
- (vii) Miradi ya kimkakati 251 imebuniwa katika mamlaka za serikali za mitaa ikiwemo stendi za mabasi, maegesho ya malori, masoko, viwanja vya michezo, maduka ya biashara, kiwanda cha chaki na machinjio. Kati ya hiyo, miradi 48 imekidhi vigezo na imeanza utekelezaji ambapo miradi 22 imekamilika na imeanza kutoa huduma na shilingi bilioni 37.55 zimekusanywa kutoka kwenye miradi hiyo;
- (viii) Ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa majengo 122 ya utawala ya halmashauri. Kati ya hayo, 66 yamekamilika na 56 ujenzi upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Pia, ofisi 4,960 za vijiji, ofisi 737 za mitaa, na nyumba

156 za viongozi na watumishi zimejengwa, kukamilishwa na kufanyiwa ukarabati;

- (ix) Kutenga maeneo yenye ukubwa wa ekari 22,000 katika mamlaka za serikali za mitaa kwa ajili ya wafanyabiashara ndogondogo. Aidha, kero 1,849 za wafanyabiashara ndogondogo zimetatuliwa ambapo wachuuzi 4,899 na watoa huduma wadogo wamesajiliwa pamoja na wafanyabiashara ndogondogo na kati 3,565 wametambuliwa. Vilevile, vituo vya kutoa huduma kwa pamoja 65 zimeanzishwa katika mamlaka za serikali za mitaa;
- (x) Watumishi 8,097 wameajiriwa katika kada zifuatazo; uhandisi 443, wakadiriaji majenzi 122, watendaji wa kata na vijiji/mtaa 4,070, maendeleo ya jamii 2,241, wasanifu majengo 22, mafundi sanifu na maafisa ugani 1,199; na
- (xi) Watumishi 3,680 katika mamlaka za serikali za mitaa (wakiwemo wakurugenzi, wakuu wa idara na vitengo) kutoka mamlaka za serikali za mitaa wameweza kupatiwa mafunzo mbalimbali yakiwemo usimamizi wa masuala ya kinidhamu, maadili, ugavi kutumia mfumo wa NeST, sheria, kaguzi, uibuaji wa miradi/vyanzo vya mapato, uandishi wa miradi, na uandaaji wa miradi ya kimkakati.

2.10 Uendelezaji Miji

47. **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 76(b) na 122(k) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 zimeelekeza kuratibu, kusimamia, kufuatilia na kutoa ushauri wa kitalaamu katika utekelezaji wa Mipango Kabambe na Mifumo ya Kijiografia ili kuwezesha mifumo ya ukusanyaji na uchakataji taarifa za kodi za majengo, mabango, pango la ardhi na vibali vya ujenzi.

48. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani katika maeneo yafuatayo:

- (i) Mipango Kabambe ya miji 33 imeandaliwa na kuidhinishwa na mamlaka za upangaji ikiwemo miji yote ya makao makuu ya mikoa 26 na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Mamlaka hizo ni Majiji matano (5) (Dodoma, Mwanza, Arusha, Dar es Salaam na Mbeya), Manispaa 12 (Musoma, Singida, Iringa, Shinyanga, Tabora, Bukoba, Songea, Sumbawanga, Mtwara-Mikindani, Kigoma-Ujiji, Mpanda na Lindi) na Miji sita (6) (Kibaha, Korogwe, Babati, Njombe, Bariadi na Geita); na
- (ii) Kuandaa Mpango Kabambe Jumuishi wa Jiji la Kibiashara na Uwekezaji la Kwala, Mkoa wa Pwani 2024 – 2054 ambao umetangazwa katika Gazeti la Serikali Na: 633 la tarehe 28 Oktoba, 2022. Ukubwa wa Jiji hilo ni hekta

130,831, limechukua jumla ya vijiji 30 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe vitano (5), Kibaha (16) na Chalinze tisa (9) ambalo ukubwa wa eneo lake unakaribia ukubwa wa Mkoa wa Dar es Salaam wenye ukubwa nchi kavu pekee wa hekta 139,300. Jiji hilo limelengwa kuwa kitovu shindani cha biashara, uwekezaji, utalii, viwanda na uendeshaji wa mifumo ya fedha kwenye Ukanda wa Magharibi mwa Bahari ya Hindi.

49. **Mheshimiwa Spika**, Jiji la Kwala litapunguza na hatimaye kuondosha changamoto za msongamano zilizopo katika Mkoa wa Dar es Salaam. Hatua hiyo ni jitihada za Serikali za kuongeza ufanisi wa ushushaji na uondoshaji mizigo kwenye bandari ya Dar es Salaam ambapo mizigo inayotoka bandari ya Dar es Salaam imeanza kupakuliwa, kuhamishiwa na kukabidhiwa kwa wateja kwenye bandari kavu ya Kwala iliyoko Vigwaza. Aidha, nalipongeza Shirika la Reli Tanzania kwa kuanzisha huduma kwenye bandari kavu ya Kwala, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Shirika la Viwango Tanzania kwa kufungua matawi yake kwenye bandari kavu ya Kwala na kuanza kutoa huduma. Kufanya hivyo kumelenga kuboresha muonekano wa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

50. **Mheshimiwa Spika**, Miongozo ya utekelezaji wa Mpango Kabambe na Mfumo wa Taarifa za Kijiografia (*Geographical Information System – GIS*) ilisambazwa kwenye Mikoa 12 katika halmashauri

56 pamoja na kuzijengea uwezo timu za menejimenti za halmashauri kama ifuatavyo: - Songwe tano (5), Rukwa tatu (3), Kigoma sita (6), Mwanza nne (4), Mara tano (5), Kagera tano (5), Dodoma tano (5), Mtwara tano (5), Singida mbili (2), Iringa tano (5), Arusha sita (6) na Tanga tano (5).

51. **Mheshimiwa Spika**, Mradi wa *Green and Smart Cities* – SASA 2022 – 2027, unatekelezwa kwenye Halmashauri za Majiji ya Tanga na Mwanza na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ambapo wanufaika 913 walijengewa uwezo katika Mfumo wa Taarifa za Kijiografia pamoja na Miongozo ya Utekelezaji wa Mpango Kabambe katika Halmashauri inayotekeleza mradi. Mgawanyo wa wanufaika hao ni vijana 337, wanawake 485 na makundi maalumu 91. Aidha, wataalamu 78 kutoka Ofisi za Wakuu wa Mikoa ya Mwanza na Tanga na halmashauri ya Jiji la Mwanza na Tanga na Manispaa ya Ilemela pia walijengewa uwezo. Aidha, ilihusisha kuwajengea uwezo wataalamu wengine 1,672 wa Halmashauri mbalimbali kwenye mikoa 12 kuhusu matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Kijiografia; na Andiko dhana la mapendekezo ya rasimu ya Sera ya Maendeleo Vijijini na Mijini limeandaliwa;

2.11 Uendelezaji wa Miji Midogo Inayochipukia

52. **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 122 (k) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 inaelekeza sera ya maendeleo ya miji na kuendelea na utekelezaji wa programu ya

uendelezaji wa miundombinu katika majiji, manisipaa na miji ili iwe ya kisasa itakayochangia ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi. Kipaumbele kitakuwa ni kuendeleza miji inayochipukia ili kuzuia uendelezaji usiozingatia taratibu za mipango miji;

53. **Mheshimiwa Spika**, miji inayochipukia ni 4,103 sawa na asilimia 91.5 ambayo ipo kwenye halmashauri za wilaya na vijiji miji (*urban villages*), 379 sawa na asilimia 8.5 ipo kwenye halmashauri za miji. Fursa mbalimbali za kiuchumi, mazingira na kijamii za miji hiyo zilibainishwa kikanda, mikoa na halmashauri kwa kutumia mfumo wa taarifa za kijiografia na hivyo kuweza kuainishia miji hiyo aina ya huduma na uwekezaji utakaokuwa na tija kulingana na maliasili zilizoko kwenye maeneo hayo.

54. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imedhamiria kuimarisha miji hii kwa kuwa inaweka msawazo katika utangamano kijamii na kiuchumi na kuchochea mapinduzi kwenye ngazi hiyo katika uwekezaji, biashara, matumizi ya ufundi, teknolojia na TEHAMA yenye manufaa kwa pande mbili hizo. Aidha, miji hiyo ndiyo msingi wa ukuaji wa miji ya baadaye na inaimarisha shughuli za maendeleo kwenye halmashauri za wilaya.

SEHEMU YA TATU

3.0 Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Mafungu 28) Kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025

3.1 Vipaumbele vya Bajeti kwa Mwaka 2024/25

55. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilipanga kutekeleza mpango na bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo: -

- (i) Kusimamia masuala ya utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuuji wa Madaraka kwa Umma (D by D);
- (ii) Kuratibu na kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2024;
- (iii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa huduma za jamii;
- (iv) Kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi yasiyo na tija katika ngazi zote ikijumuisha kuongeza kasi ya biashara ya kaboni;
- (v) Kuratibu na kusimamia mifumo na miundombinu ya TEHAMA;
- (vi) Kuendeleza rasilimaliwatu katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

- (vii) Kuratibu na kusimamia shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa;
- (viii) Kuratibu na kusimamia masuala ya michezo katika shule za msingi na sekondari;
- (ix) Kuratibu na kusimamia utendaji kazi wa taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI;
- (x) Kuratibu na kusimamia ujenzi wa miradi ya maendeleo katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI; na
- (xi) Kuratibu na kusimamia shughuli za uendelezaji wa vijiji na miji kwenye mamlaka za serikali za mitaa.

3.2 Ukusanyaji wa Kodi ya Majengo, Maduhuli na Mapato ya Ndani ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Mafungu 28) Mwaka 2024/25

56. *Mheshimiwa Spika*, Mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais – TAMISEMI na taasisi zilizo chini yake, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa iliidhinishiwa kukusanya kodi ya majengo, maduhuli na mapato ya ndani ya shilingi trilioni 1.60. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 188.96 ni makadirio ya kodi ya majengo ambayo yatakusanywa na mamlaka za serikali za mitaa zilizopewa uwakala wa kukusanya kodi hiyo na

kuwasilisha makusanyo Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, shilingi bilioni 55.42 ni mapato ya ndani ya taasisi. Aidha, shilingi milioni 315.93 ni maduhuli ya mikoa na shilingi trilioni 1.35 ni za mapato ya ndani ya halmashauri.

57. **Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2025 shilingi trilioni 1.11 zimekusanywa sawa na asilimia 93.15 ya lengo la kipindi hicho. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 61.21 ni kodi ya majengo, shilingi trilioni 1.04 ni mapato ya ndani ya mamlaka za serikali za mitaa (**Kiambatisho Na. 2**), shilingi bilioni 16.23 ni mapato ya ndani ya taasisi na shilingi milioni 201.60 ni maduhuli ya mikoa. Makusanyo hayo yalitokana na ada za wanachuo, tozo, ukusanyaji wa madeni, mauzo ya bidhaa mbalimbali na ushuru unaotozwa na mamlaka za serikali za mitaa kulingana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290.

3.3 Taarifa ya Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

58. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na taasisi zilizo chini yake (Fungu Na. 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 02) na mafungu 26 ya mikoa (yakijumuisha halmashauri 184) ilipanga kutumia shilingi trilioni 10.53 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya hizo Matumizi ya Kawaida ni shilingi 6.94 ambapo Mishahara ni shilingi trilioni 5.52 na Matumizi Mengineyo ni shilingi trilioni 1.42 yanayojumuisha shilingi bilioni

815.06 za mapato ya ndani ya halmashauri. Aidha, shilingi trilioni 3.58 ni fedha za maendeleo, kati ya hizo shilingi trilioni 2.44 ni fedha za ndani ikijumuisha shilingi bilioni 541.27 ni Mapato ya Ndani ya Halmashauri na shilingi trilioni 1.14 ni fedha za Nje.

59. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Machi, 2025 Mafungu 28 yamepokea na kukusanya shilingi trilioni 7.53 sawa na asilimia 71.47 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 5.39 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yakijumuisha Mishahara shilingi trilioni 4.08 na Matumizi Mengineyo shilingi trilioni 1.31. Aidha, shilingi trilioni 2.13 ni fedha za Miradi ya Maendeleo ikijumuisha shilingi trilioni 1.74 Fedha za Ndani na shilingi bilioni 385.83 ni Fedha za Nje.

60. ***Mheshimiwa Spika***, kati ya fedha zilizopokelewa shilingi bilioni 312.30 ni za mapato ya ndani ya halmashauri ambazo zimetumika kwenye Miradi ya Maendeleo (***Kiambatisho Na. 3***).

3.4 Mafanikio ya Utekelezaji ya Bajeti kwa Mwaka 2024/25

61. ***Mheshimiwa Spika***, Mwaka 2024/25 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, ofisi za wakuu wa mikoa na halmashauri zimefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

3.5 Shughuli Zilizotekelezwa Kupitia Fedha za Mapato ya Ndani ya Halmashauri

Mheshimiwa Spika, Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema "Tunahitajika kuongeza juhudi zetu katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ili tuweze kufikia malengo yetu ya maendeleo."

62. ***Mheshimiwa Spika***, Mwaka 2024/25 Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilipanga kutumia shilingi bilioni 541.27 za mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kuchangia utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 312.30 sawa na asilimia 57.70 zimetolewa na shughuli zifuatazo zimetekelwa:

- (i) Ujenzi wa hosteli 24 umekamilika na 105 zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, vyumba vya madarasa 122 vimekamilika na 202 vipo katika hatua za ukamilishaji, ujenzi wa nyumba za walimu 15 umekamilika na 140 zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, ofisi za walimu 14 zimekamilika na 36 utekelezaji unaendelea, ujenzi wa shule 175 umekamilika na 117 zipo hatua mbalimbali za utekelezaji, matundu ya vyoo 534 yamekamilika na 1,966 ujenzi unaendelea, madawati 17,429 yamekamilika na 11,533 yanaendelea kutengenezwa;
- (ii) Ujenzi wa hospitali mbili (2) za Manispaa ya Temeke na Jiji la Dodoma unaendelea, uendelezaji wa hospitali 22 upo katika hatua

mbalimbali za utekelezaji, usimikaji wa mfumo wa GoTHOMIS katika vituo vya afya 21 unaendelea, ujenzi wa vichomea taka 10 ambapo vitatu (3) vimekamilika na saba (7) vipo hatua mbalimbali za utekelezaji, ujenzi wa vituo vya afya 162, ambapo vituo 29 vimekamilika na 133 ujenzi unaendelea, ujenzi wa nyumba 114 za watumishi wa afya ambapo nyumba nane (8) zimekamilika na nyumba 106 zipo katika hatua mbalimbali, ujenzi na uendelezaji wa majengo 28 ya wagonjwa wa nje ambapo manne (4) yamemekamilika na yanatumika na 24 ujenzi unaendelea, ujenzi na ukamilishaji wa zahanati 347 ambapo zahanati 28 zimekamilika na 319 utekelezaji upo katika hatua mbalimbali na ujenzi wa wodi 93 ambapo wodi 21 zimekamilika na 72 ujenzi unaendelea;

- (iii) Matengenezo ya Barabara yenye urefu wa kilomita 435.75 kwa kiwango cha lami ambapo kilomita 180.75 matengenezo yamekamilika na kilomita 255 ujenzi unaendelea, ujenzi wa madaraja mawili (2) Manispaa ya Kinondoni unaendelea, ujenzi wa Kalavati tatu (3) Halmashauri ya Wilaya ya Kyela unaendelea, ujenzi wa vivuko vitatu (3) Manispaa ya Morogoro na Wilaya ya Arusha unaendelea, ununuzi magreda 11 kwa ajili ya kuchonga barabara ambapo magreda mawili (2) yamenunuliwa na tisa (9) yapo hatua ya ununuzi, uwekaji wa taa 153 za barabarani

ambapo taa 115 zimewekwa na 38 ujenzi unaendelea;

- (iv) Ujenzi wa machinjio 48 ambapo sita (6) yamekamilika na 42 ujenzi unaendelea, ujenzi wa fremu za maduka 354, fremu 48 zimekamilika na 306 ujenzi unaendelea, ujenzi wa maghala 10 ambapo matatu (3) yamekamilika na saba (7) yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, ujenzi wa vitega Uchumi 15 ambavyo vipo katika hatua mbali mbali za utekelezaji, uanzishwaji wa viwanda vidogo 21 ambapo saba (7) vimekamilika na vinafanya kazi na 14 ujenzi wake unaendelea, ujenzi wa vituo vidogo 54 vya mabasi ambapo vituo 17 vimekamilika na vinatumika na 37 ujenzi unaendelea, ujenzi wa masoko 71 ambapo 16 yamekamilika na yanatumika na 55 ujenzi unaendelea na ujenzi wa maeneo ya minada 27 ambapo mitatu (3) imekamilika na 24 ujenzi upo katika hatua mbalimbali;
- (v) Ununuzi wa magari 26 ambapo sita (6) yamenunuliwa na 20 yapo hatua mbalimbali za ununuzi, kulipa madeni ya wazabuni katika miradi 71, ujenzi wa ofisi za kata 117 ambapo saba (7) zimekamilika na 110 ujenzi unaendelea, ofisi za vijiji 49 ambapo sita (6) zimekamilika na 43 zipo hatua mbalimbali, ofisi za mitaa 87 ambapo 36 zimekamilika na 51 zipo hatua mbalimbali za utekelezaji na ukarabati wa majengo ya utawala 77 ambapo

27 yamekamiliika na 55 ukarabati unaendelea na ununuzi wa POS 266 ambapo 211 zimenunuliwa na 55 zipo hatua ya ununuzi;

- (vi) Kuanzisha mashamba darasa 261 ambapo 29 yamekamiliika na 232 yapo katika hatua mbalimbali ya uanzishwaji, kutoa chanjo 101,551 ya mifugo, ujenzi wa mabwawa tisa (9) upo hatua za ukamilishaji, majosho sita (6) yamejengwa na 23 yapo hatua mbalimbali za ujenzi, mbegu tani 3,211 za mazao ya kimkakati zimegawiwa kwa wakulima, miche 135,546 imegawiwa kwa wakulima kwa ajili ya kuimarisha sekta ya kilimo;
- (vii) Kuendelea na ukamilishaji wa vituo 77 vya polisi kata ambapo 48 vinaendelea kukamilishwa na 29 vipo kwenye hatua za awali za utekelezaji. Shughuli hii inafanywa kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na
- (viii) Hati miliki za ardhi 2,220 zimetolewa, wananchi 84 wamelipwa fidia kupisha ujenzi wa miundombinu ya umma, viwanja 324 vimepimwa na 719 vinaendelea kupimwa, kuandaa michoro ya mipango miji, ununuzi wa vifaa vya kupimia ardhi, matumizi bora ya ardhi na utekelezaji wa zoezi la anuani za makazi.

3.6 Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024

63. ***Mheshimiwa Spika***, Mwaka 2024/25 Ofisi ya Rais – TAMISEMI iliidhinishiwa shilingi bilioni 254.82 kwa ajili ya kuratibu na kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 247.03 kutoka serikali kuu na shilingi bilioni 7.78 ni fedha za mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya uchaguzi. Uchaguzi huu ulihusisha uchaguzi wa viongozi katika ngazi ya msingi ambao ni wenyeviti wa vijiji, mitaa, vitongoji, wajumbe wa halmashauri za vijiji na wajumbe wa kamati za mitaa.

64. ***Mheshimiwa Spika***, shughuli zilizotekelezwa ni uhakiki wa maeneo ya utawala yaliyojumuishwa kata 3,956, vijiji 12,333, mitaa 4,269 na vitongoji 64,274; uandaaji wa nyaraka, uhamasishaji na utoaji wa elimu ya mpiga kura; ununuzi na usambazaji wa vifaa; na uratibu wa usimamizi, ufuatiliaji na uratibu wa upigaji kura kwa ajili ya kuchagua viongozi wa ngazi za vijiji, mitaa na vitongoji katika mamlaka za serikali za mitaa. Aidha, mamlaka za serikali za mitaa zilifanya uandikishaji wa wapiga kura, uteuzi wa wagombea na kampeni.

3.7 Uratibu na Usimamizi wa Huduma za Afya ya Msingi

65. ***Mheshimiwa Spika***, Mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilipanga kutumia shilingi bilioni 357.85 za ruzuku ya fedha za maendeleo za

serikali kuu na washirika wa maendeleo katika Uratibu na Usimamizi wa Huduma za Afya ya Msingi, Ustawi wa Jamii na Lishe.

66. **Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2025 bilioni 166.38 zimepokelewa sawa na asilimia 46.49. Shughuli zifuatazo zimetokelezwa:-

- (i) Hospitali 89 za Wilaya kati ya 118 zilizopangwa kujengwa, kukarabatiwa na kukamilishwa zinaendelea na utekelezaji ambapo hospitali 24 zipo katika hatua za ununuzi na 65 zipo katika hatua za ukamilishaji wa ujenzi;
- (ii) Ukamilishaji wa Vituo vya Afya 16 ambavyo ni Kazima, Lusaba, Mwayaya, Mgunzo, Nyakiobe, Isangawana, Kilasilo, Mahongole, Igava, Kifunda, Isange, Mpata, Ntaba, Nabweko, Senga na Kasu katika Halmashauri 10 za Manispaa ya Mpanda na Halmashauri za Wilaya za Buhigwe, Kakonko, Chunya, Kyela, Mbarali, Busokelo, Ukerewe, Sumbawanga, na Nkasi. Aidha, vituo vya afya vitatu (3) vipo katika hatua za ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu iliyopelekewa fedha za ukamilishaji na vituo vya afya 13 vipo katika hatua za ununuzi na;
- (iii) Ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya hospitali 119 kati ya 136 za Halmashauri; vituo 41 kati ya 44 vya afya katika halmashauri 18 za Jiji la Tanga, Manispaa ya Songea, Musoma, Halmashauri za Wilaya za Makete, Ludewa,

Rufiji, Mkuranga, Nsimbo, Hanang, Nyasa, Mbogwe, Nyang'hwale, Tarime, Kwimba, Buhigwe, Kakonko, Kibondo, na Songwe. Vifaa tiba kwa ajili ya zahanati 356 kati ya 386 katika halmashauri 164. Aidha, vifaa na vifaa tiba vimenunuliwa na MSD inaendelea na taratibu za kukamilisha usambazaji;

- (iv) Ujenzi wa miundombinu ya maji 183 na vyoo 183 katika vituo vya kutolea huduma za afya katika mamlaka za serikali za mitaa 137;
- (v) Huduma za chanjo katika mamlaka za serikali za mitaa 184 kwa watoto chini ya miaka mitano (5) zimetolewa kupitia vituo vya kutolea huduma za afya na kwa njia ya huduma za mkoba (*outreach*) watoto 1,610,303 kati ya 1,556,556 sawa na asilimia 103 walipata chanjo ya *pentavalent* dozi ya tatu (*Penta 3*) na watoto 1,526,884 kati ya 1,556,556 sawa na asilimia 98 walipata chanjo ya surua dozi ya pili;
- (vi) Ukamilishaji wa ujenzi wa zahanati tano (5) ambapo tatu (3) zipo katika hatua za ununuzi, na mbili (2) zipo katika hatua ya plasta, rangi na uwekaji wa milango. Aidha zahanati tano (5) za Idaho, Makutupa, Kinango, Nyamahanga na Ulumi zinajengwa katika Halmashauri za Wilaya ya Mpwapwa, Magu na Kalambo;

- (vii) Kupitia Programu ya Uwekezaji katika Afya ya Mama na Mtoto Tanzania (*Tanzania Maternal Child Health Investment Programme - TMCHIP*) watumishi 300 wa mkataba wameajiriwa katika vituo vya kutolea huduma za afya, ukarabati wa vituo vya afya 25 na zahanati 2, wasimamizi wa miradi 209 walipata mafunzo kutoka ngazi ya mkoa na halmashauri, na magari mawili (2) ya usimamizi yamenunuliwa; na
- (viii) Kupitia Programu ya Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria (*Global Fund*) mafunzo kazini yametolewa kwa waganga wakuu wa halmashauri 53, wasimamizi wakuu 40 na wataalamu 60 wa mionzi kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, usimamizi shirikishi katika afua za UKIMWI, kifua kikuu na malaria umefanyika katika halmashauri 184.

3.8 Usimamizi na Uendeshaji wa Elimumsingi na Sekondari

67. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI inaratibu usimamizi na uendeshaji wa elimu ya awali, msingi na sekondari nchini kupitia mamlaka za serikali za mitaa ambapo shule zenye madarasa ya awali ni 20,607 (18,011 za Serikali na 2,596 zisizo za Serikali); idadi ya shule za msingi 20,533 (18,055 za Serikali na 2,478 zisizo za Serikali) zikiwemo shule maalumu za msingi 37 za bweni na vitengo maalumu 710. Aidha, idadi ya shule za

sekondari ni 6,269 (4,905 za Serikali na 1,364 zisizo za Serikali).

68. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2024/25 Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilipanga kutumia shilingi trilioni 1.02 kupitia ruzuku ya Serikali Kuu na washirika wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli katika sekta ya elimu.

69. **Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2025 bilioni 663.29 zimepokelewa sawa na asilimia 66.00. Shughuli zifuatazo zimetekenezwa:-

(i) **Uandikishaji wa Wanafunzi wa Elimu ya Awali, Darasa la Kwanza na Kidato cha Kwanza**

70. **Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2025 Wanafunzi wa Darasa la Awali walioandikishwa ni 1,501,368 (wavulana 754,902 na wasichana 746,466) wakiwemo wenye mahitaji maalum 3,048 (wavulana 1,649 na wasichana 1,399) sawa na asilimia 80.11 ya watoto 1,873,927 wenye umri wa miaka mitano (5) waliotarajiwa kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi, 2022.

71. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa masomo wa 2025, wanafunzi 1,729,180 walitarajiwa kuandikishwa darasa la kwanza, ambapo hadi Machi, 2025 wanafunzi walioandikishwa ni 1,778,461 (wavulana 890,056 na wasichana 888,405) wakiwemo wenye mahitaji maalumu 3,904 (wavulana 2,143

na wasichana 1,761) sawa na asilimia 102.84 ya lengo.

72. **Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2025 wanafunzi 20,665 (wavulana 11,311 na wasichana 9,354) wakijumuisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu 107 (wavulana 56 na wasichana 51) waliandikishwa katika Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA). Aidha, uandikishaji umeongezeka kwa asilimia 4.04 ikilinganishwa na wanafunzi 19,863 (wavulana 10,775 na wasichana 9,088) walioandikishwa Mwaka 2024.

73. **Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2025 wanafunzi 889,773 (wavulana 411,046 na wasichana 478,727) wakijumuisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu 2,184 (wavulana 1,074 na wasichana 1,110) waliandikishwa kujiunga na kidato cha kwanza sawa na asilimia 91.15 ya lengo.

(ii) **Upimaji na Mitihani ya Kitaifa**

74. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeratibu na kusimamia mitihani ya upimaji wa kitaifa wa darasa la nne na kidato cha pili na mitihani ya kuhitimu darasa la saba, kidato cha nne na sita.

75. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2024, wanafunzi 1,530,911 (wavulana 733,220 na wasichana 797,691) walifanya mitihani ya upimaji wa darasa la nne. Aidha, wanafunzi 1,320,227 (wavulana 620,326 na wasichana 699,901) kati ya 1,530,805 wenye

matokeo sawa na asilimia 86.24 walifaulu. Mwaka 2023 Wanafunzi waliofaulu walikuwa 1,287,934 sawa na asilimia 83.34. Hivyo, kumekuwa na ongezeko la ufaulu kwa asilimia 2.90 kwa wanafunzi waliopata fursa ya kuendelea na darasa la tano ikilinganishwa na Mwaka 2023.

76. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2024 wanafunzi 1,204,899 (wavulana 548,739 na wasichana 656,160) walifanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi, ambapo watahiniwa 1,024,229 (wavulana 449,057 na wasichana 525,172) sawa na asilimia 80.87 ya watahiniwa wenye matokeo walifaulu ikiwa ni ongezeko la asilimia 0.29 la ufaulu wa asilimia 80.58 Mwaka 2023. Aidha, wanafunzi wote waliofaulu walipata nafasi ya kuendelea na elimu ya sekondari.

77. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2024 wanafunzi 801,564 (wavulana 369,731 na wasichana 437,833) walifanya mtihani wa upimaji wa kitaifa wa kidato cha pili, ambapo wanafunzi 680,574 (wavulana 313,117 na wasichana 367,457) kati ya 796,825 wenye matokeo ambao ni sawa na asilimia 85.41 walifaulu kuendelea na Kidato cha Tatu. Mwaka 2023 wanafunzi waliofaulu walikuwa 592,741 sawa na asilimia 85.31.

78. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2024, wanafunzi 517,460 (wavulana 245,542 na wasichana 271,918) walifanya mtihani kidato cha nne. Aidha, watahiniwa wa shule 477,262 (wavulana 228,184 na wasichana 249,078) kati ya 516,695 wenye matokeo ambao ni

sawa na asilimia 92.37 walifaulu. Mwaka 2023 watahiniwa waliofaulu walikuwa 471,427 sawa na asilimia 89.36. Hivyo, ufaulu umeongezeka kwa asilimia 3.01. Kati yao wanafunzi 215,245 (wavulana 117,132 na wasichana 98,113) walikuwa na sifa za kujiunga kidato cha tano au vyuo vya kati.

79. ***Mheshimiwa Spika***, Mwaka 2024, wanafunzi 103,812 (wavulana 57,019 na wasichana 46,793) walifanya mtihani wa taifa wa kidato cha sita, ambapo watahiniwa wa shule waliofaulu ni 103,252 (wavulana 56,637 na wasichana 46,615) sawa na asilimia 99.92 ikilinganishwa na ufaulu wa Mwaka 2023 ambao ulikuwa asilimia 99.90.

80. ***Mheshimiwa Spika***, ufaulu wa mitihani ya kitaifa unadhihirisha jitihada kubwa zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau kwa kuboreshwa kwa mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Aidha, ninawapongeza walimu kwa jitihada kubwa wanazozitoa katika ufundishaji wa wanafunzi.

(iii) **Michezo kwa Shule za Msingi na Sekondari**

81. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuratibu michezo kwa kuhimiza na kusimamia maendeleo yake katika shule za msingi na sekondari. Mwaka 2024 mashindano ya michezo ya Umoja wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) na Umoja wa Michezo Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA) yalifanyika mkoani Tabora tarehe 05 hadi 26 Juni, 2024.

82. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Michezo ya UMITASHUMTA yenye lengo la kutambua na kuendeleza vipaji, jumla ya wanafunzi 3,188 (wavulana 1,600 na wasichana 1,588) walishiriki michezo mbalimbali. Aidha, wanafunzi 3,164 (wavulana 1,591 na wasichana 1,573) walishiriki mashindano ya UMISSETA. Michezo hii ilihusisha wanafunzi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Vilevile, wanafunzi 423 (wavulana 206 na wasichana 217) walishiriki Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wanafunzi wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Agosti, 2024 nchini Uganda.

83. **Mheshimiwa Spika**, mafanikio mbalimbali yamefikiwa katika usimamizi wa michezo shuleni. Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA yameendelea kuwa na mchango mkubwa kwa upatikanaji wa wachezaji wa timu za vijana wa chini ya miaka 15, 17 na 20 kwa michezo yote inayoshindaniwa Tanzania.

84. **Mheshimiwa Spika**, Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wanafunzi wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania imekuwa bingwa katika michezo ya mpira wa wavu wasichana, mpira wa goli wavulana na wasichana, mshindi wa pili netiboli na soka wasichana kwenye mashindano ya wanafunzi wa shule za msingi. Vilevile Tanzania imeshiriki katika mashindano ya Shule ya Dunia ya Mbio za Nyika yaliyofanyika nchini Kenya na kushika nafasi ya tatu kwa

wanamichezo wa umri wa miaka 12 kati ya mataifa 22 yaliyoshiriki mashindano hayo.

(iv) **Mpango wa Elimumsingi Bila Ada**

85. **Mheshimiwa Spika**, maafisa elimu kata 3,931, wakuu wa shule za msingi 18,021 na sekondari 4,944 walipokea posho ya madaraka; jumla ya wanafunzi 376,052 wamepata ruzuku ya chakula ambapo wanafunzi 330,325 wa bweni na wanafunzi 45,727 wa kutwa; na wanafunzi 12,285,382 wamepata ruzuku ya uendeshaji kwa shule za msingi 18,021. Vilevile, jumla ya wanafunzi 305,906 wa sekondari walipata ruzuku ya chakula na fidia ya ada ya bweni, fidia ya ada ya kutwa kwa wanafunzi 2,761,311 na ruzuku ya uendeshaji wanafunzi 3,067,217 kwa shule za sekondari 4,944 imetolewa.

(v) **Ujenzi na Ukamilishaji wa Miundombinu ya Shule**

86. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na umaliziaji wa maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi na miradi viporo katika shule za msingi na sekondari. Ukamilishaji unaoendelea ni madarasa 1,897, mabwalo 241, mabweni 126, majengo ya utawala tatu (3), hosteli 11, maabara 42 na nyumba za walimu sita (6). Aidha, serikali inaendelea na ujenzi wa matundu ya vyoo 2,365 pamoja na miundombinu ya kunawia mikono, kuvunia maji ya mvua na ununuzi wa matanki katika shule za msingi 139 zilizopo katika Mikoa

tisa (9) ya Mara, Shinyanga, Njombe, Tabora, Iringa, Dodoma, Kagera, Tanga na Simiyu.

(vi) **Ununuzi wa Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia**

87. **Mheshimiwa Spika**, serikali imenunua na kusambaza kemikali za maabara katika shule za sekondari za kata 231. Aidha, vifaa vya maabara kwa shule 486 vimenunuliwa katika awamu mbili (2). Vifaa vya awamu ya kwanza vimesambazwa katika shule 231 zikiwemo shule nane (8) kati ya 26 za mikoa za wasichana. Vifaa vya maabara na kemikali kwa awamu ya pili kwa ajili ya shule 255 zilizobaki vinatarajiwa kupokelewa na kusambazwa kabla ya tarehe 30 Juni, 2025.

88. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na taratibu za ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya shule za msingi 600 ambavyo ni *Smart Blackboard 416, All in One Computers 8,672, Multifunction Photocopiers (Black & White) 600, Laptops 600, UPSs 4,936, AI Smart Classrooms 184, LAN (Local Area Network) Equipment and Accessories 184 na Data Cabinets 1,104*. Aidha, vitabu 12,442,258 vikijumuisha vitabu 9,082,650 vya shule za msingi na vitabu 3,359,608 vya shule za sekondari vimenunuliwa na kusambazwa.

3.9 Utawala Bora, Usimamizi wa Rasilimali, Ujenzi wa Majengo ya Utawala na Makazi ya Viongozi

89. ***Mheshimiwa Spika, Hayati Benjamini William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu aliwahi kusema “utawala bora ni msingi wa maendeleo endelevu; bila yake, hatuwezi kufikia malengo yetu”*** kwa muktadha huo Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusimamia shughuli za utawala bora na utatuzi wa kero za wananchi katika mamlaka za serikali za mitaa kama ifuatavyo:

(i) Utatuzi wa Kero za Wananchi katika Mikoa na Wilaya

Mheshimiwa Spika, Hayati Julius Kambarage Nyerere Rais wa Awamu ya Kwanza alisema “Wananchi wanapotoa malalamiko yao, siyo uadui bali ni wajibu wao wa msingi. Ni lazima wasikilizwe na kushughulikiwa”

90. ***Mheshimiwa Spika***, Mwaka 2024/25 ofisi za wakuu wa mikoa ziliidhinishiwa shilingi bilioni 4.56 kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji, utatuzi wa kero na uhamasishaji wa shughuli za maendeleo katika mamlaka za serikali za mitaa. Hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 4.03 zimetolewa sawa na asilimia 88.37. Aidha, katika kipindi hicho kero 70,432 zimeshughulikiwa ambapo kero 52,201 mashauri yake yamefungwa na kero 18,231 zinaendelea na utekelezaji.

(ii) **Usimamizi wa Rasilimali Watu**

Mheshimiwa Spika, Hayati Waziri Mkuu Edward Moringe Sokoine alisema “Ole wake kiongozi mzembe na asiye na nidhamu nitakayemkuta, viongozi wazembe na wabadhirifu wahesabu siku zao. Labda tusiwajue. Hawa hatuna sababu ya kuwapa imani, kuwa tutawalinda kama vitendo vyao viovu”.

91. ***Mheshimiwa Spika***, serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutokuwa na muhali na watendaji wote wazembe na wabadhirifu wa mali za umma ambapo Mwaka 2024/25 watumishi 2,297 wamechukuliwa hatua za kinidhamu, kati yao wakurugenzi ni 09, wakuu wa idara na vitengo 81, watumishi wa sekta ya ujenzi 43 na watumishi 2,164 wa kada nyingine. Hivyo Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kusimamia nidhamu na uwajibikani wa utumishi wa umma.

(iii) **Usimamizi wa Kituo cha Huduma kwa Wateja**

92. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ina Kituo cha Huduma kwa Wateja kwa lengo la kushughulikia malalamiko na kero za wananchi. Hadi Machi, 2025 kituo kimehudumia wananchi 43,710. Aidha, masuala mengi yaliyopokelewa na kusikilizwa kutoka kwa wananchi yalikuwa katika sekta za afya, elimu na ardhi. Kituo kimekuwa msaada kwa wananchi katika kupunguza na kutatua changamoto zinazowakabili na kupata

taarifa sahihi. Wananchi wanakaribishwa kupiga simu Kituo cha Huduma kwa Wateja kupitia namba **0735 160 210** au **0262 160 210** kuanzia saa mbili asubuhi mpaka saa tisa jioni kwa siku za kazi.

(iv) **Uwezeshaji Ngazi za Msingi za Mamlaka za Serikali za Mitaa**

93. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza dhana ya Ugatuuji Madaraka kwa Wananchi, serikali imeendelea kuboresha utendaji kazi katika ngazi za msingi ili kuimarisha utawala bora, maendeleo endelevu, na ushiriki wa wananchi katika maamuzi yanayogusa maisha yao.

94. **Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua umuhimu huo, serikali katika Mwaka 2024/25 ilitenga shilingi bilioni 1.73 za Matumizi Mengineyo kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya posho ya mawasiliano kwa wenyevidi wa vijiji na mitaa. Hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 1.15 zimetolewa sawa na asilimia 66.47 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya posho ya mawasiliano katika halmashauri 165 ambazo mapato yake ni chini ya shilingi bilioni 5 katika vijiji 12,263 na mitaa 2,161.

(v) **Ununuzi wa Magari**

95. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha utekelezaji wa miradi na shughuli za maendeleo zinafanyika na kufuatiliwa kwa karibu, serikali imeendelea kuwezesha upatikanaji wa magari

ambapo hadi Machi, 2025 jumla ya magari 102 yamenunuliwa na kusambazwa katika taasisi, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa. Kati ya magari hayo 39 ni kwa ajili ya usimamizi wa miundombinu ya barabara inayosimamiwa na TARURA; nane (8) wakuu wa mikoa; saba (7) makatibu tawala mikoa, 43 wakuu wa wilaya na matano (5) wakurugenzi wa halmashauri.

(vi) **Ushirikishwaji wa Wananchi kupitia Mfumo wa O&OD Ulioboreshwa**

96. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo katika ngazi za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwa kutumia Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo Ulioboreshwa. Hadi Machi, 2025 jumla ya mikoa 26 na halmashauri 184 zimepata mafunzo kuhusu mfumo ulioboreshwa wa fursa na vikwazo kwa maendeleo ambao umewezeshwa halmashauri kuandaa mipango na bajeti kwa Mwaka 2025/26.

(vii) **Ujenzi wa Majengo ya Utawala na Makazi ya Viongozi**

97. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2024/25, shilingi bilioni 171.34 ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa ofisi za wakuu wa mikoa 16, ukarabati wa ofisi za wakuu wa wilaya 22, ikulu ndogo nane (8), ofisi za maafisa tarafa 19, nyumba 124 za wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa, makatibu tawala

wasaidizi wa mikoa, wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa wilaya, maafisa tarafa, wakurugenzi na wakuu wa idara wa halmashauri; ujenzi wa majengo ya utawala katika halmashauri 72, pamoja na ununuzi wa samani za majengo ya utawala katika halmashauri 50.

98. **Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 53.14 zimepokelewa, sawa na asilimia 84.00 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa majengo ya utawala katika halmashauri 73 ambayo yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, majengo 32 yamekamilika na yanatumika. Kazi zinazoendelea katika majengo hayo ni kazi za nje ikiwemo kujenga uzio, *landscaping*, kibanda cha mlinzi na mgahawa. Majengo 15 yapo katika hatua ya ukamilishaji na baadhi yameanza kutumika wakati shughuli za ukamilishaji zikiendelea, majengo manne (4) yapo hatua ya kuta, majengo matatu (3) yapo hatua ya kupaua, majengo nane (8) yapo hatua ya kumwaga zege la sakafu ya kwanza. Majengo sita (6) yapo hatua ya msingi na majengo matano (5) yapo hatua za ununuzi. Vilevile ununuzi wa samani za majengo ya utawala katika halmashauri 19 unaendelea. Aidha, ukamilishaji wa nyumba 24 za wakurugenzi wa halmashauri unaendelea.

99. **Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 36.09, sawa na asilimia 73.99 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa majengo ya utawala na makazi ya

viongozi na watumishi katika ofisi za wakuu wa mikoa. fedha hizo zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa ikulu ndogo moja (1), ujenzi wa nyumba mbili (2) za viongozi na ukarabati wa ikulu ndogo nne (4), ukamilishaji wa ofisi za wakuu wa mikoa sita (6), ukarabati wa ofisi za wakuu wa mikoa 15, ujenzi wa nyumba za wakuu wa mikoa minne (4) na ukarabati wa nyumba za wakuu wa mikoa mitano (5). Ujenzi wa nyumba za makatibu tawala wa mikoa miwili (2) na ukarabati wa nyumba za makatibu tawala wa mikoa mitatu (3). Ujenzi wa nyumba nne (4) za makatibu tawala wasaidizi. Vilevile, fedha hizo zimetumika kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa ofisi za wakuu wa wilaya 11, ujenzi wa uzio katika ofisi za wakuu wa wilaya nne (4) na ukarabati wa ofisi za wakuu wa wilaya nne (4). Ujenzi wa nyumba za wakuu wa wilaya nne (4), ujenzi wa uzio katika nyumba za wakuu wa wilaya mbili (2) na ukarabati wa nyumba za wakuu wa wilaya za 12. Pia ujenzi wa nyumba za makatibu tawala wa wilaya sita (6) na ujenzi wa uzio katika nyumba za makatibu tawala wa wilaya 14. Ujenzi wa ofisi za tarafa 48 na nyumba za maafisa tarafa sita (6).

3.10 Usimamizi wa Mifumo ya TEHAMA

Mheshimiwa Spika, Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema "Tunahitaji kuwekeza katika TEHAMA ili kuweza kujenga uchumi wa kidijitali ambao utawafaidisha wananchi wote."

100. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2024/25, mifumo ya TEHAMA imeendelea kuboreshwa na kujengwa ili kukidhi mahitaji stahiki katika maeneo ya kiutendaji yanayosimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na kuwezesha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

101. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais -TAMISEMI imetekeleza maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa Mwaka 2024 ya uunganishaji wa mifumo ya TEHAMA. Hadi Machi, 2025 Ofisi ya Rais -TAMISEMI imeunganisha mifumo yake na mifumo ya taasisi 24 za serikali na sekta binafsi ili kuongeza ufanisi wa kumhudumia mwananchi, kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati, kudhibiti upotevu wa mapato na kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

102. **Mheshimiwa Spika**, Mifumo inayosimamiwa na Ofisi ya Rais -TAMISEMI ni pamoja na Mfumo wa Uendeshaji na Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Afya yaani GoTHOMIS. Mfumo huu umeboreshwa na unaendelea kuunganishwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo hadi Machi, 2025, jumla ya vituo 5,505, sawa na asilimia 74.93 ya vituo vya umma ngazi ya afya ya msingi vinatumia mfumo huo. Vituo hivyo ni hospitali teule za wilaya tisa (9), hospitali za wilaya 188, vituo vya afya 883, zahanati 4,431 na kliniki tatu (3). Aidha, wagonjwa zaidi ya milioni sita wamepatiwa huduma kupitia

Mfumo wa GoTHOMIS, kufanikisha rufaa 13,329, kusimamia mapato yanayotokana na uchangiaji, upatikanaji wa taarifa za magonjwa na ugonjwa pamoja na usimamizi wa madawa.

103. **Mheshimiwa Spika**, lengo la Ofisi ya Rais -TAMISEMI ni kuweka Mfumo wa GoTHOMIS katika vituo vyote vya ngazi ya msingi ifikapo Juni, 2025. Vilevile, mfumo huu unatumiwa na vituo vya kutoa huduma ya afya vilivyo chini ya Benki Kuu ya Tanzania, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, baadhi ya vituo vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na taasisi nyingine.

104. **Mheshimiwa Spika**, Mfumo mwingine ulio chini ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI ni Mfumo wa TAUSI ambao umeongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri. Aidha, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia Mfumo wa TAUSI imewezesha:

- (i) Kupunguza matumizi ya fedha mbichi na ucheleweshaji wa kuwasilisha fedha benki;
- (ii) Kumwezesha mwananchi kununua viwanja vinavyouzwa na halmashauri nchini;
- (iii) Kumwezesha mteja kujihudumia mwenyewe hata akiwa nje ya nchi na kupata huduma pasipo kufika ofisi za halmashauri;
- (iv) Kupunguza muda wa kupata huduma za leseni na vibali na kuwezesha utoaji wa leseni na vibali kielektroniki;

- (v) Kuwa na taarifa sahihi za walipakodi na watumiaji kwa kutumia Namba ya Utambulisho ya Taifa (NIDA) na Namba ya utambulisho wa mlipa kodi yaani *TIN*; na
- (vi) Kukusanya mapato kupitia *Control Number* Jumuishi.

105. **Mheshimiwa Spika**, Mfumo wa TAUSI unasomana na mifumo ya Mamlaka ya Serikali Mtandao, Wizara ya Fedha, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma, Baraza la Sanaa Tanzania, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Zoezi linaendelea kuziunganisha taasisi za Mfuko wa Bima ya Afya, Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi, Mamlaka ya Usafirishaji Nchi Kavu na Jeshi la Polisi Tanzania.

106. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeanza utoaji wa mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa kutumia Mfumo wa Wezesha. Matumizi ya mfumo huu yamesaidia kuondoa changamoto zilizokuwepo awali ikiwa ni pamoja na kudhibiti uwepo wa vikundi hewa, watu kujisajili katika kikundi zaidi ya kimoja na wakopaji hewa. Vilevile, mfumo umeimarisha usimamizi, usajili wa vikundi, utoaji na urejeshaji wa mikopo, upatikanaji wa taarifa sahihi za mikopo kwa wakati, kuondoa upendeleo na kuongeza uwazi na uwajibikaji. Mfumo huu utaunganishwa na mifumo ya benki kuwezesha kutoa mikopo hii kwa halmashauri 10 zitakazotumia mabenki.

107. **Mheshimiwa Spika**, katika kuendelea kuboresha utoaji wa huduma bora za afya kidijitali, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Vodacom *Foundation* imeendelea kuboresha Mfumo wa Huduma ya Usafiri wa Dharura kwa Mama Wajawazito na Watoto Wachanga yaani M-MAMA ambapo gharama za usafiri wa dharura zimepungua kwa asilimia 33 ikilinganishwa na matumizi ya magari ya kubebea wagonjwa peke yake. Matumizi ya mfumo huu yamepunguza muda wa kumhudumia mgonjwa kwa asilimia 50 sambamba na watumiaji kuongezeka kutoka 45,000 hadi 70,000 kwa mwaka. Aidha, Mfumo wa M-MAMA ni moja kati ya afua zilizochangia kupunguza vifo vya kinamama kutoka vifo 504 kwa vizazi hai 100,000 hadi vifo 104.

108. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imekamilisha uboreshaji na kuanza matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Shule unaosaidia kupata taarifa za shule kwa wakati, kufuatilia maendeleo ya wanafunzi kimasomo, kung'amua vihatarishi vya uoro kwa wanafunzi vinavyoweza kusababisha wanafunzi kuacha shule na hivyo kuwezesha waalimu kuchukua hatua mapema. Mfumo huu unatumika katika shule zote za umma na zisizo za umma nchini katika ngazi ya elimumsingi na sekondari.

109. **Mheshimiwa Spika**, ili kuiwezesha serikali kuwa na picha kamili ya nguvu kazi ya walimu kote nchini, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa

kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imebuni na kuanza ujenzi wa kanzidata (Mwalimu *Data Lake*) itakayotunza taarifa za uzalishaji wa walimu, ajira na uendelezaji wao.

110. **Mheshimiwa Spika**, Mfumo wa Mwalimu *Data Lake* utaunganishwa na mifumo kutoka Sekretarieti ya Ajira (*Ajira Portal*), Tume ya Vyuo Vikuu (Mfumo wa UIMIS), Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo - NACTVET (Mfumo wa TVET-MIS), Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekinolojia (Mfumo wa TCMS na TE-MIS), Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (Mfumo wa OS-MIS), Tume ya Utumishi ya Walimu (Mfumo wa TSC-MIS) pamoja na Taasisi ya Elimu – TIE (Mfumo wa Kusimamia Taarifa za Uendelezwaji wa Walimu).

111. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma katika ngazi ya msingi na vituo vya kutoa huduma zaidi ya elfu hamsini kupitia Mfumo wa Uhasibu na Utoaji wa Taarifa katika Vituo vya Kutolea Huduma yaani FFARS. Mfumo huu unaongeza uwazi, uwajibikaji, na ufanisi wa usimamizi wa rasilimali za umma. Aidha, mfumo huu unaziwezesha shule na vituo vya afya kutoa taarifa za fedha (mapato na matumizi) kwa wakati halisi na kuongeza ufanisi wa upangaji wa bajeti.

112. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Wizara ya Fedha, mfumo unaboresha ili kuendelea kusomana na mifumo mingine kama Mfumo wa

Uhasibu Serikalini, Mfumo wa Mipango na Bajeti na benki kwa kuzingatia mahitaji na maelekezo mapya na kuimarisha usimamizi bora wa fedha za umma. Huu ni uthibitisho wa dhamira ya Serikali katika kujenga mifumo thabiti ya uwajibikaji kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu. Dhamira ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI katika Mwaka 2025/26 mfumo huu utumike kwenye kata, vijiji, mitaa, shule na vituo vyote vya kutoa huduma za afya.

113. ***Mheshimiwa Spika***, Februari, 2025 Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilifanikiwa kupata tuzo nane (8) za TEHAMA zilizoandaliwa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Tuzo hizi zinadhihirisha mafanikio makubwa ya mapinduzi ya TEHAMA yanayofanywa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Kwa ufafanuzi wowote wa namna ya kutumia mifumo hii ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, wananchi wanakaribishwa kupiga simu Kituo cha Huduma kwa Wateja.

3.11 Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu

Mheshimiwa Spika, Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema “Mikopo ya asilimia 10 ni njia mojawapo ya kusaidia jamii katika kuleta usawa wa kijamii na kiuchumi”.

114. ***Mheshimiwa Spika***, Mwaka 2024/25 serikali ilitarajia kutoa mikopo ya shilingi bilioni 227.96, ambapo shilingi bilioni 63.67 ni fedha za marejesho

zilizokusanywa kutokana na mikopo iliyotolewa kabla ya kusimamishwa. Aidha, shilingi bilioni 63.24 ni fedha zilizokuwa zinatengwa kwa ajili ya mikopo na shilingi bilioni 101.05 ni fedha ambazo zimetengwa kutokana na makadirio ya makusanyo ya mapato ya ndani ya Mwaka 2024/25.

115. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 82.84 zilikopeshwa kwa vikundi 8,275 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 40.71 kwa vikundi 4,557 vya wanawake, shilingi bilioni 36.64 kwa vikundi 2,827 vya vijana na shilingi bilioni 5.48 kwa vikundi 891 vya watu wenye ulemavu. Aidha, hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 14.04 zimerejeshwa kutoka vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

3.12 Huduma Ndogo za Fedha

116. ***Mheshimiwa Spika***, Mwaka 2024/25 mamlaka za serikali za mitaa ziliidhinishiwa shilingi bilioni 4.76 kwa ajili ya uratibu wa huduma ndogo za fedha ambapo hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 3.17 zimetolewa sawa na asilimia 66.59 kwa ajili ya uratibu wa huduma ndogo za fedha kwenye sekta ndogo ya fedha ambapo vikundi 58,271 vimesajiliwa.

3.13 Usimamizi wa Mazingira, Uhifadhi wa Maliasili na Mabadiliko ya Tabianchi

117. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea na uratibu wa shughuli za usimamizi wa mazingira, ulinzi maliasili pamoja na

uratibu wa mabadiliko ya tabianchi. Mafunzo kwa wataalamu 45 wa mikoa sita (6) na halmashauri 15 zilizoanza utekelezaji wa Biashara ya Kaboni na uhifadhi wa bioanuwai yametolewa. Aidha, mafunzo ya kuhimili athari ya mabadiliko ya tabianchi yametolewa kwa wenyeviti/mameya wa halmashauri, wakurugenzi, wakuu wa idara za mipango wa halmashauri 184 na makatibu tawala wasaidizi wa sehemu ya mipango na uratibu wa mikoa 26.

118. ***Mheshimiwa Spika*** hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 12.93 zimepokelewa kutokana na mauzo ya hewa ya kaboni yaliyoishia Mwezi Novemba, 2024 kutokana na uhifadhi wa Maliasili kwa Halmashauri za Tanganyika, Mbulu, Kiteto na Karatu. Mapato hayo yametolewa na Kampuni ya Kaboni Tanzania kwa kuzingatia Kanuni ya Udhhibiti na Usimamizi wa Kaboni nchini za Mwaka 2022.

3.14 Uendelezaji Vijiji na Miji

119. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imesimamia ofisi za wakuu wa mikoa na mamlaka za upangaji kwa kushirikiana na wizara za kisekta, sekta binafsi, wadau wa maendeleo wa jamii kwa jumla katika kuandaa na kutekeleza mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 3,641 sawa na asilimia 29.52 kati ya vijiji 12,333 vilivyopo nchini. Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imezielekeza halmashauri za wilaya zisimamie ipasavyo uendelezaji wa maeneo ya visiwa na fukwe kwenye maeneo yao ya utawala.

120. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi imeweza kufuatilia urejeshwaji wa mkopo wa bilioni 49.47 ambao ulikopeshwa kwa halmashauri 51 kwa ajili ya Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK) ambao unalenga kuboresha utoaji wa huduma za ardhi. Hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 32.21 kati ya bilioni 49.47, sawa na asilimia 65.11 ya fedha zilizokopeshwa zimerejeshwa. Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaendelea kufuatilia halmashauri ambazo bado hazijakamilisha kulipa mikopo hiyo na kuhakikisha zinalipa katika bajeti ya Mwaka 2025/26.

3.15 Ujenzi, Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Wilaya

121. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2024/25 ziliidhinishwa shilingi bilioni 908.16 kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara kupitia Mfuko wa Barabara, Tozo ya Mafuta, Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na washirika wa maendeleo. Hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 468.40 zimetolewa kwa ajili ya miundombinu ya barabara na usafirishaji, sawa na asilimia 55.68 ya fedha zilizoidhinishwa.

122. **Mheshimiwa Spika**, naomba kunukuu maneno ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyasema akiwa Wilaya ya Kalambo Mkoa wa Rukwa Julai, 2024.

"Ninatoa wito kwa wasafirishaji wote nchini pamoja na wananchi kuhakikisha wanalinda miundombinu ya barabara inayojengwa na Serikali kwa kutofanya shughuli za kijamii kama kulima, kuchimba pembezoni mwa barabara pamoja na kazi nyingine zinazoathiri barabara. Ujenzi wa barabara ni gharama sana, ukijenga kilomita moja ya barabara ni sawa na kujenga vituo vitatu vya afya pamoja na kuweka vifaa tiba ndani yake, hivyo niwaombe sana tutunze barabara zetu."

123. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali ya Awamu ya Sita kwa kulitambua hilo, imeendelea kutoa fedha kupitia TARURA kwa ajili ya ujenzi, matengenezo na ukarabati wa barabara kutoka shilingi bilioni 275 Mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 772.19 Mwaka 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 180.80 ya fedha za ndani.

124. ***Mheshimiwa Spika***, ongezeko hili la fedha limewezesha kujenga barabara za lami kilomita 1,442.30, barabara za changarawe kilomita 19,879.21 na madaraja 3,195 yanayohudumiwa. Kutokana na ongezeko la fedha, kazi zimeongezeka ambapo makandarasi wa ndani wamenufaika na ongezeko hilo la fedha, hivyo wastani wa mikataba 844 ya kazi za barabara imeongezeka na kufikia wastani wa mikataba 1,167.

125. ***Mheshimiwa Spika***, Shughuli zilizotekelezwa hadi Machi, 2025 ni kama ifuatavyo: -

- (i) Fedha za Mfuko wa Barabara zimetumika kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 4,057.74, ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 2.75, barabara za changarawe zenye urefu wa kilomita 32.36 na ukarabati wa madaraja 15, makalavati 52 na mifereji ya kuondoa maji barabarani yenye urefu wa mita 23,972.14 katika wilaya 139 za Tanzania Bara;
- (ii) Fedha za tozo ya mafuta zimetumika kujenga barabara za lami zenye urefu wa kilomita 8.0, ujenzi wa barabara za changarawe zenye urefu wa kilomita 992 na ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua yenye urefu wa mita 7,338. Fedha za Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali zimetumika kujenga barabara za lami zenye urefu wa kilomita 61.77, ujenzi wa barabara za changarawe kilomita 435.26 na makalavati 90;
- (iii) Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia TARURA kwa kushirikiana na Benki ya CRDB imeratibu uanzishwaji wa Hati Fungani ya Miundombinu iitwayo Samia *Infrastructure Bond* iliyolenga kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 150 ambapo hadi dirisha la ununuzi wa hisa lilipofungwa shilingi bilioni 323.00 sawa na asilimia 215.33 zimekusanywa na zitatumika kuwakopesha (kwa masharti nafuu) makandarasi watakaolingia mikataba ya kazi na TARURA. Hii itamrahisishia mkandarasi kupata haraka fedha za kuanza kazi kwa miradi ambayo haina kipengele cha malipo ya

awali. Aidha, itawezesha uwepo wa fedha zinazoweza kukopwa (kwa masharti nafuu) na mkandarasi mwenye mkataba na TARURA na kuwezesha kukamilisha mradi kwa wakati na hivyo kuepuka gharama za kuhudumia mradi zaidi ya muda uliopangwa na hivyo mkandarasi kupata faida zaidi;

- (iv) Programu ya Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini (*Roads to Inclusion and Socioeconomic Opportunities – RISE*) inaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa barabara za lami za Wenda – Mgama kilomita 19 na Mtili – Ifwagi kilomita 14 zilizopo Halmashauri za Wilaya ya Iringa na Mufindi mtawalia. Aidha, taa za barabarani 170 kwenye barabara hizo zinaendelea kuwekwa. Vilevile, madaraja 35 kati ya madaraja 130 yamekamiliika na kazi nyingine zinaendelea zikiwa zimefikia asilimia 70 kupitia Miradi ya Uondoaji Vikwazo vya Upitikaji. Ujenzi wa barabara awamu ya pili za Halmashauri za Wilaya za Handeni, Ruangwa na Mbogwe tayari nyaraka za zabuni zinasubiri kupitishwa baada ya marekebisho toka Benki ya Dunia;
- (v) Mradi wa Kuboresha Miundombinu Shindanishi katika Miji 45 Tanzania - *Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness (TACTIC)* unatekelezwa kama ifuatavyo:
 - (a) Kuendelea na ujenzi wa barabara kilomita 147.54 katika halmashauri 12 na mitaro ya maji ya mvua kilomita 24.66 katika Miji

ya Dodoma, Kahama, Mbeya, Kigoma na Morogoro ambapo kilomita 25.23 sawa na asilimia 17 zimekamiliwa. Aidha, mikataba ya ujenzi wa masoko tisa (9), stendi za mabasi tano (5), stendi ndogo mbili (2) na ujenzi wa ghala la kuhifadhia mazao imeisainiwa na makandarasi wameanza ujenzi;

(b) Kazi iliyofanyika kundi la pili la mradi katika halmashuri za miji 15 ni ununuzi wa makandarasi unayotarajiwa kukamilishwa Aprili, 2025. Aidha, utekelezaji wa kundi la pili utakapokamilika itajengwa miundombinu ya barabara za lami kilomita 141.56, daraja moja (1), mifereji kilomita 31.15, masoko 12, maeneo mawili (2) ya kupumzikia na stendi za mabasi sita (6);

(c) Kazi iliyofanyika kundi la tatu katika Halmashauri za miji 18 ni maandalizi ya kuanza usanifu wa miradi inayotarajiwa kutekelezwa katika miji hiyo. Aidha, awamu hii inatarajia kujenga barabara za lami zenye urefu wa kilomita 89.40, mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita 5.0, masoko 16 na stendi za mabasi 14;

(vi) Mradi wa Uendelezaji wa Bonde la Mto Msimbazi upo katika hatua za utekelezaji ambapo kazi zinazoendelea kutekelezwa ni

pamoja na taratibu za ununuzi wa mkandarasi wa kuchimba na kujenga kingo za Mto Msimbazi na mtaalamu mshauri atakayesimamia kazi;

- (vii) Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam Awamu ya Pili (*Dar es Salaam Metropolitan Development Project II – DMDP II*) unaendelea ambapo kazi zinazotekelezwa ni pamoja na ukamilishaji wa taratibu za ununuzi wa ujenzi wa barabara kilomita 148 zitakazojengwa katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuingia mikataba 17 yenye thamani ya shilingi bilioni 411.00. Aidha, malipo ya awali ya shilingi bilioni 28.53 kwa makandarasi nane (8) watakaotekeleza miradi hiyo yamefanyika;
- (viii) Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia TARURA inaendelea na utekelezaji wa miradi kwa teknolojia za *Ecoroads*, *Ecozyme* na *GeoPolymer*. Hadi sasa kwa kutumia teknolojia ya *Ecoroads*, ujenzi wa barabara ya Itilima Oil – Ikindilo kilomita 5.2 Wilaya ya Itilima kwa kutumia teknolojia ya *Ecozyme* umefikia asilimia 95 na utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya Himo - Makuyuni - Lotima kilomita 6.16 Wilaya ya Moshi kwa kutumia teknolojia ya *Ecoroads* unaendelea na umefikia asilimia 65 ya utekelezaji;
- (ix) Madaraja 82 yamejengwa kwa kutumia malighafi ya mawe inayopatikana karibu na eneo la ujenzi kwa gharama ya shilingi bilioni

8.7 ambapo ingekuwa shilingi bilioni 17.4 kama yangejengwa kwa zege; na

- (x) Mradi wa *Agriconnect* unaendelea na unahusisha ujenzi wa barabara za Itulahumba - Igwachanya (kilomita 19.25) - Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Ndulilo - Itete (kilomita 8.9) - Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Lwangwa - Kejo Gas (kilomita 6.41) - Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo, Kidabaga - Bomalang'ombe (kilomita 1.10) - Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, Bomalang'ombe Mwatasi - Kibengu Road (kilomita 13.3) Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, Ilolo - Ndolezi (kilomita 11.01) - Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, *Park at Old Airport* (kilomita 1.5) - Halmashauri ya Jiji la Mbeya na Utili - Mahande (kilomita 14.414) - Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

126. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia TARURA iliidhinishiwa fedha za dharura shilingi bilioni 71.46 kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya miundombinu ya barabara zilizoathiriwa na mafuriko ya maji ya mvua. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 50 ni nyongeza ya bajeti kwa Mwaka, 2024/25. Hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 8.01 zimepokelewa sawa na asilimia 11.28.

127. **Mheshimiwa Spika**, Shughuli zilizotekelezwa kwa fedha za dharura za ndani ni pamoja na kurekebisha barabara zenye urefu wa kilomita 78 na daraja moja (1) la waenda kwa miguu. Aidha,

tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutoa fedha ili kurejesha hali ya barabara za vijijini na mijini ambazo huathiriwa na maji ya mvua za msimu.

128. **Mheshimiwa Spika**, kuanzia mwishoni mwa Mwaka 2023 nakuendelea mpaka Mei, 2024, kulijitokeza mvua nyingi zisizo za kawaida ambazo ziliharibu miundombinu mingi ya barabara na kusababisha kukatika kwa mawasiliano. Fedha zilizohitajika kutengeneza miundombinu hiyo ni takribani shilingi bilioni 250. Kupitia miradi ya Benki ya Dunia inayoendelea hapa nchini chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Benki ya Dunia kupitia madirisha ya *Contingent Emergency Response Component* (CERC) chini ya mradi wa DMDP2 na *Crisis Response Window* (CRW) chini ya mradi wa RISE imetoa jumla ya shilingi bilioni 235 kwa ajili ya kutengeneza miundombinu ya barabara iliyoharibika. Kupitia CERC shilingi bilioni 170 zimeidhinishwa na CRW shilingi bilioni 65 zimeidhinishwa. Miradi hii itatekelezwa katika mikoa yote 26 Tanzania Bara. Utekelezaji wa CERC kupitia DMDP2 umeanza ambapo hadi sasa mikataba 30 ya jumla ya shilingi bilioni 12 imesainiwa kwa ajili ya matengenezo na taratibu za ununuzi zinaendelea kwa miradi mingine inayohitaji usanifu wa kina.

3.16 Huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka

129. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia DART inaendelea na usimikaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji Nauli (*Automated*

Fare Collection System-AFCS) ambao utafungamanishwa na Mfumo wa Kuongozea Magari (*Intelligent Transport System - ITS*) ikiwa ni sehemu ya maboresho endelevu ya huduma hii kwa wananchi waishio mijini, na pia kuondoa mianya ya upotevu wa mapato yatokanayo na nauli.

130. **Mheshimiwa Spika**, Hadi Machi, 2025 Wakala imesambaza kadi janja 62,000 kati ya 200,000 za kukusanyia mapato na kusimika mageti janja kwenye vituo vyote 27. Aidha, mapato yanatarajiwa kuongezeka kutoka shilingi milioni 100 hadi milioni 120 kwa siku baada ya kuanza kutumia kadi janja.

3.17 Shirika la Masoko ya Kariakoo

131. **Mheshimiwa Spika**, shirika lilipanga kuboresha mazingira ya kufanyia biashara ambapo wafanyabiashara watapangwa katika jengo jipya lenye ghorofa nane na jengo lililokarabatiwa. Hadi Machi, 2025 Shirika limetekeleza shughuli zifuatazo;

- (i) Wafanyabiashara 1,520 waliohakikiwa na kukidhi vigezo vya kurejeshwa sokoni tayari wameshapangiwa maeneo ya kufanyia biashara kwenye Mfumo wa TAUSI. Aidha, maeneo mengine 387 yatatangazwa katika Mfumo wa TAUSI kwa ajili ya kuingizwa katika mnada;

- (ii) Kamera 40 zimesimikwa kwa ajili kuimarisha ulinzi na usalama katika soko;
- (iii) Kutenga maeneo manne (4) ya mashine za kutolea fedha na maeneo mawili (2) kwa ajili ya huduma za kibenki;
- (iv) Kutenga eneo la maegesho ya magari lenye uwezo wa kuegesha magari 138;
- (v) Kuboresha mpangilio wa maeneo 1,907 ya biashara katika soko linalokarabatiwa na linalojengwa tofauti na hapo awali kwa kuzingatia aina ya biashara zinazofanana kuuzwa katika eneo moja *market segmentation*;
- (vi) Kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba la Taifa tumefanya upembuzi yakinifu wa awali kwa ajili ya mradi wa uwekezaji wa kibiashara katika eneo la Mbezi Beach Makonde;
- (vii) Kuboresha mikataba ya Shirika na wafanyabiashara ambayo itatumika kwenye Soko la Kariakoo ili kuendana na mabadiliko ya soko, mahitaji ya kibiashara na kupunguza migogoro ya baadae;
- (viii) Kuwajengea uwezo watumishi 29 juu ya matumizi ya mifumo mbalimbali ya kiutendaji na utekelezaji wa shughuli za Shirika ikiwemo Mfumo wa TAUSI na Mfumo wa Mpango na Bajeti; na

- (ix) Ukarabati wa nyumba tatu (3) ambapo nyumba moja (1) Mbezi Beach Makonde na nyumba mbili (2) Tabata Bima.

3.18 Chuo cha Serikali za Mitaa

132. **Mheshimiwa Spika**, Chuo kilipanga kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa waheshimiwa madiwani, wenyeviti wa vijiji, wenyeviti wa mitaa pamoja na wenyeviti wa vitongoji katika halmashauri zote 184 nchini katika masuala mbalimbali yanayohusu uendeshaji wa mamlaka za serikali za mitaa; Kufanya tafiti 30 na kutoa ushauri elekezi kwa serikali kuu, mamlaka za serikali za mitaa, mashirika na watu binafsi juu ya masuala mbalimbali ya maendeleo na kuimarisha mifumo ya TEHAMA; Kuandaa Mtaala wa Shahada ya Kwanza ya Nyaraka na Kumbukumbu; Kuendeleza watumishi 27 katika ngazi mbalimbali za elimu; na kujenga miundombinu ya chuo ikiwemo ofisi ndogo, jengo la mhadhara lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 na nyumba ya mtumishi.

133. **Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2025 Chuo kimetekeleza shughuli zifuatazo;

- (i) Kudahili wanafunzi wa mwaka wa kwanza 6,805 kati ya 9,300;
- (ii) Kutoa mafunzo kwa wenyeviti wa vijiji 8,117, wenyeviti wa mitaa 3,126 na wenyeviti wa vitongoji 37,237 katika halmashauri 116 kati ya 184 waliochaguliwa katika Uchaguzi wa Serikali za

Mitaa uliofanyika Novemba, 2024. Aidha, chuo kimetoa mafunzo kwa waheshimiwa madiwani 68 kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita na Halmashauri ya Mji Babati. Lengo la mafunzo haya ilikuwa kuwajengea uwezo washiriki kuhusu maadili ya viongozi, usimamizi wa mapato, kuibua miradi na kusimamia utekelezaji wake, uendes haji wa vikao vya kisheria na uendes haji wa shughuli katika mamlaka za serikali za mitaa;

- (iii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa kutumia Mfumo wa Ujifunzaji Kielekitroniki (MUKI) kwa waheshimiwa madiwani 1,570 na watendaji wa vijiji na mitaa 2007 kutoka katika halmashauri 31;
- (iv) Kufanya tafiti mbili (2) na machapisho 30 ya kitaaluma katika majarida ya kitaifa na kimataifa yenye lengo la kuboresha utendaji katika mamlaka za serikali za mitaa;
- (v) Kufungamanisha mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji mapato na udahili wa wanafunzi ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma na kudhibiti mapato;
- (vi) Kuandaa na kukamilika kwa mtaala wa Shahada ya Kwanza ya Nyaraka na Kumbukumbu ambapo masomo yataanza kutolewa mwaka wa masomo 2025/26;

- (vii) Kuendeleza kitaaluma watumishi 27 katika shahada za uzamivu 11, uzamili 11 na shahada ya kwanza watano (5); na
- (viii) Ukarabati wa miundombinu ya maji na umeme katika mabweni ya wanafunzi na nyumba za watumishi umefanyika ambapo shilingi milioni 61.37 zimetumika.

3.19 Shirika la Elimu Kibaha

134. ***Mheshimiwa Spika***, Shirika lilipanga kutoa elimumsingi kwa wanafunzi 3,141 na elimu ya sekondari kwa wanafunzi 329; Kukamilisha, kuandaa na kusimamia mfumo wa mafunzo kwa njia ya mtandao; Kutoa elimu ya sekondari mubashara kwa shule za sekondari nchini; Kuboresha utoaji wa elimu kwa wahudumu wa afya 512 katika fani ya utabibu na uuguzi kupitia Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha.

135. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile chuo kilipanga kutoa elimu ya afya dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza kwa wananchi; kutoa elimu na mafunzo ya stadi za ujuzi na ubunifu katika fani za umeme wa majumbani, ufundi wa magari, uundaji na uungaji vyuma, ujenzi (useremala, uashi na bomba), kilimo, mifugo, upishi, na ushonaji kwa vijana 400 kwa kozi za muda mrefu na wananchi 1,000 kwa kozi za muda mfupi kwa mafunzo ya ana kwa ana na kwa njia ya mtandao; na kufanya ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha.

136. **Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2025
Shirika limetekeleza shughuli zifuatazo;

- (i) Elimumsingi imetolewa kwa wanafunzi 3,282 sawa na asilimia 104 ya lengo na elimu ya sekondari imetolewa kwa wanafunzi 315 sawa na asilimia 96 ya lengo. Aidha, Shirika limetoa huduma za maktaba kwa wananchi 25,496 ambapo wananchi 24,221 walisoma vitabu na machapisho mbalimbali ndani ya maktaba na wananchi 1,275 waliazima vitabu kwa ajili ya kwenda kujisomea nyumbani;
- (ii) Kukamilisha maandalizi ya mada za nadharia kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa Mradi wa Utoaji wa Elimu ya Sekondari kwa njia ya masafa. Aidha, Shirika limeendelea kusimamia ufundishaji wa elimu ya sekondari mubashara kupitia madarasa janja yaliyopo Shule ya Sekondari Kibaha ambapo wanafunzi wa shule tatu (03) za sekondari ambazo ni Shule ya Sekondari Dodoma (Dodoma), Shule ya Sekondari Tumekuja (Zanzibar) na Shule ya Sekondari Dkt. Samia (Dodoma) wa masomo ya sayansi wameendelea kufundishwa kwa njia ya mtandao mubashara kwa siku za Jumatano na Ijumaa;
- (iii) Mafunzo kwa kada mbalimbali za afya yametolewa kwa wanachuo 564 sawa na asilimia 110 ya lengo. Kati ya hizo kada ya uuguzi na ukunga kwa wanachuo 240, utabibu kwa wanachuo 285 na uhudumu wa afya ngazi ya

jamii kwa wanachuo 39. Kada ya uhudumu wa afya ngazi ya jamii ni kozi mpya iliyoanza kutolewa Mwezi Septemba, 2024 na ina mwitikio mkubwa;

- (iv) Elimu ya afya dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza ilitolewa kwa wananchi 324 sawa na asilimia 65 ya lengo; na
- (v) Elimu na mafunzo ya stadi za ujuzi na ubunifu katika fani za umeme wa majumbani, ufundi wa magari, uundaji na uungaji vyuma, ujenzi (useremala, uashi na bomba), kilimo, mifugo, upishi, na ushonaji imetolewa kwa vijana 315 sawa na asilimia 79 ya lengo kwa kozi za muda mrefu. Aidha, kwa upande wa kozi za muda mfupi, elimu ya ujasiriamali na udereva ilitolewa kwa wahitaji 154.

3.20 Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa

137. **Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ilipanga kukusanya marejesho ya mikopo yenye jumla ya shilingi bilioni 1.25; Kukusanya michango ya shilingi bilioni 2.62; Kutoa mikopo kwa Halmashauri zitakazokidhi vigezo vya kukopeshwa na kufanya uwekezaji kwenye Taasisi za fedha, Kukamilisha mapitio ya sheria ili kuboresha utendaji wa Bodi; Kutoa mafunzo kwa ajili ya kuboresha usimamizi na utoaji wa mikopo katika mamlaka za serikali za mitaa na kuweka mikakati ya kuboresha mtaji kwa kuandika maandiko ili kupata fedha kwa ajili ya

kuongeza Mtaji. Hadi kufikia Machi, 2025 Bodi imetekeleza shughuli zifuatazo;

- (i) Ufuatiliaji wa Marejesho ya mikopo yenye jumla ya shilingi bilioni 1.25 umefanyika kwenye Halmashauri saba (7) kati ya Halmashauri 10 zilizokopeshwa na Taasisi. Katika ufuatiliaji huo, jumla ya shilingi milioni 517.26 sawa na asilimia 41.22 ya lengo zilikusanywa kutoka Halmashauri za Manispaa ya Singida na Morogoro, Halmashauri ya Mji wa Mbinga na Halmashauri ya Wilaya za Kishapu, Ruangwa, Mlele na Mbinga. Aidha, Halmashauri ya Manispaa ya Singida imemaliza kulipa mkopo wake wa shilingi milioni 28, Pia Halmashauri ya Manispaa ya Songea na Halmashauri za Miji ya Kasulu na Makambako bado zinaendelea na utekelezaji wa miradi hivyo muda wa kuanza kurejesha bado haujafika;
- (ii) Ufuatiliaji wa Mchango wa Akiba na Nyongeza ya Mtaji wenye jumla ya shilingi bilioni 2.62 umefanyika kwenye Halmashauri 40 kati ya Halmashauri 114 ambazo bado hazijakamilisha michango. Katika ufuatiliaji huo, jumla ya shilingi milioni 73.77 sawa na asilimia 2.82 ya lengo zimekusanywa kutoka Halmashauri 10 za Manispaa ya Morogoro, Halmashauri ya Mji wa Bunda na Halmashauri ya Wilaya za Itilima, Ikungi, Bukoba, Makambako, Itigi, Rungwe, Songea na Urambo. Aidha, katika

kipindi hiki, Halmashauri ya Wilaya za Njombe, Songea, Mbinga na Itigi ziliweza kukamlisha michango yao;

- (iii) Bodi inaendelea na marekebisho ya sehemu ya (V) ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura ya 290 inayohusu usimamizi na uendeshaji wa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa;
- (iv) Bodi imewekeza shilingi milioni 827.00 kwenye Soko la Hisa kwenye Benki ya CRDB ambapo inatarajia kupata gawio la wastani wa shilingi milioni 65.00 kwa mwaka; na
- (v) Bodi imeidhinisha mikopo yenye jumla ya shilingi milioni 537.21 ambapo shilingi milioni 270.00 ni kwa ajili ya mradi wa kiwanda cha kutengeneza kuni mbadala kwa ajili ya kupikia kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nyangh'wale na shilingi milioni 267.21 ni mkopo wa nyongeza kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Soko la Kisasa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo.

3.21 Tume ya Utumishi wa Walimu

138. **Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2025 Tume imetumia shilingi bilioni 16.04 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zifuatazo;

- (i) Wilaya 139 zilifanya vikao viwili (2) vya kisheria kila wilaya, ambapo jumla ya tuhuma za kinidhamu 1,379 zilipokelewa na

mamlaka ya nidhamu ngazi ya wilaya kutoka kwa waajiri. Kati ya mashauri hayo, mashauri ya nidhamu 1,141 yalifanyiwa uchunguzi na mashauri 238 yapo katika hatua mbalimbali za maamuzi;

- (ii) Vikao vitatu (3) vya kisheria vilifanyika ambapo rufaa 64 zilitolewa uamuzi;
- (iii) Walimu 158,916 walipandishwa vyeo sawa na asilimia 214 ya waliokasimiwa. Vilevile, walimu 2,358 walibadilishiwa muundo baada ya kujiendeleza kati ya walimu 5,027 walioomba;
- (iv) Mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi makao makuu unaendelea na umefikia asilimia 51 ya utekelezaji;
- (v) Usimikaji wa miundombinu ya TEHAMA kwenye ofisi 139 za wilaya umekamilika;
- (vi) Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaoajiriwa kwenye Utumishi wa Umma umeandaliwa na kukamilika; Mwongozo huu unatarajia kusambazwa kwa walimu wapya 14,648;
- (vii) Uandaaji wa mwongozo wa mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi wa tume katika uendeshaji wa mashauri ya nidhamu na rufaa kwa walimu umekamilika; na
- (viii) Kutoa mafunzo ya kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwenye wilaya 34 za mikoa 13; wakuu wa

shule 3,066 kati ya 17,463 walishiriki mafunzo kuhusu haki, wajibu, miiko na maadili ya kazi ya ualimu ambao ni mamlaka ya nidhamu katika ngazi ya shule; wajumbe tisa (9) wa tume na wajumbe 417 wa kamati za wilaya walijengewa uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao baada ya kuteuliwa; Wajumbe 14 wa menejimenti ya tume walipatiwa mafunzo ya uongozi na utawala bora.

SEHEMU YA NNE

4.0 Makadirio ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26

139. **Mheshimiwa Spika**, Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mwaka 2025/26, yamezingatia Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; Mpango Mikakati ya Taasisi; Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyotoa wakati akilihutubia Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021; Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26; Sheria ya Bajeti Sura 439; Sera za Kisekta; Maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; malengo yaliyomo katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

4.1 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26 Fungu Namba 56

140. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutekeleza Mpango na Bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:

- (i) Kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuuji wa Madaraka kwa Umma (D by D);

- (ii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa Huduma za jamii;
- (iii) Kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi yasiyo na tija katika ngazi zote;
- (iv) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mikoa, mamlaka za serikali za mitaa na taasisi zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI;
- (v) Uratibu wa usimamizi wa mifumo ya TEHAMA;
- (vi) Kuendeleza rasilimali watu katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI;
- (vii) Kuratibu na kusimamia shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa;
- (viii) Kuratibu na kushiriki michezo ya shule za msingi (UMITASHUMTA), sekondari (UMISSETA) na mashindano ya michezo ya shule za sekondari za Afrika Mashariki;
- (ix) Kuratibu shughuli za utendaji wa kazi wa taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI;
- (x) Kuratibu na kusimamia ujenzi wa miradi ya maendeleo katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

- (xi) Kuratibu uibuaji wa miradi ya kimkakati na miradi inayopaswa kutekelezwa kwa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika mamlaka za serikali za mitaa;
- (xii) Kusimamia na kuratibu shughuli za utunzaji wa mazingira na uhifadhi wa maliasili katika mikoa na mamlaka za serikali za mitaa;
- (xiii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa afua za mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa utalii, uhamasishaji wa nishati safi ya kupikia na uendelezaji wa Biashara ya Kaboni katika mikoa na mamlaka za serikali za mitaa; na
- (xiv) Kuratibu shughuli za uendelezaji wa vijiji na miji kwenye mamlaka za serikali za mitaa.

4.2 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26 Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Na. 2

141. ***Mheshimiwa Spika***, Tume ya Utumishi wa Walimu inatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo;

- (i) Kusimamia ajira, maadili, nidhamu na maendeleo ya walimu kwa kuhakikisha walimu wanasajiliwa, kwa wale wenye sifa wanathibitishwa kazini na wanapandishwa vyeo/wanabadilishiwa vyeo kwa wakati kwa walimu wa shule za msingi na sekondari katika utumishi wa umma;

- (ii) Kufanya utafiti na kutathmini hali ya walimu nchini;
- (iii) Uwezeshaji wa matumizi ya mifumo ya TEHAMA;
- (iv) Kuboresha utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu za walimu;
- (v) Kuwajengea uwezo watumishi wa tume; na
- (vi) Kuwezesha mazingira bora ya kufanyia kazi.

4.3 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26 Mafungu 26 ya Mikoa ikijumuisha Halmashauri 184

142. **Mheshimiwa Spika**, ofisi za wakuu wa mikoa zinatarajia kutekeleza vipaumbele mbalimbali kama ifuatavyo:

- (i) Usimamizi wa masuala ya usalama;
- (ii) Uimarishaji wa utawala bora, uwajibikaji na uwazi kwa kufanya vikao vyote vya kisheria;
- (iii) Uratibu na usimamizi wa utoaji wa huduma za jamii;
- (iv) Uratibu wa uwezeshaji wananchi kiuchumi;
- (v) Uboreshaji wa mazingira ya kufanyia kazi na makazi ya viongozi na watumishi wa mikoa na wilaya;
- (vi) Uendelezaji wa rasilimaliwatu katika mikoa;

- (vii) Kusimamia na kuratibu miradi inayotekelezwa kwa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika mamlaka za serikali za mitaa;
- (viii) Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
- (ix) Kusimamia na kuratibu shughuli za utunzaji wa mazingira na uhifadhi wa maliasili katika mamlaka za serikali za mitaa;
- (x) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa afua za mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa utalii, uhamasishaji wa nishati safi ya kupikia na uendelezaji wa Biashara ya Kaboni katika mamlaka za serikali za mitaa;
- (xi) Ufuatiliaji na utatuzi wa kero na malalamiko ya wananchi; na
- (xii) Uratibu wa utekelezaji wa sera za kisekta.

143. ***Mheshimiwa Spika***, mamlaka ya serikali za mitaa zinatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

- (i) Kusimamia na kutoa huduma za jamii na shughuli za kiuchumi;
- (ii) Kusimamia na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri;
- (iii) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji;
- (iv) Kusimamia na kutekeleza miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi;

- (v) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
- (vi) Kuwezesha wananchi kiuchumi;
- (vii) Kuendeleza vijiji, miji na miji inayochipukia;
- (viii) Kuimarisha huduma za ugani na ushirika;
- (ix) Kusimamia na kuratibu shughuli za utunzaji wa mazingira na uhifadhi wa maliasili katika ngazi za msingi;
- (x) Kutekeleza afua za mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa utalii, uhamasishaji wa nishati safi ya kupikia na uendelezaji wa Biashara ya Kaboni katika ngazi za msingi;
- (xi) Kutambua na kuwapanga wafanyabiashara ndogondogo;
- (xii) Ukamilishaji wa miradi viporo iliyoanzishwa na nguvu za wananchi;
- (xiii) Kulipa madeni ya watumishi na wazabuni;
- (xiv) Kuanzisha miradi mikubwa inayotekelezwa na mapato ya ndani ya halmashauri;
- (xv) Ulipaji wa madeni na michango ya mikopo ya Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa pamoja na mkopo wa KKK; na
- (xvi) Kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji.

4.4 Makadirio ya Kodi ya Majengo, Maduhuli na Mapato ya Ndani ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri Mwaka 2025/26

144. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2025/26, Taasisi za Ofisi ya Rais - TAMISEMI, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa zinakadiria kukusanya kodi ya majengo, maduhuli na mapato ya ndani ya shilingi trilioni 1.92 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.60 iliyoidhinishwa Mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la shilingi bilioni 324.83 au asilimia 20.29. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 56.10 ni za taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, shilingi milioni 306.07 ni Maduhuli ya Mikoa na shilingi trilioni 1.68 ni za mapato ya ndani ya halmashauri (**Kiambatisho Na. 4**).

145. **Mheshimiwa Spika**, shilingi bilioni 188.96 ni Kodi ya Majengo ambayo itakusanywa na mamlaka za serikali za mitaa ambazo zimepewa uwakala wa kukusanya kodi hiyo na kuwasilisha makusanyo hayo Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

4.5 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Mafungu 28) kwa Mwaka wa Fedha 2025/26

146. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake (Fungu Na. 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) na Mafungu 26 ya Mikoa

(yakijumuisha Halmashauri 184) yanaomba kuidhinishiwa shilingi trilioni 7.83 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Mishahara ni shilingi trilioni 6.29 na Matumizi Mengineyo shilingi trilioni 1.54 yanayojumuisha shilingi trilioni 1.06 za mapato ya ndani ya halmashauri (***Kiambatisho Na. 4***).

4.6 Makadirio ya Mpango na Bajeti ya Maendeleo ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI (Mafungu 28) kwa Mwaka 2025/26

147. ***Mheshimiwa Spika***, Mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake (Fungu Na. 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) na Mafungu 26 ya Mikoa (yakijumuisha Halmashauri 184) inaomba kuidhinishiwa shilingi trilioni 3.94 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 2.49 ni fedha za ndani ikijumuisha shilingi bilioni 613.44 za mapato ya ndani ya halmashauri (***Kiambatisho Na. 4***) na shilingi trilioni 1.44 ni fedha za nje. Fedha hizi zimepangwa kutekeleza miradi na program mbalimbali.

4.7 Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Mafungu 28) kwa Mwaka 2025/26

(i) Shughuli zitakazotekelezwa kupitia Fedha za Mapato ya Ndani ya Halmashauri

148. ***Mheshimiwa Spika***, Mwaka 2025/26 Ofisi ya Rais – TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 613.44 za mapato ya ndani ya halmashauri

kwa ajili ya kuchangia utekelezaji wa shughuli za maendeleo kama ifuatavyo:

- (a) Ujenzi wa hospitali za halmashauri tatu (3) katika Manispaa ya Temeke, Jiji la Ilala na Mwaza na ukamilishaji wa hospitali moja (1) katika Manispaa ya Kahama;
- (b) Ujenzi wa vituo vya afya 28 na ukamilishaji wa vituo vya afya 72;
- (c) Ujenzi wa zahanati 32 na ukamilishaji wa zahanati 325;
- (d) Ujenzi wa majengo matatu (3) ya *x-ray* katika vituo vya afya katika Halmashauri ya Wilaya za Kibaha (2), Geita (1) na ukamilishaji majengo matano (5) katika Halmashauri ya Jiji la Tanga (2), Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni (1), Halmashauri za Wilaya ya Mbarali (1) na Mufindi (1);
- (e) Ujenzi wa wodi 15 na ukamilishaji wa wodi 49 katika vituo vya afya;
- (f) Ujenzi wa jengo la huduma za dharura katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya na ujenzi wa Hosteli moja (1) ya wahudumu wa Afya Wilaya ya Mbinga,
- (g) Ujenzi wa majengo 14 na ukamilishaji wa majengo 20 ya wagonjwa wa nje katika vituo vya afya;

- (h) Ununuzi wa vifaa na vifaa tiba;
- (i) Ujenzi wa vyumba vya madarasa 880 na ukamilishaji 1,919;
- (j) Kuanza ujenzi wa shule za msingi tisa (9) na sekondari 40 mpya na ukamilishaji wa miundombinu katika shule mpya 52 ambapo msingi 32 na sekondari 20 na ukarabati wa shule nne (4) za sekondari;
- (k) Ujenzi wa matundu ya vyoo 4,125 na ukamilishaji 1,528 katika shule za msingi na sekondari;
- (l) Ujenzi wa hosteli 10 na ukamilishaji 10, ujenzi wa mabweni 12 na ukamilishaji 52, ujenzi wa ofisi za walimu tano (5) na ukamilishaji 60, utengenezaji wa viti na meza 47,979, madawati 71,482, ujenzi wa maabara 105 na ukamilishaji 194, ukamilishaji wa maktaba 15, ujenzi wa Mabwalo manne (4) na ukamilishaji 11 na ununuzi wa vitanda 504;
- (m) Ujenzi wa barabara kilomita 1,028.02 ambapo kilomita 15.92 kwa kiwango cha lami nyepesi na kilomita 1,012.1 kwa kiwango cha changarawe, kuchonga mifereji yenye urefu wa kilomita 806.32 ununuzi wa mitambo 11 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya miundombinu ya barabara, ujenzi wa daraja moja (1), makalavati

mawili (2), vivuko 29 vya waenda kwa miguu na ujenzi wa taa za barabarani 590;

- (n) Ulipaji wa fidia kwa wanachi 504 katika maeneo yatakayotwaliwa na serikali kwa ajili ya kupisha ujenzi wa miundombinu.;
- (o) Upimaji wa viwanja 7,538, kuandaa michoro ya mipango miji na mipango kabambe, kufanya matumizi bora ya ardhi, kurasimisha makazi yaliyojengwa kiholela, kuendeleza zoezi la kuandaa anuani za makazi na ununuzi wa vifaa vya upimaji wa ardhi na utoaji wa hatimiliki 6,711;
- (p) Ujenzi wa vitega uchumi 16 na uendelezaji wa vitega uchumi 18. Baadhi ya vitega uchumi hivyo ni; ujenzi wa bandari kavu katika Jiji la Tanga, vituo vya mafuta, kituo cha kibiashara Jiji la Arusha, ununuzi wa eneo la uwekezaji na uwanja wa mpira Manispaa ya Kinondoni, ujenzi wa eneo la biashara Sinza Manispaa ya Ubungo na Manispaa ya Iringa. Ujenzi wa viwanda saba (7) na ukamilishaji wa viwanda 21, ujenzi wa machinjio matatu (3) na ukamilishaji na ukarabati wa machinjio 120, ujenzi wa minada 16 na uendelezaji wa minada 19, ujenzi wa masoko 26 na uendelezaji wa masoko 130, ujenzi wa vituo vya mabasi 32 na uendelezaji wa vituo 68 na ujenzi wa vibanda vya biashara

512 kwa ajili ya wafanyabiashara wakubwa, wakati na wadogo;

- (q) Ujenzi wa nyumba za viongozi na watumishi 80 na ukamilishaji wa nyumba 358, ununuzi wa magari 99, pikipiki 114, bajaji 27, boti 12, lori sita (6) na trekta tano (5). Ulipaji wa madeni ya wazabuni ya miaka ya nyuma, ujenzi wa ofisi za watendaji wa kata 211, vijiji 88, mitaa 78, ujenzi wa majengo mawili (2) ya utawala katika Jiji la Dodoma na Arusha, ujenzi wa vituo vya polisi vya kata 35 na uendelezaji vituo 36 na ukarabati wa majengo 69 ya utawala; na
- (r) Uanzishaji wa mashamba 188 na mashamba darasa 88 katika halmashauri, kuanzisha skimu 18 za umwagiliaji, kuimarisha huduma ya ugani kwa kutoa mafunzo kwa wakulima, wavuvi na wafugaji, kutoa mbegu tani 142,917 kwa wakulima wa mazao ya kimkakati, kugawa miche 90,508 ya mazao ya biashara kwa wakulima, ujenzi wa majosho 66, mabanio 34, ujenzi wa malambo mawili (2) katika Halmashauri ya Manispaa ya Geita na kuanzisha maeneo ya malisho kwa ajili ya mifugo.

149. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa miradi hiyo utaboresha upatikanaji wa huduma mbalimbali kwenye mamlaka za serikali za mitaa ikiwemo afya, elimu, barabara, kilimo, mifugo, uvuvi na kurahisisha

uendeshaaji wa shughuli mbalimbali za serikali na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi.

(ii) **Uratibu na Usimamizi wa Huduma za Afya ya Msingi, Ustawi wa Jamii na Lishe**

150. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 502.09 za ruzuku ya matumizi mengineyo, fedha za maendeleo za Serikali Kuu na washirika wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali.

151. **Mheshimiwa Spika**, shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:

- (a) Kuendelea na ujenzi wa hospitali za halmashauri 43;
- (b) Ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali za halmashauri 142, vituo vya afya 184 na zahanati 184;
- (c) Kutoa chanjo kwa watoto chini ya miaka mitano (5), kutoa vitamin A na madini ya chuma kwa wajawazito katika halmashauri 184, kuratibu Mkakati wa Kimataifa wa 95-95-95 (asilimia 95 ya watu wanaoishi na VVU wanajua hali zao za VVU, asilimia 95 ya watu wanaojua hali zao wanapata matibabu ya kurefusha maisha na asilimia 95 ya watu wanaopata matibabu wamevifubaza virusi hivyo) kwa lengo la

kutokomeza UKIMWI, kutoa vyandarua kwa watoto chini ya miaka mitano (5) na wajawazito katika halmashauri 184;

- (d) Kutoa huduma za lishe zilizoinishwa kwenye Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe (2020/21 - 2025/26) kwa makundi yote ya jamii wakiwemo wanawake walio katika umri wa uzazi, akinamama wajawazito na wanaonyonyesha, watoto, vijana, wanaume na wazee;
- (e) Usimamizi shirikishi wa utekelezaji wa huduma endelevu za maji na usafi wa mazingira vijijini katika mikoa 25 na halmashauri za wilaya 137 kupitia Programu ya Usafi wa Maji na Mazingira;
- (f) Usimamizi na uratibu wa utoaji wa huduma za chanjo katika halmashauri 184 kupitia Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Utoaji wa Huduma za Chanjo;
- (g) Ufuatiliaji wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya kupitia Programu ya Kuimarisha Mifumo ya Afya;
- (h) Kuratibu na kusimamia Utekelezaji wa Mafunzo Jumuishi ya Kitaifa ya Ukuaji wa Awali wa Mtoto kwa halmashauri 184;
- (i) Kuwajengea uwezo wataalamu wa ustawi wa jamii kuhusu usimamizi wa kesi za ulinzi wa mtoto katika halmashauri 184 ili kuboresha huduma za ulinzi wa watoto;

- (j) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa afua za lishe kwenye mikoa na mamlaka za serikali za mitaa, kwa kuwajengea uwezo watumishi kuhusu kupanga na kusimamia bajeti za huduma za lishe, kuwajengea uwezo watendaji wa kata na vijiji/mitaa na kutathmini utekelezaji wake;
- (k) Kuwezesha upatikanaji wa watumishi 400 wa mkataba watakaofanya kazi katika vituo vya kutolea huduma za afya, kuratibu ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya 175 (hospitali 25, vituo vya afya 50 na zahanati 100) na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma ya afya ya msingi 175 (hospitali 25, vituo vya afya 50 na zahanati 100) vitakavyokarabatiwa au kujengwa kupitia Programu ya Uwekezaji katika Afya ya Mama na Mtoto Tanzania (Tanzania Maternal Child Health Investment Programme - TMCHIP); na
- (l) Kutoa mafunzo kazini kwa watumishi wa vituo vya kutolea huduma za afya, kufanya usimamizi shirikishi katika afua za UKIMWI, kifua kikuu na malaria katika halmashauri 184 kupitia Programu ya Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund).

(iii) **Usimamizi na Uendeshaji wa Elimumsingi na Sekondari**

152. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutumia shilingi trilioni 1.44 za ruzuku ya matumizi mengineyo, fedha za maendeleo za serikali kuu na washirika wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli katika sekta ya elimu.

153. **Mheshimiwa Spika**, Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:

- (a) Ujenzi wa madarasa 8,402 kati ya hayo 8,057 ni shule za msingi na 345 ni sekondari, matundu ya vyoo 19,095, umaliziaji wa maboma ya maabara 350; mabweni 129 kwenye shule za sekondari na maboma ya madarasa 700 shule za msingi;
- (b) Ujenzi wa shule mpya 184 za sekondari, nyumba za walimu 211 (*two in one*). Kati ya hizo 184 ni za sekondari na 27 za msingi;
- (c) Ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwenye shule za sekondari 400;
- (d) Ununuzi wa vifaa na kemikali za maabara katika shule mpya 300 za sekondari;
- (e) Utoaji wa ruzuku ya Elimu Bila Ada kwa shule za msingi 18,055 na sekondari 4,905;
- (f) Ununuzi wa vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu na vifaa vya elimu ya awali katika halmashauri 184;

- (g) Uratibu na usimamizi wa shughuli za mitihani katika mikoa yote 26;
 - (h) Kutoa mafunzo endelevu ya walimu kazini (MEWAKA) kwenye shule za awali na msingi kwenye halmashauri 184;
 - (i) Kutekeleza mpango wa shule salama kwenye shule za awali na msingi 1,500;
 - (j) Kuanzisha madarasa janja (*smart classes*) saba (7) kwa ajili ya ufundishaji mubashara katika shule za sekondari saba (7) Halmashauri za Manispaa ya Mpanda moja (1), Kigoma moja (1), Sumbawanga moja (1), Shinyanga moja (1), Geita moja (1) na Halmashauri za Wilaya za Pangani moja (1), na Mbinga moja (1); na
 - (k) Kuratibu michezo ya shule za msingi (UMITASHUMTA), sekondari (UMISSETA) na mashindano ya michezo ya shule za sekondari za Afrika Mashariki (FEASSA).
- (iv) **Utawala Bora, Usimamizi wa Rasilimali, Ujenzi wa Majengo ya Utawala na Makazi ya Viongozi**

154. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 204.90 kwa ajili ya: Ununuzi wa magari ya viongozi wa mikoa, wilaya na halmashauri; Ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa miundombinu ya mikoa, wilaya, halmashauri na tarafa ikiwemo majengo ya utawala, ikulu ndogo na makazi ya viongozi.

155. ***Mheshimiwa Spika***, shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:

- (a) Ununuzi wa magari 91 ya viongozi, kati ya magari hayo, magari 6 ya Wakuu wa Mikoa ya Simiyu, Geita, Arusha, Dodoma, Ruvuma, Kagera; magari 11 ya Makatibu Tawala wa Mikoa ya Simiyu, Geita, Arusha, Dodoma, Lindi, Mara, Morogoro, Mwanza, Tabora, Tanga, Kagera; gari moja (1) la katibu tawala msaidizi Mkoa wa Lindi; magari mawili (2) ya Wakuu wa Wilaya za Temeke na Ubungo; magari 71 ya wakurugenzi wa halmashauri. Lengo la ununuzi wa magari haya ni kuongeza ufanisi katika usimamizi na utekelezaji wa shughuli za serikali katika maeneo yao ikiwemo ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na utatuzi wa kero za wananchi; na
- (b) Ujenzi wa ofisi za wakuu wa mikoa minne (4), ukarabati wa ofisi za wakuu wa mikoa 12, ukamilishaji wa Ofisi za wakuu wa mikoa minne (4); ujenzi wa ofisi za wakuu wa wilaya 31, ukamilishaji wa ofisi za wakuu wa wilaya 11, ukarabati wa ofisi za wakuu wa wilaya 26, ujenzi/ukarabati wa ikulu ndogo sita (6); ujenzi wa nyumba za wakuu wa mikoa miwili (2), ukamilishaji wa nyumba za wakuu wa mikoa minne (4), ukarabati wa nyumba za wakuu wa mikoa minne (4); ujenzi wa nyumba za makatibu tawala wa mikoa mitano (5), ukamilishaji wa nyumba za makatibu tawala

wa mikoa mitatu (3), ukarabati wa nyumba za makatibu tawala wa mikoa sita (6), ukamilishaji wa nyumba za makatibu tawala wasaidizi wanne (4), ukarabati wa nyumba za makatibu tawala wasaidizi wa mikoa minne (4); ujenzi wa nyumba za wakuu wa wilaya 20, ukamilishaji wa nyumba za wakuu wa wilaya 12, ukarabati wa nyumba za wakuu wa wilaya 26, ukamilishaji wa nyumba za makatibu tawala wa wilaya tisa (9), ukarabati wa nyumba za makatibu tawala wa wilaya 18; ukamilishaji wa ofisi za tarafa 11, ukarabati wa ofisi za tarafa 18, ukarabati wa nyumba za maafisa tarafa tatu (3); ujenzi wa majengo 16 mapya ya utawala, ukamilishaji wa majengo 85 ya utawala, ununuzi wa samani katika majengo 38 ya halmashauri; ujenzi wa nyumba moja (1) ya mkurugenzi na ukamilishaji wa nyumba 83 za wakurugenzi na ujenzi wa nyumba 46 za wakuu wa idara na ukamilishaji nyumba saba (7) za wakuu wa idara.

(v) **Ufuatiliaji na Tathmini**

156. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2025/26 Ofisi ya Rais - TAMISEMI, mikoa na halmashauri imepanga kutumia shilingi bilioni 18.57 kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini wa shughuli zitakazotekelezwa katika ngazi zote ili kubaini mafaniko na changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji na kuweka mikakati ya utatuzi wa changamoto hizo. Hii itasaidia miradi kutekelezwa

kwa ubora na kuhakikisha inakuwa na thamani ya fedha.

(vi) **Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa Majimbo ya Tanzania Bara**

157. *Mheshimiwa Spika*, Mwaka 2025/26 Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 15.99 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Majimbo ya Uchaguzi 214 ya Tanzania Bara.

(vii) **Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati**

158. *Mheshimiwa Spika*, Mwaka 2025/26 Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 44.85 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati. Kati ya fedha hizo shilingi 28.75 ni za utekelezaji wa miradi mipya 31 na shilingi bilioni 16.10 ni za miradi 19 inayoendelea.

(viii) **Ushirikishwaji wa Wananchi kupitia Mfumo wa O&OD Iliyoboreshwa**

159. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo katika ngazi za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwa kutumia Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo Ulioboreshwa. Aidha, mwaka 2025/26 mafunzo yatatolewa kwa wataalamu 184 waliopo ngazi ya kata katika kata 62 ili kujengea uwezo jamii ziweze kushiriki katika shughuli za maendeleo na kufanya mafunzo kwa vikosi kazi 1,288 katika halmashauri 184 na mikoa 26.

(ix) **Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu**

160. **Mheshimiwa Spika**, wote tunafahamu kuwa **“Kila mkopo unahitaji mpango; bila mpango ni kama safari bila ramani”** Mwaka 2025/26 shilingi bilioni 123.92 zimetengwa na mamlaka za serikali za mitaa kwa ajili ya utoaji wa mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 18.35 zitakopeshwa kupitia Mfumo wa Kibenki katika halmashauri 10 za mfano ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Siha (Uchumi Commercial Benki), Bumbuli (NMB), Itilima (NMB) na Nkasi (CRDB); Halmashauri ya Jiji la Dodoma (NMB na CRDB) na Dar es Salaam (NMB na CRDB); Halmashauri ya Mji wa Newala (NMB) na Mbulu (CRDB); Halmashauri ya Manispaa ya Songea (NMB) na Kigoma (CRDB). Aidha, shilingi bilioni 105.57 zitatolewa kupitia Mfumo wa Serikali Ulioboreshwa kwa halmashauri 174 (**Kiambatisho Na. 5**).

161. **Mheshimiwa Spika**, sehemu ya fedha hizo zitatumika kwa ajili ya utambuzi na uhamasishaji wa wananchi ili kuunda vikundi, utoaji wa mafunzo na ufuatiliaji wa vikundi kabla na baada ya kupata mikopo kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni ya 38(1) na (2) ya Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za Mwaka 2024.

(x) **Uendelezaji Vijiji na Miji**

162. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2025/26 Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 32.04 kwa ajili ya uendelezaji wa vijiji na miji.

163. **Mheshimiwa Spika**, shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:

- (a) Kukamilisha mapitio ya muundo wa Mji wa Dar es Salaam uendane na ukuaji wake kijiografia na kiuchumi ili kuwa Jiji Kuu (*Metropolitan Assembly*) lenye utawala na uendeshaaji;
- (b) Kuratibu utekelezaji wa Mpango Kabambe Jumuishi wa Jiji la Kibiashara na Uwekezaji la Kwala, Mkoa wa Pwani;
- (c) Kukamilisha mapendekezo ya rasimu ya Sera ya Maendeleo Vijijini na Mijini;
- (d) Kusimamia uendelezaji wa Miji Midogo Inayochipukia 101 na vijiji vya mfano 284 vilivyoainishwa katika kutekeleza mpango wa kuiendeleza miji ya aina hiyo;
- (e) Kuzisimamia mamlaka za serikali za mitaa kutumia Mfumo wa Taarifa za Kijiografia (*Geographical Information System - GIS*) ili ziweze kutambua hali halisi ilivyo kwa wakati husika ya uendelezaji uliopo na mali asilia zilizopo uwandani;
- (f) Kusimamia uendelezaji wa Jiji la Dodoma likiwa ndiyo makao makuu ya nchi;

- (g) Kufanya mapitio ya Mwongozo wa Utoaji wa Vibali vya Ujenzi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2018 ili kudhibiti ujenzi holela;
- (h) Kudhibiti uendelezaji wa ardhi kwa kutoa vibali vya ujenzi kupitia Mfumo wa kielektroniki wa TAUSI;
- (i) Kuwezesha ukusanyaji wa takwimu kwa mfumo wa kijiografia kwa ajili ya uimarishaji wa ukusanyaji wa mapato ya ndani;
- (j) Kuwezesha usimamizi wa uthamini wa majengo kwenye halmashauri 184;
- (k) Kuwezesha ukusanyaji wa taarifa za maeneo ya ukanda wa kijani, maeneo ya wazi na maeneo ya umma kwa mfumo wa kijiografia;
- (l) Kuwezesha upatikanaji wa leseni, michoro na picha za anga kwa ajili ya mifumo ya GIS kwenye halmashauri;
- (m) Kuwezesha usimamizi wa mazoezi ya uwandani ya uthamini na ukadiriaji wa kodi za majengo, ardhi na mabango;
- (n) Uboreshaji wa miundombinu ya masoko na mialo ya samaki katika Halmashauri za Majiji ya Mwanza na Tanga na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela; na
- (o) Utoaji wa elimu kwa makundi mbalimbali ya jamii ya Mwanza na Tanga, ujasiriamali na kutoa mikopo yenye riba nafuu kama mitaji kwa Wananchi wa Mwanza na Tanga.

(xi) **Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini
(TARURA)**

164. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutumia shilingi trilioni 1.18 kwa ajili ya ujenzi, matengenezo, ukarabati wa miundombinu ya barabara na usafiri na usafirishaji wa vijijini na mijini. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 257.03 ni za Mfuko wa Barabara, shilingi bilioni 127.50 Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, shilingi bilioni 325.77 ni za tozo ya mafuta ya petroli na dizeli ya shilingi 100 kwa lita na shilingi bilioni 423.79 ni fedha za nje.

165. **Mheshimiwa Spika**, shughuli zitakazotekelezwa ni:

- (a) Ukamilishaji wa miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami kilomita 33 katika Halmashauri za Wilaya za Iringa (Wenda – Mgama kilomita 19) na Mufindi (Mtili – Ifwagi kilomita 14);
- (b) Kuanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kilomita 33 kwa awamu ya pili katika Halmashauri za Wilaya za Handeni, Ruangwa na Mbogwe. Kazi zitakazofanyika ni ujenzi wa barabara na mitaro, uwekaji wa taa za barabarani, ujenzi wa maeneo ya kupaki bodaboda na magari ya abiria pamoja na maeneo ya waenda kwa miguu;
- (c) Matengenezo ya barabara kilomita 23,105.78 kupitia Mfuko wa Barabara, Kalavati aina ya boksi 23, makalavati aina ya mabomba ya

zege mistari 1,647, drift 2, na mifereji ya maji ya mvua mita 73,405, barabara za lami kilomita 17, barabara za changarawe kilomita 108.8 na madaraja 2. Kazi hizi zitafanyika katika wilaya 139 Tanzania Bara.

- (d) Ujenzi wa barabara kilomita 91.97 kwa kiwango cha lami, kilomita 2,621.40 za changarawe, madaraja 85, boksi kalavati 91, mitaro ya maji ya mvua mita 10,989, drift tano (5), mistari ya kalavati 666 na taa za barabarani 345 katika wilaya 139 Tanzania Bara;
- (e) Ujenzi wa barabara kilomita 252.42 kwa kiwango cha lami, kilomita 6,939.41 za changarawe, madaraja 51, boksi kalavati 336, mistari ya kalavati 1,719, drift 2, na mifereji ya maji ya mvua mita 63,836 katika wilaya 139 Tanzania Bara;
- (f) Kuendelea na ujenzi wa barabara za lami kilomita 147.50 kwenye miji 12 ya Fungu la Kwanza la Mradi wa TACTIC;
- (g) Kuendelea na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua mita 24,600;
- (h) Kuendelea na ujenzi wa masoko tisa (9) katika Majiji ya Mwanza, Mbeya, Arusha, Dodoma, na Manispaa za Songea, Ilemela, Kigoma, Tabora na Kahama;
- (i) Kuendelea na ujenzi wa stendi kuu nne (4) za mabasi katika Halmashauri za Majiji ya Arusha, Mbeya na Manispaa za Kahama na

Geita na stendi ndogo mbili (2) katika Jiji la Dodoma na Manispaa ya Morogoro;

- (j) Kuendelea na ujenzi wa maghala mawili (2) ya kuhifadhia mazao katika Manispaa za Sumbawanga na Songea;
- (k) Kuanza ujenzi kwenye Halmashauri za Miji 15 za Fungu la Pili la Mradi wa TACTIC;
- (l) Kukamilisha mchakato wa maandalizi ya Mradi wa TACTIC Fungu la Tatu katika Halmashauri za Miji 18;
- (m) Kuendelea na uboreshaji wa Bonde la Msimbazi lenye Hekta 5.7;
- (n) Kuendelea na ujenzi wa karakana ya mabasi ya mwendo kasi katika eneo la Ubungo Maziwa;
- (o) Kuendelea na ujenzi wa tuta kilomita 6.7 katika eneo la Bonde la Mto Msimbazi;
- (p) Ujenzi wa Bohari Mpya ya BRT eneo la Ubungo Maziwa;
- (q) Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya barabara awamu ya kwanza zenye jumla ya kilomita 132 katika Manispaa za Kinondoni, Ubungo, Temeke, Ilala na Kigamboni;
- (r) Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya barabara awamu ya pili ya Mradi wa DMDP zenye urefu wa kilomita 118 kiwango cha lami katika Manispaa za Kinondoni, Ubungo, Temeke, Ilala na Kigamboni;

(s) Kuwasimamia wataalamu washauri wa *Traffic Management and Parking Study* na Utafiti wa Maegesho katika eneo la kibiashara katikati ya Jiji la Dar es Salaam; na

(t) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwenye miradi yote ya maendeleo ikijumuisha miradi inayotekelezwa kupitia fedha za ndani katika ngazi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na taasisi zilizo chini yake, mikoa 26 na halmashauri 184.

(xii) **Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam**

166. **Mheshimiwa Spika**, Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam imepanga kutumia shilingi bilioni 4.83 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 4.10 kwa ajili ya Mishahara na shilingi milioni 731.21 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

167. **Mheshimiwa Spika**, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni:

- (a) Kukamilisha taratibu za ununuzi wa mtoa huduma kwa njia ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ya uendeshaji wa mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Kwanza na ya Pili;
- (b) Kuendelea na maandalizi ya usanifu na ujenzi wa miundombinu Awamu ya Tano (V)

ya Barabara za Nelson Mandela, Mbagala na Tabata -Segerea – Kigogo zenye urefu wa kilomita 26;

- (c) Kuendelea na ukarabati wa mara kwa mara wa miundombinu ya Mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT *system*) na ujenzi wa vituo mlishi (*feeder*);
- (d) Kukamilisha ufungamanishaji wa mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji nauli (*Automated Fare Collection System-AFCS*) na mfumo wa kuongozea magari (*Intelligent Transport System-ITS*) ikiwa ni sehemu ya maboresho endelevu ya huduma hii kwa wananchi waishio Dar es salaam;
- (e) Kufanya pembuzi yakinifu nne kwa ajili ya upanuzi wa miundobinu ya barabara za nyongeza za Mabasi Yaendayo Haraka za Mbagala Rangitatu – Vikindu (BRT 2) kilomita tano (5), Tegeta - Bunju (BRT 4) kilomita 13, Kimara – Kibaha (BRT1) kilomita 20 na kuunganisha BRT Awamu ya Kwanza na BRT Awamu ya Nne kupitia Barabara ya Mwai Kibaki kilomita saba 7(;) na
- (f) Kufanya utafiti na kuibua vyanzo vipya vya mapato ya ndani kwa kuendeleza maeneo ya ushoroba wa mradi (*Transit Oriented Development*) ikiwemo ujenzi wa vitega uchumi kwenye maeneo ya Mtoni kwa Aziz Ally na eneo la Kariakoo Gerezani.

(xiii) **Shirika la Masoko ya Kariakoo**

168. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2025/26 Shirika la Masoko ya Kariakoo limepanga kutumia shilingi bilioni 1.90 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 1.51 kwa ajili ya Mishahara na shilingi milioni 388.22 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

169. **Mheshimiwa Spika**, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni:

- (a) Kuboresha uendeshaji wa biashara wa kisasa kwa kutumia mifumo ya kidijitali itakayosaidia kutoa huduma bora kwa wafanyabiashara na wadau wa shirika;
- (b) Kufanya uchunguzi wa udongo pamoja na kuandaa michoro ya majengo kwa ajili ya kuendelea na uwekezaji wa miradi ya kibiashara katika eneo la Mbezi Beach Makonde na Tabata Bima;
- (c) Kuboresha utendaji wa shirika kwa kuimarisha rasilimaliwatu na kuhakikisha upatikanaji wa vitendea kazi kwa Watumishi;
- (d) Kuwajengea uwezo watumishi wa shirika kupitia mafunzo mbalimbali;
- (e) Kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato kikamilifu;
- (f) Kuimarisha mahusiano na Mamlaka ya Mapato Tanzania, Taasisi za fedha, Taasisi ya kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania,

Mamlaka ya Uthibiti wa Mbolea, Wizara ya Kilimo, Taasisi za utafiti na vyuo vya kilimo. Vyombo vya Usalama na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa; na

(g) Kuanzisha kituo cha kutolea Habari.

(xiv) **Chuo cha Serikali za Mitaa**

170. **Mheshimiwa Spika**, Chuo kimepanga kutumia shilingi bilioni 7.77 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 7.42 kwa ajili ya Mishahara na shilingi milioni 349.30 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

171. **Mheshimiwa Spika**, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni:

(a) Kudahili wanafunzi 9,300 kuanzia ngazi ya Astashahada hadi Shahada ya Kwanza;

(b) Kuanza kutoa mafunzo ya Shahada ya Kwanza ya Nyaraka na Kumbukumbu kwa kudahili wanafunzi 100 baada ya mtaala kukamilika;

(c) Kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa 40 na Taasisi tano (5) kupitia mafunzo ya muda mfupi ili kutoa huduma bora kwa wananchi;

(d) Kufanya tafiti sita (6) na machapisho 30 ya kitaaluma katika majarida mbalimbali yenye

lengo la kuboresha utendaji katika mamlaka za serikali za mitaa na wadau wengine;

(e) Kufanya ukarabati wa mabweni manne (4) ya wanafunzi na nyumba saba (7) za watumishi ikiwa ni pamoja na miundombinu ya maji na umeme ambapo shilingi milioni 575 zimepangwa kutumika; na

(f) Kuendeleza watumishi 27 katika ngazi mbalimbali za elimu. Kati ya hao, Shahada ni watano (5), Uzamili 11 na Shahada ya uzamivu 11.

(xv) **Shirika la Elimu Kibaha**

172. **Mheshimiwa Spika**, Shirika la Elimu Kibaha limepanga kutumia shilingi bilioni 9.51 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 7.94 kwa ajili ya Mishahara, shilingi bilioni 1.30 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi milioni 276 za Maendeleo.

173. **Mheshimiwa Spika**, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni:

(a) Kuendelea kutoa elimumsingi kwa wanafunzi 3,282 na elimu ya sekondari kwa wanafunzi 315;

(b) Kuboresha utoaji wa elimu kwa wahudumu wa afya 564 katika fani ya utabibu, uuguzi na ukunga; na uhudumu wa afya ngazi ya jamii kupitia Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha, sambamba na kutoa elimu ya

afya dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza kwa wananchi 500;

(c) Kutoa elimu na mafunzo ya stadi mbalimbali za ujuzi na ubunifu katika fani za umeme wa majumbani, ufundi wa magari, uundaji na uungaji vyuma, ujenzi (useremala, uashi na bomba), kilimo, mifugo, upishi, na ushonaji kwa vijana 400 kwa kozi za muda mrefu na wananchi 500 kwa kozi za muda mfupi; na

(d) Kuendelea na ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha.

(xvi) **Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

174. **Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imepanga kutumia shilingi milioni 756.26 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

175. **Mheshimiwa Spika**, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni:

(a) Kutoa mikopo kwa halmashauri zitakazokidhi vigezo vya kukopeshwa na kufanya uwekezaji kwenye taasisi za fedha ambapo shilingi bilioni 3.51 zitatumika;

(b) Kufanya ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo kwenye halmashauri zilizokopeshwa na bodi ili kukusanya marejesho ya mikopo ya shilingi bilioni 1.25;

(c) Kufanya ufuatiliaji wa ukusanyaji wa mchango wa akiba na nyongeza ya mtaji kwenye halmashauri 104 ambazo bado hazijakamilisha kuchangia

mchango kwenye bodi ili kukusanya jumla ya shilingi bilioni 2.12;

(d) Kukamilisha mapitio ya sheria ili kuboresha utendaji wa bodi; na

(e) Kukamilisha taratibu za kuhuisha muundo wa bodi ikiwa ni pamoja na kuifanya bodi iwe taasisi inayojitegemea.

(xvii) **Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2)**

176. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2025/26, tume imepanga kutumia shilingi bilioni 21.84 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 11.79 kwa ajili ya Mishahara na shilingi bilioni 8.11 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, shilingi bilioni 1.94 ni fedha za Maendeleo.

177. **Mheshimiwa Spika**, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni:

(a) Kutoa barua za ajira kwa walimu wapya 14,648;

(b) Kuhuisha Tange ya Walimu 273,736 kwenye wilaya 139 kutoka mamlaka za serikali za mitaa 184;

(c) Kuchambua taarifa za walimu 14,648 kwa ajili ya kuthibitishwa kazini, 79,777 kupandisha vyeo waliokasimiwa Mwaka 2024/25 na walimu 4,422 kubadilishiwa cheo/muundo baada ya kujiendeleza;

- (d) Kuchapisha na kusambaza Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu 14,648;
- (e) Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi za tume makao makuu; na
- (f) Kuwajengea uwezo watumishi wa tume 509 na wajumbe 9 wa tume kuhusu uendeshaji wa mashauri ya nidhamu na rufaa.

178. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kuwaelekeza waheshimiwa wakuu wa mikoa kuwasimamia wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:

- (a) Kuhakikisha ukusanyaji wa mapato unafikia malengo;
- (b) Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya afya ya msingi, elimumsingi na sekondari kulingana na mipango iliyowekwa;
- (c) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidigitali ikiwemo uwekaji na matumizi ya mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika mikoa na mamlaka za serikali za mitaa ikiwa ni pamoja na vituo vya huduma za afya na elimu;
- (d) Kuhakikisha mapato katika mikoa na mamlaka za serikali za mitaa yanakusanywa kupitia mifumo ya TEHAMA ya Serikali pamoja na kufanya ufuatiliaji wa karibu wa mifumo hiyo ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;

- (e) Mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha inatekeleza Mikakati ya Uchumi wa Buluu, nishati safi ya kupikia na mabadiliko ya tabianchi na utunzaji wa mazingira;
- (f) Mikoa na mamlaka za serikali za mitaa iendeleo kuimarisha mifumo stahimilivu na endelevu ya utoaji wa huduma bora za afya, ustawi wa jamii na lishe ili kuboresha huduma ambayo ni nguzo muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote; na
- (g) Wakuu wa mikoa na wakurugenzi wahakikishe watoto walio chini ya miaka mitano wanajiunga kwenye vituo vya jamii vya kulelea watoto wadogo mchana.

179. **Mheshimiwa Spika**, kila halmashauri itapimwa utekelezaji wa vipaumbele hivi kwa kuzingatia miradi iliyotengewa bajeti kwa Mwaka 2025/26.

180. **Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, nitumie fursa hii kuwashukuru wadau mbalimbali walioshirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kufanikisha utekelezaji wa mpango na bajeti ya 2024/25. Vilevile, ninawashukuru wadau wote ambao wametoa ahadi za kuchangia utekelezaji wa bajeti ya 2025/26 kwa mafungu 28. Wadau hao ni pamoja na: Benki ya Dunia, UNICEF, Global Fund, Twiga Barrick Tanzania, EU, JICA, KOICA, GiZ, UNCDF, CDC, SIDA, UNDP, UNFPA, UN Women, Carbon Tanzania, UNEP, WHO, AfDB,

WWF, FCDO, DANIDA, CANADA, SDC SWISS, Shirika la Korea - KOFIH, Serikali ya Shirikisho la Ujerumani, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kupitia FOCAC, *Global Facility Financing* na GAVI.

181. **Mheshimiwa Spika**, aidha, ninawashukuru viongozi wa Chama Cha Mapinduzi katika ngazi zote kwa kutekeleza wajibu wao wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 katika maeneo yao, watendaji wote ngazi za msingi bila kusahau wenyevidi wa vitongoji, vijiji na mitaa, watendaji wa mitaa na vijiji, watendaji wa kata, maafisa tarafa, wakuu wa idara na vitengo, wakurugenzi wa halmashauri, makatibu tawala wa wilaya, waheshimiwa madiwani, waheshimiwa wabunge, wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa mikoa, wakuu wa mikoa na watumishi wote wa tawala za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwa utendaji kazi wao mzuri.

182. **Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine ninawashukuru sana wananchi wa jimbo langu la Rufiji kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kitaifa na jimbo na kuniombea kila siku. Ninaahidi kuendelea kuwatumikia na kushirikiana nao kila hatua katika kuleta maendeleo ya jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

183. **Mheshimiwa Spika**, kipekee, ninaishukuru kwa dhati familia yangu kwa upendo wao, uvumilivu na maombi yao wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yangu ya kitaifa. Ninawashukuru kwa kusimama

nami katika safari hii ya kuleta maendeleo ya Taifa letu.

4.8 Makadirio ya Makusanyo ya Kodi ya Majengo, Maduhuli na Mapato ya Ndani kwa Mwaka 2025/26

184. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, taasisi zilizo chini yake, mikoa 26 ikijumuisha halmashauri 184 inaomba idhini ya kukusanya kodi ya majengo, maduhuli na mapato ya ndani ya shilingi trilioni moja, bilioni mia tisa ishirini na tano, milioni mia nane themanini na moja, mia tatu ishirini na tatu elfu, mia nne sitini na nne (1,925,881,323,464.00).

185. **Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha hizo, shilingi bilioni hamsini na sita, milioni mia moja na nane, mia moja sabini na nne elfu na sitini na nne (56,108,174,064.00) ni mapato ya ndani ya taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, shilingi milioni mia tatu na sita, sabini na tisa elfu na mia nne (306,079,400.00) ni maduhuli ya mikoa na shilingi trilioni moja, bilioni mia sita themanini, milioni mia tano na sita, mia saba sitini na nne elfu (1,680,506,764,000.00) ni za mapato ya ndani ya halmashauri. Aidha, shilingi bilioni mia moja themanini na nane, milioni mia tisa sitini, mia tatu na sita elfu (188,960,306,000.00) ni kodi ya majengo ambayo itakusanywa na mamlaka za serikali za mitaa ambazo zimepewa uwakala wa kukusanya kodi hiyo na kuwasilisha makusanyo hayo Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali **Jedwali Na. 1.**

Jedwali Na. 1: Makadirio ya Makusanyo ya Kodi ya Majengo, Maduhuli na Mapato ya Ndani kwa Mwaka 2025/26

Ofisi/Taasisi	Makadirio ya Makusanyo 2025/26
Ofisi ya Rais - TAMISEMI	188,960,306,000.00
Taasisi	56,108,174,064.00
Mikoa	306,079,400.00
Halmashauri	1,680,506,764,000.00
Jumla Kuu	1,925,881,323,464.00

4.9 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Mafungu 28) kwa Mwaka 2025/26

186. **Mheshimiwa Spika**, sasa naomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2025/26 yenye jumla ya shilingi trilioni kumi na moja, bilioni mia saba themanini na mbili, milioni mia tisa themanini na nne, mia mbili na mbili elfu (shilingi 11,782,984,202,000.00) kwa ajili ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na taasisi zilizo chini yake (Fungu Na. 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) na Mafungu 26 ya Mikoa (yakijumuisha Halmashauri 184).

187. **Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha zinazoombwa, shilingi trilioni saba, bilioni mia nane thelathini na sita, milioni mia moja arobaini, mia saba na nane elfu (shilingi 7,836,140,708,000.00) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yanayojumuisha Mishahara shilingi trilioni sita, bilioni mia mbili tisini na mbili, milioni mia tano hamsini na saba, mia sita arobaini na nane elfu (shilingi 6,292,557,648,000.00) na Matumizi Mengineyo shilingi

trilioni moja, bilioni mia tano arobaini na tatu, milioni mia tano themanini na tatu na sitini elfu (shilingi 1,543,583,060,000.00) ikijumuisha shilingi trioni moja, bilioni sitini na saba, milioni sitini na tano, mia tatu ishirini na nane elfu (shilingi 1,067,065,328,000.00) za mapato ya ndani ya halmashauri.

188. **Mheshimiwa Spika**, shilingi trilioni tatu, bilioni mia tisa arobaini na sita, milioni mia nane arobaini na tatu, mia nne tisini na nne elfu (shilingi 3,946,843,494,000.00) zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo shilingi trilioni mbili, bilioni mia nne tisini na nane, milioni mia tisa thelathini na moja, mia nne sabini na sita elfu (shilingi 2,498,931,476,000.00) ni fedha za ndani, ikijumuisha shilingi bilioni mia sita kumi na tatu, milioni mia nne arobaini na moja, mia nne thelathini na sita elfu (613,441,436,000.00) za mapato ya ndani ya halmashauri na shilingi trilioni moja, bilioni mia nne arobaini na saba, milioni mia tisa kumi na mbili na kumi na nane elfu (shilingi 1,447,912,018,000.00) ni fedha za nje **Jedwali Na. 2**.

Jedwali Na. 2: Muhtasari wa Makadirio ya Mpango wa Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI Mwaka 2025/26

Maelezo	Makadirio ya Bajeti 2025/26
Matumizi ya Kawaida	
Mishahara	
Makao Makuu	13,460,722,000.00
Taasisi	72,506,144,000.00
Tume ya Utumishi wa Walimu	11,792,001,000.00
Mikoa	90,577,132,000.00
Halmashauri	6,104,221,649,000.00
Jumla ndogo	6,292,557,648,000.00
Matumizi Mengineyo	
Makao Makuu	23,582,719,500.00
Taasisi	3,525,430,500.00
Tume ya Utumishi wa Walimu	8,110,307,000.00
Mikoa	119,332,530,000.00
Halmashauri – SK	321,966,745,000.00
Halmashauri – OS	1,067,065,328,000.00
Jumla Ndogo	1,543,583,060,000.00
Jumla Matumizi ya Kawaida	7,836,140,708,000.00
Matumizi ya Maendeleo	
Ndani	
Makao Makuu	6,724,914,000.00
Taasisi	710,592,035,000.00
Tume ya Utumishi wa Walimu	264,215,000.00
Mikoa	117,058,250,000.00
Halmashauri – SK	1,050,850,626,000.00
Halmashauri – OS	613,441,436,000.00
Jumla Ndogo	2,498,931,476,000.00
Nje	
Makao Makuu	144,441,979,794.00
Taasisi	423,798,057,206.00
Tume ya Utumishi wa Walimu	1,678,508,000.00
Mikoa	57,272,703,000.00
Halmashauri	820,720,770,000.00
Jumla Ndogo	1,447,912,018,000.00
Jumla Maendeleo	3,946,843,494,000.00
Jumla Kuu	11,782,984,202,000.00

SK - Serikali Kuu

OS - *Own Source*

189. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na hotuba hii, yapo majedwali ambayo yamefafanua kwa kina makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa ajili ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na taasisi zilizo chini yake (Fungu Na. 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) na mafungu 26 ya mikoa (yakijumuisha halmashauri 184).

190. **Mheshimiwa Spika**, ninapohitimisha hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ninaomba tusimame pamoja si tu kama viongozi wa leo, bali kama warithi wa kesho tunaojenga Tanzania mpya kwa misingi ya uwajibikaji, ushirikishwaji na maendeleo yanayogusa maisha ya kila mtanzania kuanzia mjini hadi vijijini.

191. **Mheshimiwa Spika**, leo hii tumewasilisha si tu makadirio ya mapato na matumizi, bali tumeweka mbele yetu dira ya matumaini, ramani ya maendeleo na ahadi ya uongozi unaowajibika.

Kama alivyoandika Nelson Mandela:

“Education is the most powerful weapon which you can use to change the world.”
Tumewekeza katika elimu kwa watoto wetu wote, bila ubaguzi.

Na Kama alivyosema John F. Kennedy:

“Let us not seek the Republican answer or the Democratic answer, but the right answer.” TAMISEMI haitafuti sifa ya kisiasa, tunatafuta suluhisho sahihi kwa maisha ya mtanzania wa kawaida.

Na kama alivyosema Mwalimu Julius Kambarage Nyerere: ***“Maendeleo Hayataletwa na Mtu Mmoja. Maendeleo ni Kazi ya Pamoja.”*** Na hivyo, kwa kauli moja, tunatoa wito kwa mikoa, mamlaka za serikali za mitaa na wananchi wote: tushirikiane, tusonge mbele kwa mshikamano.

192. ***Mheshimiwa Spika***, kwa dhamira hii, na kwa imani kubwa katika maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunawasilisha bajeti hii kama zana ya kazi, dira ya matumaini na silaha ya mapinduzi ya kiutawala, kiuchumi na kijamii.

Kwa hiyo, tunasema kwa ujasiri mkubwa:

"TAMISEMI – Ndiyo Msingi wa Maendeleo Endelevu!"

“Kila Shilingi ina Jukumu, Kila Kiongozi ana Wajibu na Kila Mwananchi ana Nafasi!”

193. ***Mheshimiwa Spika***, hotuba hii inapatikana pia kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambayo ni www.tamisemi.go.tz.

194. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kutoa hoja.

Kiambatisho Na. 1

Orodha ya Shule za Sekondari za Serikali zenye Mchepuo wa Elimu ya Ufundi/Amali

S/N	Name of School	Region	District	Vocational Programmes Applied by Secondary Schools	Approved Curricula for Vocational Programmes
1	Korogwe Girls Secondary School	Tanga	Korogwe	Agriculture	Horticulture
					Field Crop Production Attendant
					Animal Health and Production
				Home Economics	N/A
				Food and Nutrition	Food Production
				Textile and Dress Making	Designing, Sewing and Cloth Technology
2	Bwiru Boys Secondary School	Mwanza	Ilemela	Computer Programming	Computer Programming
				Electrical Installation	Electrical Installation
				Refrigeration and	Refrigeration and Air

S/N	Name of School	Region	District	Vocational Programmes Applied by Secondary Schools	Approved Curricula for Vocational Programmes
				Air Condition	Conditioning
				Designing, Sewing Cloth	Designing, Sewing and Cloth Technology
				and Technology	
				Computer Graphics and Design	Computer Graphics Designing
3	Chang'ombe Secondary School	Dar-es-Salaam	Temeke	Theatre Arts	Theatre Arts
4	Chief Sarwatt Secondary School	Manyara	Mbulu	Track Events	Track Event
				Ball Games	N/A
				Athletics	N/A
5	Morogoro Secondary School	Morogoro	Morogoro	Foot Ball	Football
				Net Ball	Netball
				Volley Ball	N/A
				Tennis	N/A

S/N	Name of School	Region	District	Vocational Programmes Applied by Secondary Schools	Approved Curricula for Vocational Programmes
6	Msangano Secondary School	Songwe	Momba	Animal Health and Production	Animal Health and Production
				Agriculture	Field Crop Production
					Horticulture
7	Mtwara Technical Secondary School	Mtwara	Mtwara	Carpentry and Joinery	Carpentry, Joinery and Metal Works
				Electrical Installation	Electrical Installation
				Masonry and Bricklaying	Solar Power Installation
				Welding and Metal Fabrication	Welding and Metal Fabrication
8	Musoma Technical Secondary School	Mara	Musoma	Aut Electric	Auto - electric
				Electrical Installation	Electrical Installation

S/N	Name of School	Region	District	Vocational Programmes Applied by Secondary Schools	Approved Curricula for Vocational Programmes
				Refrigeration and Air Conditioning	Refrigeration and Air Conditioning
				Solar System Installation	Solar Power Installation
				Welding and Metal	
				Fabrication	Welding and Metal Fabrication
9	Nkowe Secondary School	Lindi	Ruangwa	Football	Football
				Netball	Netball
10	Iyunga Secondary School	Mbeya	Mbeya	Electrical	Electrical Installation
				Installation	
				Carpentry and Joinery	Carpentry, Joinery and Metal Works
				Metal Works	Painting and Sign Writing
				Computer Programming	Computer Programing

S/N	Name of School	Region	District	Vocational Programmes Applied by Secondary Schools	Approved Curricula for Vocational Programmes
				Masonry and Bricklaying	Masonry and BrickLaying
11	Matola Secondary School	Njombe	Njombe	Foot Ball	Football
				Basket Ball	Netball
				Net Ball	Event Track
				Volley Ball	N/A
				Hand Ball	N/A
				Tennis	N/A
				Spear	
				Throwing/Javelin Throw	N/A
				Athletics	N/A
				Rugby	N/A
12	Mwadui Technical Secondary School	Shinyanga	Kishapu	Welding and Metal Fabrication	Welding and Metal Fabrication
				Fitting and Tuner Mechanics	Fitting and Tuner Mechanics

S/N	Name of School	Region	District	Vocational Programmes Applied by Secondary Schools	Approved Curricula for Vocational Programmes
				Foundry	Motor Vehicle Mechanics
				Electrical Installation	Electrical Installation
				Electronics and Communication	Carpentry, Joinery and Metal Works
				Building Construction	Masonry and BrickLaying
				Architecture	Painting and Sign Writing
13	Mafiga Secondary School	Morogoro	Morogoro	Animal Health and Production	Animal Health and Production
				Horticulture	Horticulture
				Field Crop Production	Field Crop Production
14	Kibasila Secondary School	Dar-es-Salaam	Temeke	Textile and Dress Making	Designing, Sewing and Cloth Technology
				Food and Nutrition	Acting
				Home Economics	N/A
				Physical	N/A

S/N	Name of School	Region	District	Vocational Programmes Applied by Secondary Schools	Approved Curricula for Vocational Programmes
				Education	
15	Uwemba Secondary School	Njombe	Njombe	Horticulture Production	Horticulture
				Field Crop Production	Field Crop Production Attendant
				Animal Health and Production	Animal Health and Production
16	Tanga Technical Secondary School	Tanga	Tanga	Electrical Installation	Electrical Installation
				Solar System Installation	Solar Power Installation
				Welding and Metal Fabrication	Welding and Metal Fabrication
				Masonry and Bricklaying	Masonry and Bricklaying
				Fitter Mechanics	Carpentry, Joinery and Metal Works
				Computer Programming and	Computer Programming

S/N	Name of School	Region	District	Vocational Programmes Applied by Secondary Schools	Approved Curricula for Vocational Programmes
				Designing	
				Motor Vehicle Mechanics	Motor Vehicle Mechanics
17	Darajani Secondary School	Kilimanjaro	Moshi	Music Performance	Music Performance
				Theatre Arts	Acting
18	Pamba Secondary School	Mwanza	Nyamagana	Food Production	Food Production
				Food and Beverages Services and Sales	Food and Beverage Sales and Services
19	Ukombozi Secondary School	Tabora	Urambo	Foot Ball	Football
				Net Ball	Netball
20	Kigoma Secondary School	Kigoma	Kigoma	Foot Ball	Football
				Net Ball	Netball

S/N	Name of School	Region	District	Vocational Programmes Applied by Secondary Schools	Approved Curricula for Vocational Programmes
21	Chato Technical Secondary School	Geita	Chato	Motor Vehicle Mechanics	Motor Vehicle Mechanics
				Masonry and Bricklaying	Masonry and BrickLaying
				Electrical Installation	Electrical Installation
				Solar System Installation	Solar Installation
				Motorcycle Mechanics	Motorcycle and Tricycle Mechanics
22	Mbeya Secondary School	Mbeya	Mbeya	Physical Education	Music Performance
				Fine Arts	Acting
23	Dar es Salaam Secondary School	Dar es Salaam	Ilala	Design, Sewing and Cloth Technology	Design, Sewing and Cloth Technology
				Handloom Weaving	Handloom Weaving
24	Moshi Technical	Kilimanjaro	Moshi	Building	Masonry and BrickLaying

S/N	Name of School	Region	District	Vocational Programmes Applied by Secondary Schools	Approved Curricula for Vocational Programmes
	Secondary School			Construction	
				Architectural Drawings	Leather Goods and Footwear Production
				Civil Engineering Survey	Masonry and BrickLaying
				Masonry and Bricklaying	Computer Graphics and Design
				Woodwork and Painting Engineering	Carpentry, Joinery and Metal Works
				Electrical Engineering	Computer Graphics and Design
				Electronics Engineering	N/A
				Electrical Installation	Electrical Installation
				Electrical Drafting	N/A
				Electronics Drafting	N/A
				Mechanical	Motorcycle and Tricycle

S/N	Name of School	Region	District	Vocational Programmes Applied by Secondary Schools	Approved Curricula for Vocational Programmes
				Engineering	Mechanics
				Engineering Drawings	N/A
				Manufacturing Engineering	N/A
				Automotive Engineering	Motor Vehicle Mechanics
25	Iringa Girls Secondary School	Iringa	Iringa	Food Production	Food Production
				Food and Beverage Sales and Services	Food and Beverage Sales and Services
26	Ifunda Technical Secondary School	Iringa	Iringa (R)	Electrical Installation	Electrical Installation
				Solar Power Installation	Solar Power Installation
				Plumbing and Pipe Fitting	Plumbing and Pipe Fitting
				Auto Electric	Auto Electric

S/N	Name of School	Region	District	Vocational Programmes Applied by Secondary Schools	Approved Curricula for Vocational Programmes
				Wood Processing	Wood Processing
27	Arusha Day	Arusha	Arusha	Designing, Sewing and	Designing, Sewing and Cloth Technology
				Cloth Technology	
					Handloom Weaving
28	Usangi Day Secondary School	Kilimanjaro	Usangi	Designing, Sewing and Cloth Technology	Designing, Sewing and Cloth Technology

Mwenendo wa Bajeti na Makusanyo Halisi ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri Mwaka 2020/21 hadi Machi, 2024/25

Na.	Mkoa/Halmashauri	2020/21		2021/22		2022/23		2023/24		2024/25	
		Makadirio	Mapato Halisi	Makadirio	Mapato Halisi	Makadirio	Mapato Halisi	Makadirio	Mapato Halisi	Makadirio	Mapato Halisi hadi Mwezi Machi, 2025
	Katavi										
1	Mpanda MC	2,627,606,000	2,673,539,958.43	3,577,000,000	3,460,508,782.76	3,579,400,000	3,633,105,491	3,937,340,000	4,111,865,404.00	5,241,761,500.00	3,921,026,026.99
2	Tanganika DC	3,194,167,656	2,939,644,693.55	4,448,338,801	4,452,617,529.98	6,273,421,124	9,523,221,307	6,532,409,650	7,902,866,837.31	9,964,980,450.00	9,697,117,997.02
3	Nsimbo DC	1,247,386,800	1,238,389,525.41	1,191,000,000	1,421,815,379.66	1,327,189,000	1,526,453,526	1,392,000,000	2,256,958,838.30	1,996,568,200.00	2,072,065,624.24
4	Mlele DC	869,043,900	1,004,142,178.51	957,000,000	1,774,087,420.79	1,569,791,950	1,677,928,561	2,177,920,000	2,082,797,107.60	2,601,837,240.00	1,932,030,646.10
5	Mipimbiwe DC	1,376,595,000	1,870,591,648.75	1,973,554,176	2,540,837,090.99	1,768,800,000	2,346,779,192	2,181,000,000	2,911,786,900.61	3,224,000,000.00	2,298,550,940.86
	Jumla ndogo	9,314,739,364	9,726,308,005	12,146,892,577	13,649,866,204	14,516,602,074	18,707,488,077	16,220,669,650	19,266,275,086	23,029,147,390	19,920,791,235
	Sinuiyu										
6	Bariadi TC	2,755,744,743	2,418,138,036.54	2,924,000,000	3,018,493,009.35	3,456,400,000	2,914,417,168	3,370,374,000	3,109,152,035.18	3,759,760,874.90	2,086,937,273.22
7	Bariadi DC	1,759,350,000	1,743,728,071.10	1,851,000,000	2,044,130,711.57	2,179,096,460	2,014,798,036	2,261,664,836	2,242,354,104.88	2,525,309,900.00	1,948,470,037.00
8	Maswa DC	3,395,561,002	2,263,752,754.20	2,777,000,000	2,841,640,408.33	4,106,681,948	3,602,442,448	4,251,133,753	3,377,309,076.54	4,251,133,999.71	2,698,565,087.29
9	Meatu DC	2,476,736,848	2,586,397,661.08	2,574,000,000	2,745,041,807.39	2,831,400,000	3,084,022,717	2,930,499,000	3,250,502,599.33	3,734,987,600.00	2,913,896,910.89
10	Busega DC	2,345,145,305	1,461,954,993.58	2,064,000,000	2,042,663,322.60	2,270,400,000	2,012,002,138	2,349,864,000	2,201,704,758.53	2,517,098,350.00	1,958,958,461.04
11	Ililima DC	1,434,558,633	958,479,191.79	1,487,000,000	1,347,444,780.79	1,635,700,000	1,758,346,905	1,692,949,500	1,819,648,544.82	2,021,670,470.00	1,485,369,644.23
	Jumla ndogo	14,167,096,550	11,432,450,708	13,677,000,000	14,039,414,040	16,479,678,408	15,386,029,411	16,856,485,089	16,000,671,119	18,809,961,225	13,092,197,414
	Njombe										
12	Njombe TC	6,704,334,000	8,778,571,111.65	8,137,412,513	8,473,310,666.44	7,773,619,280	8,185,249,751	9,378,952,411	8,932,486,189.44	9,533,473,751.00	8,233,321,683.84
13	Makambako TC	2,878,062,000	2,862,861,147.43	3,238,000,000	3,074,135,456.35	2,888,070,000	3,210,219,800	4,047,520,000	3,839,979,181.08	4,068,000,000.00	2,937,281,090.18
14	Njombe DC	2,776,998,200	3,541,785,372.49	3,443,600,000	3,969,289,407.91	3,131,475,000	3,112,802,590	3,363,735,800	3,931,387,490.52	6,132,189,436.00	3,610,315,866.99
15	Ludewa DC	1,896,599,231	1,552,360,476.15	2,237,000,000	2,323,981,840.68	2,460,700,000	2,286,919,054	3,588,309,100	2,899,063,345.20	3,718,177,000.00	2,904,800,815.30
16	Makete DC	2,441,877,000	2,738,358,431.34	2,987,000,000	3,888,132,651.45	3,000,320,000	3,610,655,244	4,087,000,000	4,162,741,719.32	3,785,142,000.00	3,616,925,812.19
17	Wangingombe DC	3,332,136,800	3,198,180,620.10	4,189,000,000	4,186,701,020.13	4,387,900,000	4,462,826,399	5,865,981,000	5,310,176,943.29	5,141,681,238.91	5,103,069,786.36
	Jumla ndogo	20,030,007,231	22,672,117,159	24,222,012,513	25,915,551,043	23,642,084,280	24,868,672,839	30,291,498,311	29,075,834,869	32,378,663,426	26,405,715,055
	Geita										
18	Geita MC	10,511,616,818	10,331,917,302.28	10,254,000,000	9,024,149,589.59	12,180,500,000	12,370,288,933	14,043,539,070	14,765,049,058.71	19,965,455,260.00	14,588,511,703.82
19	Geita DC	4,078,343,000	4,920,258,658.37	5,168,000,000	5,186,022,221.22	5,135,900,000	6,312,408,413	6,774,614,317	7,326,743,444.14	8,348,128,909.52	7,321,024,992.40
20	Bukombe DC	1,945,991,292	1,556,458,666.62	2,347,000,000	2,283,111,563.77	2,663,200,000	2,698,769,856	2,993,791,335	3,232,616,659.18	3,417,000,000.00	2,555,426,126.24
